# UKRISTO

## SAFARI KUTOKA HAKIKA

## KUELEKEA KWENYE UBUNIFU

**MWANDISHI:**
**HADHRAT MIRZA TAHIR AHMAD**

**MFASIRI:**
**JAMIL R. RAFIQ**

***Ukristo - Safari kutoka Hakika kuelekea kwenye Ubunifu***
***Mtunzi: Hadhrat Mirza Tahir Ahmad***
***Kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya katika Islam.***

| | | |
|---|---|---|
| Chapa ya kwanza: | 1994, | Uingereza |
| Chapa ya pili: | 1996, | Uingereza |
| Chapa ya tatu: | 1997, | Uingereza |
| Tafsiri ya Kiswahili: | Des. 1999, | Tanzania - Nakala 3000 |

Idhini ya kunakili: Islam International Publications Ltd.

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Tanzania
S. L. P. 376
Dar es Salaam

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
S. L. P. 376
Dar es Salaam.
Tanzania

**Haki zote zimehifadhiwa.**
Sehemu yoyote ya kitabu hiki hairuhusiwi kunukuliwa au kuhifadhiwa kwa njia yoyote, mfano kivuli (photocopying) kanda za sauti au njia yoyote ile itakayotumiwa kwa kunakili au kuhifadhi bila ya ruhusa ya waenezaji.

*Habari za Mwandishi*

## HADHRAT MIRZA TAHIR AHMAD

Hadhrat Mirza Tahir Ahmad, alizaliwa tarehe 18 Desemba 1928 huko Qadian, India. Yu Khalifa wa Nne wa Masihi Aliyeahidiwa. Yeye ni kiongozi wa kiroho na msimamizi wa shughuli za Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, na mjukuu wa mwanzilishi wa Jumuiya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Wadhifa rasmi wa Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ni: Hadhrat Khalifatul Masih IV - Khalifa wa nne wa Masihi Aliyeahidiwa.

## NENO LA MFASIRI

Hadhrat Khalifatul-Masih IV, Kiongozi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya , aliniamuru kukifasiri kitabu chake cha Kiingereza "CHRISTIANITY- A Journey from facts to fiction" kwa lugha ya Kiswahili. Kwa baraka za maombi yake Mwenyezi Mungu amenisaidia na ameniwezesha kutimiza kazi hii kubwa sana. Kitabu hiki naona alikiandika Khalifa wetu Mtukufu kwa msaada maalum wa Allah. Ametumia kipawa chake alichojaaliwa na Mwenyezi Mungu kwa njia iliyo bora sana. Ni kitabu cha ajabu kinacholeta hoja imara sana kuhakikisha ukweli hadi kupenya rohoni. Sidhani kwamba mtu baada ya kukisoma kwa uangalifu anaweza kushindwa kutambua uhakika wa mambo kumhusu Yesu. Ni kazi ya kitaalamu inayoonekana katika kurasa za kitabu hiki. Mungu na ampe Khalifa wetu malipo bora kabisa ya huduma hii njema.

Naweka mbele ya wasomaji wetu wajuao Kiswahili tafsiri hii kwa kutegemea ya kwamba wataisoma kwa makini na kunufaika nayo.

Jamil R. Rafiq

**YALIYOMO**

UTANGULIZI. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

1. UANA WA YESU KRISTO 7
Msingi wa Kisayansi wa uzazi. . . . . . . . . . . 7
Je, mwana halisi wa Mungu anawezekana . . . . . . 9
Hermaphroditism . . . . . . . . . . . . . . . . 11
Parthenogenesis. . . . . . . . . . . . . . . . . 11
Miujiza ni nini? . . . . . . . . . . . . . . . . . 12
Je, Yesu yu Mwana wa Mungu? . . . . . . . . . . 14

2. DHAMBI NA KAFARA 19
Kafara kwa mwanadamu . . . . . . . . . . . . . 20
Dhambi ya Adamu na Hawa . . . . . . . . . . . 21
Mateso ya binadamu yaendelea . . . . . . . . . . 24
Dhambi ya kurithiwa . . . . . . . . . . . . . . 26
Kuhamishwa kwa dhambi . . . . . . . . . . . . 28
Adhabu yaendelea kutolewa. . . . . . . . . . . . 30
Uadilifu na Msamaha . . . . . . . . . . . . . . 36
Yesu hawezi kuwa kafara. . . . . . . . . . . . . 40
Kutoa dhabihu pasipo kupenda . . . . . . . . . . 41
Nani alitolewa kuwa dhabihu?. . . . . . . . . . . 45
Mashaka ya Yesu . . . . . . . . . . . . . . . . 46
Je, Mungu Baba naye alisumbuka . . . . . . . . . 48
Adhabu ya Motoni . . . . . . . . . . . . . . . 49
Kujitoa na kufurahia kiroho . . . . . . . . . . . 50
Maana ya kifo kulingana na Yesu . . . . . . . . . 51
Adhabu ya kiasi kwa dhambi isiyo ya kiasi . . . . . 53
Kafara ilileta badiliko gani? . . . . . . . . . . . . 54

3. KAZI YA ROHO MTAKATIFU 56
Ushirikiano wa Roho Mtakatifu katika uumbaji. . . . 57
Siri ama hitilafu . . . . . . . . . . . . . . . . 60

4. KUSULUBIWA 63
Ishara ya Yona . . . . . . . . . . . . . . . . . . 65
Ahadi ya Yesu kwa nyumba ya Israeli . . . . . . . 67
Mambo yahusuyo tukio la msalaba . . . . . . . . . . 68

5. KUHUIKA AU KUFUFUKA 78
Maneno makali dhidi ya Watukufu . . . . . . . . . 87
Kupaa kwake . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 91
Ilitendeka nini kwa mwili wa Yesu? . . . . . . . . . 92
Maoni ya Waislamu Waahmadiyya . . . . . . . . . 96
Mifano ya kuponea chupuchuppu . . . . . . . . . . 98

6. UTATU 101
Uhusiano wa nafasi tatu zenyewe kwa zenyewe. . . . . 102
Hali au jiha mbalimbali za nafsi moja . . . . . . . . 103
Nafsi mbalimbali zikishirikiana katika umilele . . . . 104
Nafsi mbalimbali zenye sifa tofauti kabisa. . . . . . 108
Nafsi tofauti zenye sifa zifananazo zilizo sawa . . . . 113

7. MAGEUZI YENYE KUENDELEA YA UKRISTO 116
Wafuasi wa kwanza wa Yesu . . . . . . . . . . . . 116
Kazi ya Mtakatifu Paulo . . . . . . . . . . . . . . 119
Uhakika wa Yesu . . . . . . . . . . . . . . . . . 120
Kuendelea Dini . . . . . . . . . . . . . . . . . . 123
Upeo wa mwisho wa maendeleo ya dini . . . . . . . 124

8. UKRISTO KATIKA ZAMA HIZI . . . . . . . . . . 127
Ukristo na ukoloni. . . . . . . . . . . . . . . . . 127
Ujaji wa Yesu Kristo mara ya pili . . . . . . . . . . 131
Masihi Aliyeahidiwa. . . . . . . . . . . . . . . . 137
Mwisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 144

NYONGEZA I . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 149
NYINGEZA II. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 151

## UTANGULIZI

Dhati ya Yesu ni ya muhimu sana kwa ulimwengu wa kisasa. Umuhimu wake haukomei ulimwengu wa Kikristo pekee, bali unaenea hadi kwa dini nyingi pia mashuhuri kama vile dini ya Kiyahudi na Islam. Kama dini hizo zenye nguvu zikielewana kuhusu uhakika wa dhati ya Yesu, ujaji wake wa mara ya kwanza na ule wa mara ya pili, hapo bila shaka uelewano huo utatatua matatizo mengi yanayowakabili wanadamu katika zama hizi. Kwa bahati mbaya mambo ya msingi ya maisha ya Yesu, shabaha yake, nadharia na dhati yake vimeeleweka visivyo kabisa. Katika kufahamu mambo hayo, dini hizo zinazozana vikali sana zenyewe kwa zenyewe hata kwamba ushindani mkali unazuka baina yao. Tunapochunguza hakika ya tukio la msalaba na kutafakari yale yaliyotukia na kwa nini yalitukia na pia katika wokovu na hekima yake, tunapata maelezo yanayopinzana kutoka njia tofauti za zamani. Nimechagua kutumia mantiki pekee kwa kuzungumzia swala hilo. Naamini ya kwamba hilo ndilo jukwaa lililo sawa kwa wote linaloweza kutumiwa kwa maongezi yafaayo. La sivyo, majadiliano yoyote juu ya msingi wa maandiko pamoja na maelezo ya aina tofauti yataelekeza kwenye mgogoro wa mabishano ambao kutoka nje yake kutakuwa vigumu.

Miaka elfu mbili imekwisha pita, hata hivyo kwa msingi wa maandiko peke yake hakuna suluhisho ambalo litakubaliwa na wote lililokwisha fikiwa hadi sasa. Kiini cha tatizo ni tegemeo la baadhi ya maandiko ambayo yanapinzana yenyewe kwa yenyewe. Pia matatizo makubwa yamejitokeza kwa kukua polepole kutokana na kutoelewana kulikoizunguka historia ya Yesu Kristo. Mtazamo wa picha ya kihistoria kama kawaida huelekea kutiwa

ukungu na hufifia. Kwa vyovyote muda wa miaka elfu mbili kupita si kikwazo cha kawaida kwa kufahamu matukio yaliyotukia zama za uhai wa Yesu. Mantiki ya binadamu na akili yake zikisaidiwa na mwanga wa ujuzi wa elimu ya sayansi hazitegemei imani ama rangi au dini ya mtu. Bali ziko sawa kwa watu wote na dini zote. Ni mantiki peke yake inayoweza kutupatia msingi kwa kuleta umoja wa fikra.

Nitajaribu kutathmini tatizo hili kwa njia mbalimbali. Hebu nianze kwa kuuchunguza Ukristo jinsi wanavyoufahamu Wakristo wenyewe na kisha kuuchanganua kwa kuuangalia na hadubini ya kiakili na hoja. Lakini sina budi kusisitiza ya kwamba simaanishi kwa vyovyote kutokuwa na heshima kwa Wakristo ama Yesu Kristo. Nikiwa Mwislam ni nguzo ya imani yangu kumwamini Yesu Kristo na kumkubali kwamba yu Nabii wa Mungu mwenye shani na utukufu, aliyekuwa na daraja la pekee baina ya Manabii wa Kiisraeli. Lakini pale ukweli unapoamuru kwa haki na busara, akili na fahamu ya binadamu, mtu hawezi kujizuia kusahihisha fikra zake kuhusu Ukristo. Sina shabaha ya kuleta mfarakano baina ya Wakristo na Kristo, bali napenda kuwasaidia Wakristo kusogelea karibu zaidi uhakika kumhusu Yesu Kristo na kujitenga mbali na hadithi zilizobuniwa kumhusu yeye.

Zama zinaweza kupotoa hakika na kuigeuza kuwa hadithi na ngano zisizo za kweli. Athari ya hadithi hizo za kubuniwa humpeleka mtu mbali na hakika halisi za maisha. Matokeo yake ni kwamba imani inakuwa mawazo ya kubuni tu, yasiyo ya kweli, yasiyo sawa. Ambapo imani ya kweli inayo asili yake katika mambo na matukio ya kweli ya kihistoria, ni ya hakika halisi na ina nguvu ya kutosha kuleta mabadiliko katika jamii ya binadamu. katika jitihada ya kufahamu imani ya kweli na mafunzo hasa ya Yesu, ni jambo la muhimu kabisa kuchuja uhakika kutoka na ngano za kubuniwa. Kutafuta ukweli ndiyo shabaha hasa ya zoezi hili lote. Natumai mtaniwia radhi na kufahamu kwamba simaanishi kudharau imani ya mtu ama kuchochea hisia zake.

Uchunguzi wa kina ni jambo la muhimu ili kuulinda ulimwengu wa Kikristo kutokana na bahati mbaya ya maanguko ya khulka, hali ambayo imekuwa vigumu kwa Ukristo kuibadili. Sawa na uchunguzi wangu, kijana wa zama hizi haraka sana anaendelea kupoteza imani yake juu ya Mungu. Kulikuwa na wakati ambapo wanasayansi walianza kwenda mbali na Mungu kwani walifikiri ya kwamba fikra za Kiyahudi na Kikristo kuhusu maumbile ya asili zilizoelezwa katika Agano la Kale na Agano Jipya hazikuwa sahihi. Ujuzi wa ulimwengu na maumbo ya kimbingu na vile vilivyo mbali na hayo jinsi ulivyoelezwa katika Biblia ni kinyume kabisa na uvumbuzi wa kisayansi uliofanyika tangu kuanzia zama za kufufuka Elimu na Maarifa Ulaya ( mwaka 1300- 1600 A.D ). Tofauti hizo zikaendelea kukua kati yao kadri sayansi ilivyoendelea kusonga mbele na ujuzi wa mtu kutambua hali ya asili ya ulimwengu ulipopata mabadiliko ya kimapinduzi. Habari hiyo pamoja na sababu nyinginezo zikaanzisha miongoni mwa vikundi vya wanataaluma maelekeo ya hatari ya kutomwamini Mungu. Baadae elimu ilipoenea huko na huko vyuo vikuu na makao ya wataalamu yakageuka kuwa mwahali mwa kuzalisha imani ya kuwa hakuna Mungu. Mashaka ya maarifa ya Kiyahudi na ya Kikristo kuhusu ulimwengu yalikuwa ni kwamba Neno la Mungu likapingana na kitendo cha Mungu. Hoja dhidi ya imani ya kuwepo kwa Mungu ikawa hivi: Ikiwa Mungu ndiye Mwumbaji wa ulimwengu na vyote vilivyomo humu na ikiwa yeye ndiye Mtungaji na Mdumishaji wa kanuni za ulimwengu zilizogunduliwa na akili tafiti ya kibinadamu, imekuwaje Yeye Mwenyewe yu mjinga kabisa asijue hakika hizo?

Mtu anaposoma maelezo ya Biblia kuhusu jinsi mbingu na ardhi zilivyoumbwa na jinsi ambavyo mtu alitengenezwa kutoka katika vumbi na jinsi Bi Hawa alivyochongwa kutoka katika ubavu wa Adamu na kadhalika (Hiyo ni mifano miwili tu miongoni mwa mingi zaidi ambapo Neno la Mungu na kitendo cha Mungu vinapingana kwa hali ya kushtusha), mtu anastaajabu na kushangaa kwa kuona tofauti moja kwa moja baina ya mwanzo

wa uhai juu ya ardhi na maelezo yaliyotolewa katika kitabu cha Mwanzo.
Tofauti kama hizo zikalifanya Kanisa Kutumia mabavu katika zama zile ambapo Kanisa lilikuwa na madaraka ya kisiasa yasiyoweza kupingwa. Mfano mmoja mashuhuri ni wa kugongana baina ya Kanisa na Mwanasayansi Galileo.
Galileo (1564 - 1642) alipoeneza uvumbuzi wake kuhusu mfumo wa jua, dunia na sayari, ya kwamba ni sayari zinazozunguka, habari hiyo ikalikasirisha Kanisa kwani uvumbuzi wake huo ulipinzana na utambuzi wa Kanisa kuhusu utaratibu wa jamii ya jua, ardhi na sayari nyingine. Alitishwa vikali na kulazimishwa kukanusha uvumbuzi wake wa kisayansi. La sivyo angeweza kuuawa kwa kuteswa vibaya mno. Hata hivyo alihukumiwa kifungo cha nyumbani kwake mpaka mwisho wa maisha yake. Ni mnamo mwaka 1992 ambapo Kanisa likaamua kutangua hukumu iliyotolewa dhidi ya Galileo, baada ya kujadiliana kwa muda mrefu wa miaka kumi na miwili katika kamati iliyoundwa na Papa John Paul II.
Mwanzo athari ya hitilafu hizo haikupenya kwa watu wa kawaida katika jamii na kwa muda fulani ikabakia baina ya eneo maalum la wataalamu pekee. Lakini kwa kutapakaa kwa mwanga wa elimu ya kidunia, ule ulioitwa 'mwanga wa itikadi za kidini' ukafifia polepole mpaka ukawa sawa na giza. Mnamo siku za mwanzo za zama za kufufuka Elimu na Maarifa Ulaya ( karne ya 15) shughuli za wanasayansi ziliishia miongoni mwao wenyewe walioelimika. Uhusiano wao na watu wa kawaida unaoonekana siku hizi haukuwepo wakati huo. Kwahiyo imani yao kwamba hakuna Mungu haikuathiri jamii kwa jumla. Hata hivyo elimu ya dunia ilipotolewa kwa vijana wa mataifa yaliyoendelea mambo yakaanza kubadilika polepole kuelekea mwelekeo potofu dhidi ya dini. Saikolojia mpya ya jamii na filosofia vikaanza kuongezeka haraka hususan mnamo karne ya kumi na tisa na ishirini. Falsafa za kidunia zikichanganyika na maendeleo na fikara za kidunia zikaangamiza msingi wa dini yaani imani juu ya Mungu.

Khulka siku zote huongozwa na kulindwa na imani ya mtu katika Mungu. kama imani hiyo ni dhaifu au pungufu ama kitu fulani kinakosekana humo, basi kwa kiasi hicho hicho khulka itaathirika. Kwa mfano, kama imani juu ya Mungu inapingana na ujuzi wa kanuni za asili za ulimwengu na jinsi akili na busara inavyoamuru, hapo polepole ubora wa imani juu ya Mungu unaendelea kupungua na papo hapo khulka za watu zinaathirika vibaya. Ndipo jamii kwa vitendo hugeuka kuwa jamii isiyomwamini Mungu, ijapokuwa kwa kiasi kikubwa watu wanaweza kuwa waumini juu ya Mungu. Si vigumu kabisa kuhakikisha habari hii na kutambua usafi wa imani ya jamii juu ya Mungu. Kadri imani inavyokuwa dhaifu ama pungufu ndivyo inavyodhoofika nguvu yake juu ya khulka za watu. Wakati wowote hayo mawili yanapogongana, imani juu ya Mungu hulegea kuziachia nafasi tamaa mbovu

Kwa kutumia kanuni hiyo kwa jamii yoyote ya kidini popote duniani daima twaweza kufikia maamuzi sahihi ya kutegemewa. Kwa kuichunguza jamii ya Kikristo inayojidai kuwa na imani, mtu anaweza kuangalia tu ya kwamba khulka za Kikristo zinapatikana katika jamii hiyo ama hapana. Kwa mfano je, wanawatendea majirani zao jinsi Amri kumi zinavyowaamuru? Je, wanawatendea maadui zao sawa na kanuni za Kikristo wakati wa hatari za kitaifa katika hali ya vita na kadhalika? Je, wasio na kosa wakiteswa na kushambuliwa wanawageuzia maadui zao shavu la pili kwa kupigwa? Swali ni kwamba ni kwa kiasi gani matendo ya mtu yanaonesha imani yake? Kama matendo hayaoneshi picha hasa ya imani yake, basi hiyo ndiyo tuliyosema kwamba hapo imani juu ya Mungu imegongana na matakwa ya kibinadamu na mahitaji yake. Kama imani juu ya Mungu ni kitu bora kuliko vyote na kama matakwa ya mtu na mahitaji yake yanatolewa dhabihu juu ya madhabahu ya imani hiyo, hapo mtu anaweza kusema kweli ya kwamba imani hiyo hata ikiwa ya aina gani, kwa akali, ni halisi safi na imara.

Kuchunguza ulimwengu wa Kikristo ulivyo siku hizi, na kuutahini ili kutambua usafi wa imani yake juu ya Mungu, kunahuzunisha na kunamtoa mtu katika dhana za uwongo na kumwonesha ukweli. Kinachoonekana kama kawaida ni uhalifu dhidi ya imani juu ya Mungu moja kwa moja, na wakati mwingine ni maasi baridi yasiyodhihirisha kukanusha imani juu ya Mungu waziwazi. Pingamizi baina ya imani juu ya Mungu na vitendo vya watu binafsi unamdanganya mtu kufikiri kwamba ipo jamii ya kidini ya waumini, ilhali ukweli ndiyo tofauti kabisa. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa jamii zote za dini nyingine. Lakini kila mara siyo sababu moja inayoleta matokeo ya aina moja. Kila jamii inastahili kuchunguzwa sawa na hali yake maalum. Ndiyo maana uchunguzi unaofanywa kwa ukweli na utulivu bila upendeleo juu ya asili ya upinzani baina ya imani ya watu na matendo yao unakuwa wa muhimu sana.

Ni muhimu kuzingatia ya kwamba wakati mwingine imani yenyewe inapotoka na inakuwa siyo ya asili. Kwa mfano, sehemu fulani ya mafunzo ya Talmud kuwahusu wasiokuwa Wayahudi, na mafundisho ya Wahindu yaliyomo katika Manu Samarti kuwahusu Wasioguswa, bila shaka kutokutenda sawa nayo ndiyo afadhali sana kwa jamii hizo. (Wasioguswa ni watu wa jamii fulani ya Wahindu ambao wanahesabiwa duni sana hata kwamba mtu wa jamii nyingine akiwagusa ananajisika moja kwa moja). Na pengine imani yenyewe ni nzuri na inafaa kama watu wanatenda sawa nayo, lakini watu wanakuwa waovu na wanaachana nayo kwa kuona ni vigumu kutenda sawa nayo na wanaipuuzilia mbali. Tukirejea kwenye suala la Ukristo, twasema ya kwamba itikadi za msingi za Kikristo zinagongana na kanuni za asili za ulimwengu wala hazitimizi matumaini ya mtu yanayotegemea akili na busara. Katika hali kama hiyo Wakristo hawana budi polepole kuzipuuza itikadi zao na kutoziruhusu ziongoze maisha yao.

## 1 UANA WA YESU KRISTO

Uhusiano wa Baba na Mwana baina ya Mungu na Yesu Kristo ni imani ya msingi katika Ukristo. Hebu tujaribu kwanza kuelewa muradi wa kuwa mwana halisi. Tunapofikiria sana maana hasa ya kuwa mwana halisi wa baba tunalazimika kusahihisha maoni yetu kuhusu 'uana' wa Yesu. Mwana maana yake nini? Katika zama ambapo elimu ya sayansi ilikuwa haijaendelea mbele na ilikuwa haijajulikana mtoto anazaliwaje, swali hilo liliweza kujibiwa kwa njia isiyokuwa ya yakini hasa. Watu wa kale waliona kwamba inawezekana Mungu kupata mwana anayezaliwa na mtu. Imani hiyo ilienea pote duniani katika jamii ya kipagani. Maitholojia ya kigiriki imejaa hekaya za aina hiyo na maitholojia ya Kihindu nayo haikubakia nyuma pia. Kwani miungu kujipatia wana na mabinti wengi walivyopenda haikuhojiwa kwa makini na akili ya kibinadamu. Lakini siku hizi sayansi imekwisha pata maendeleo kiasi hiki kwamba njia ya kuzaliwa imefafanuliwa mno kuliko zamani. Habari hii ya Mungu kupata mwana imekuwa tata mno na wale ambao bado wanaamini kwamba wana na mabinti halisi wa Mungu waweza kuzaliwa, basi wanakabiliwa na tatizo kubwa la kutatua na baadhi ya maswali magumu kuyajibu.

**MSINGI WA KISAYANSI WA UZAZI:**

Kwanza kabisa ningependa kuwakumbusha ya kwamba mama na baba wanashiriki kwa usawa katika kuzaa mtoto. Chembehai (cell) za binadamu zina kromosom 46 ambazo zinakuwa na nyuzi -nyuzi zile za kumjaalia mtoto sifa mbalimbali. 'Yai' la mwanamke lina kromosom 23 pekee ambazo ni nusu nzima ya kromosom 46

kwa jumla zinazopatikana katika kila mwanamume na mwanamke. 'Yai' la mwanamke linapokuwa tayari kwa kushika mimba, nusu nyingine ya kromosom zinazopungua humo zinatimizwa na mbegu ya mwanamume inayoingia mle na kulirutubisha. Ndivyo alivyopanga Mwenyezi Mungu; la sivyo, idadi ya kromosom zingeongezeka mara mbili kila kizazi. Na matokeo ya kuongezeka huko maradufu ni kwamba kizazi cha pili kingekuwa na krosom 92, na binadamu haraka sana wangegeuka kuwa majitu na mpango mzima wa ukuaji ungelivurugika. Mungu amepanga vizuri kabisa mpango wa kuokoa viumbe kwa kufanya idadi ya kromosom iwe nusu katika seli wakati wa kuzaana. 'Yai' la mama lina kromosom 23, na kadhalika mbegu ya baba pia inazo kromosom 23. Hivyo basi mtu anaweza kutazamia kwamba mtoto atapata nusu ya nyuzi-nyuzi za kumtilia sifa kadha kutoka kwa mama na nusu nzima kutoka kwa baba. Hiyo ndiyo maana hasa ya mwana halisi. Hakuna ufafanuzi mwingine wowote ule wa 'mwana halisi' anayezaliwa kwa sura ya binadamu. Ziko njia mbalimbali za kutunga mimba lakini hakuna tofauti katika kanuni iliyoelezwa hapo juu.

Tukichunguza vizuri kuzaliwa kwa Yesu, hebu tutafakari nini kinaweza kuwa kilitendeka. Uwezekano wa kwanza unaoweza kufikiriwa kisayansi ni kwamba 'yai' la Mariamu lilitoa kromosom 23 kwa kushika mimba. Kama ndivyo hivyo, hapo swali linazuka kwamba 'yai' lilirutubishwaje na kromosom nyingine 23 za lazima zilitokea wapi? Haiwezekani asilani kusema kwamba chembehai za Yesu zilikuwa na kromosom 23 tu. Hakuna mtoto wa kawaida wa kibinadamu anayeweza kuzaliwa akiwa hai hata kama anazo kromosom 45. Kama mtu anakosa hata kromosom moja tu miongoni mwa 46 ambazo ni za lazima sana kwake kuumbika, kama kuna matokeo yake, basi hayatukuwa chochote ila machafuko. Kisayansi Mariamu peke yake asingeweza kutoa kromosom 46; ni lazima nyingine 23 zingetokea mahali fulani. Kama Mungu ndiye baba, hapo tena kuna chaguzi kadha.

Kwanza, Mungu pia anazo kromosom sawasawa na kromosom za kibinadamu. Kwahiyo hizo kromosom zikaingia katika mfuko wa uzazi wa Mariamu kwa namna fulani. Lakini hiyo haiaminiki wala haikubaliki. Kama Mungu anazo kromosom za kibinadamu, Yeye hawezi kubaki kuwa Mungu. Hivyo matokeo ya imani katika Yesu kuwa mwana wa halisi wa Mungu ni kuhatarisha Uungu wa Baba pia.

Uwezekano wa pili ni kuwa Mungu aliumba kromosom za ziada kwa njia isiyo ya kawaida ya uumbaji. Kwa usemi mwingine hizo hazihusikani hasa na nafsi ya Mungu, isipokuwa ziliumbwa kimwujiza. Hii itatuelekeza moja kwa moja kuukataa uhusiano wa Yesu na Mungu kuwa ni wa mwana na Baba, na utatuongoza kuukumbatia uhusiano ule ulio mkuu wa ulimwengu kwa Mungu, yaani uhusiano wa kila kilichoumbwa kwa Muumbaji wake.

## JE, MWANA HALISI WA MUNGU ANAWEZEKANA?

Ni dhahiri kwamba haiwezekani kupatikana mwana halisi wa Mungu, kwani hapana budi huyo mwana halisi apate kromosom zake nusu kutoka baba yake na nusu kutoka kwa mama yake. Hapa panazuka tatizo jingine: Mwana atakuwa nusu mtu na nusu mungu. Lakini wale wanaomwamini Yesu kuwa mwana halisi wa Mungu wanadai na wanasisitiza kwamba yeye alikuwa mtu mkamilifu na mungu mkamilifu.

Na kama kromosom zilikuwa nusu tu ya idadi iliyotakiwa, hapo hamna tatizo tena, kwani mtoto hawezi kuzaliwa abadan. Na tukidhani alizaliwa na kromosom nusu, basi atakuwa nusu mtu. Achilia mbali kromosom 23 nzima nzima, hata kama 'nyuzi' moja pekee ya kromosom moja ina upungufu, hiyo italeta hatari kubwa kabisa kwa mtoto atakayezaliwa akiwa na upungufu katika mwili wake. Anaweza kuwa kipofu, hana mikono na miguu kiziwi na bubu. Hatari zitokanazo na bahati hiyo mbaya hazina kikomo. Mtu anapaswa kukubali uhakika; haiwezekani kuwaza kwamba

Mungu anazo kromosom za kibinadamu ama za aina yoyote nyingine. Hivyo, ushirikiano wa Mungu binafsi kwa njia ya kiwiliwili unapofutiliwa mbali, endapo Mariamu angezaa mtoto kutokana na vijine (genes) vya kumtilia mtoto sifa za kibinadamu vilivyokuwamo ndani ya 'yai' (ovum) lake (Mariamu), kwa vyovyote itakavyokuwa mtoto huyo hatakuwa mwana wa Mungu. Sana sana unaweza kusema kwamba huyo kiumbe wa ajabu atakuwa nusu mtu tu, basi. Kama viungo vya uzazi vya Mariamu vilikuwa sawasawa na vile vya mwanamke yeyote wa kawaida, na hata hivyo kama 'yai' likashika mimba lenyewe, tunachoweza kutazamia kuzaliwa kwa wingi ni kiumbe fulani chenye sifa nusu za kibinadamu. Itachukiza kukiita kitu hicho 'Mwana' wa Mungu. Alizaliwaje, basi, Yesu? Tunajua ya kwamba uchunguzi kuhusu kuzaliwa mtoto kwa mama pasipo ushirikiano wa mwanamume unaendelea katika nchi zilizoendelea. Lakini mpaka sasa utaalamu wa mtu upo mahali ambapo elimu yake ya sayansi haijaendelea kiasi cha kuweza kuhakikisha pasipo shaka kwamba mtoto wa kibinadamu anaweza kuzaliwa kwa bikira bila kushirikiana na mwanamume. Hata hivyo, upo uwezekano wa jambo hilo kutokea katika hali mbalimbali.

Katika uhai wa daraja la chini mambo mawili yamethibitika Kisayansi: Hermaphroditism (yaani kuwa huntha) na Parthenogenesis. Kwahiyo kuzaliwa Yesu kimwujiza kwa Mariamu kunaweza kusababishwa na kanuni fulani aina hiyo ambayo ni ya nadra sana na mipaka yake haijapimwa na mtu kwa ukamilifu.

Hapa chini kuna maelezo mafupi ya *Hermaphroditism* na *Parthenogenesis.* Wasomaji wanaopenda kujua hayo zaidi kisayansi wanaweza kurejea kwenye Nyongeza II mwishoni mwa kitabu hiki.

## HERMAPHRODITISM:

Hermaphroditism inapatikana wakati ambapo viungo vya kiume na kike vinapatikana katika mwanamke mmoja na kromosom zinaonesha sifa zote mbili za kike na kiume zilizojipanga moja kando ya nyingine. Majaribio katika maabara yamethibitisha ya kwamba sungura mmoja huntha (Hermaphrodite) aliwapanda sungura wengi majike ambao wakazaa watoto 250 ambamo kuna majike na madume. Lakini sungura huyo huntha wakati mwingine alitengwa peke yake na akashika mimba bila kupandwa na akazaa sungura majike na madume saba kwa jumla. Alipochunguzwa alipatikana na vifuko viwili vya 'mayai' tumboni vilivyofanya kazi na pia makende mawili yasiyoweza kuzaa wakati alipokwisha shika mimba. Uchunguzi wa siku za karibu umeeleza ya kwamba jambo hili linawezekana kwa nadra katika wanadamu pia.

## PARTHENOGENESIS:

Parthenogenesis ndiyo 'yai' la jike kupata kukua pasipo kusaidiwa na dume. Jambo hili linaonekana katika namna nyingi za uhai wa daraja la chini kama vile vijidudu na pia samaki . Kuna ushahidi pia ya kwamba Parthenogenesis inaweza kutokea katika mijusi wanaoishi katika sehemu zenye mvua haba. Katika maabara, panya na sungura waliweza kushika mimba nusu-nusu kwa njia ya Parthenogenesis, lakini mimba hizo zikaharibika. Katika uchunguzi wa siku za karibu wanasayansi wamegundua ya kwamba mara moja moja Parthenogenesis inaweza kupatikana katika binadamu pia, na mwanamke anaweza kushika mimba bila mume kwa msaada wa *Calcium Ionophore* ambayo inawekwa humo pasipo kutumika isipokuwa tu kuwapo kwake kunaathiri. Uchunguzi huu unaelekeza kwenye matarajio ya kwamba kuharibika mimba ya mwanadamu katika siku za mwanzoni kunaweza kusababishwa na ukuaji wa mimba kwa njia ya Parthenogenesis.

Sawa na uchunguzi wa hivi karibuni, imehakikishwa ya kwamba kuzaa bila baba kunawezekana kisayansi. Taarifa moja iliyochapishwa katika gazeti la *Nature genetics* la Oktoba 1995 inaeleza habari ya mvulana mmoja mwenye umri wa miaka mitatu ambaye mwili wake kiasi fulani ulitokana na 'yai' lisilochanganyikana na mbegu ya mwanamume. Wachunguzi walikagua mifuatano yote ya DNA kuhusu X-Kromosom katika ngozi na damu ya mvulana na wakagundua ya kuwa X-Kromosom katika chembehai zake zote zilitokana na mama peke yake. Kadhalika sehemu zote mbili za kila Kromosom miongoni mwa jozi 22 za Kromosom nyingine katika damu yake zilikuwa kabisa zinafanana na zilitokana zote na mama yake.

**MIUJIZA NI NINI ?**

Kwa kudhihirika uwezekano wa bikira kuzaa, hivyo jambo hili haliwi tena lisilowezekana na kinyume cha kanuni ya asili ya ulimwengu. Ipo wapi basi haja ya kutafuta maelezo ya Yesu kuzaliwa nje ya kanuni za asili, ama kupita kiasi katika kuamini kuwa 'Mwana' halisi wa Mungu aliyezaliwa kwa uzazi wa kibinadamu? Pale mambo mbali mbali kama yalivyoelezwa hapo juu yanapoonekana kwamba ni ukweli wa asili, unaoshuhudiwa katika ulimwengu, kwa nini basi iwe vigumu kuamini kuzaliwa kwa Yesu kuwa sawa na kanuni fulani ya ulimwengu iliyofichikana, iliyofanya kazi sawa na mpango maalum wa Mungu? Hali fulani ikapatikana ndani ya Mariamu iliyosababisha mtoto kuzaliwa kimwujiza bila mwanaume kumgusa. Hii ndiyo imani ya Waislamu Waahmadiyya kwamba ndivyo hasa ilivyotendeka. Imani yetu hiyo ni imara kwani hakuna mwanasayansi anayeweza kuikanusha kwa kuihesabu kuwa upuuzi, wala imani yetu hiyo haiko kinyume cha kanuni ya asili iliyopo ulimwenguni.

Katika Islam miujuiza haihesabiwi kuwa matukio yaliyo dhidi ya kanuni ya asili ya ulimwengu, bali sawasawa kabisa na kanuni

ya ulimwengu iliyofichikana tu katika zama fulani wasiitambue watu. La sivyo, hapo patazuka matatizo mengi dhidi ya hekima ya Mungu. Kama ni Mungu ndiye aliyeunda kanuni za asili za ulimwengu, bila shaka Yeye angeweka taratibu ambazo pasipo kuzivunja angeweza kutoa ufumbuzi unaohitajika kwa kila tatizo. Siyo kwamba kanuni zote za ulimwengu zinajulikana kwa mtu. Ziko aina mbalimbali za kanuni zinazofanya kazi katika tabaka tofauti na maeneo mbali mbali. Wakati mwingine kanuni hizo zinajulikana kwa mtu katika eneo moja tu lakini uwezo wake wa kuona unashindwa kupenya nje ya eneo hilo. Kadiri wakati unavyopita ujuzi wa mtu unaongezeka, kadhalika na uwezo wake wa kuona unazidi kupenya zaidi ya eneo hilo na anaweza kushuhudia zile kanuni ambazo hapo kabla alikuwa hazitambui. Elimu ya sayansi ikiendelea mbele, uvumbuzi wa aina aina unazitilia mwanga kanuni hizo zinazoonekana kufanya kazi katika vikundi. Hivyo kazi zake na ushirikiano wake pamoja na kanuni nyingine hujulikana vizuri zaidi.

Mambo yale yaliyoonekana ni miujiza katika zama za kale hayahesabiwi kuwa miujiza katika zama hizi. Mambo yanahesabiwa kuwa miujiza kwa kulingana na ujuzi wa mtu katika nyakati maalum. Mungu anapodhihirisha nguvu yake maalum, huonekana kana kwamba kanuni fulani imevunjiliwa mbali. Lakini sivyo ilivyo bali kanuni nyingine iliyofichikana kwa macho ya binadamu ilikuwapo hapo mapema ambayo sasa imefanya kazi kwa amri ya Mungu . Watu wa zama hizo hawakuweza kutambua kanuni hiyo wala hawakuidhibiti. Kwa mfano, nguvu ya sumaku haikujulikana kwa mtu miaka elfu chache iliyopita. Kama mtu fulani angeliigundua nguvu hiyo kwa bahati na kisha kama angefanya hila ya kuvifanya vitu viangame hewani kwa kutumia nguvu hiyo ya sumaku pasipo watu kujua uhakika huo, yeye mtu huyo angeliweza kuwashangaza watu kwa kusema: Lo, mwujiza umetendeka. Siku hizi hila kama hizo ni mambo ya kawaida yasiyotiwa maanani sana. Ujuzi wa mtu una kikomo, lakini ujuzi wa Mungu hauna mwisho. Kama kanuni fulani isiyojulikana kwa

mtu inafanya kazi, hiyo huonekana kama mwujiza. Lakini kwa kuangalia mambo ya ajabu ya aina hiyo yaliyofanyika zamani baada ya kwisha kupata ujuzi wake sasa twaweza kukanusha kwamba kanuni za ulimwengu zilivunjika, bali hayo yalitendeka sawasawa kabisa na kanuni ambazo hazikujulikana kwa watu wa zama hizo. Ndiyo maana nilisema kwamba ni lazima ilikuwepo kanuni fulani iliyosababisha Yesu kuzaliwa bila baba, ambayo haikujulikana kwa watu wa zamani zile; haijaeleweka vizuri hata sasa. Lakini sayansi inasonga mbele upande huo na mengi yanazidi kueleweka. Hivyo utawadia wakati ambapo mtu yeyote hataweza kudai ya kwamba kuzaliwa kwa Yesu pasipo baba kulikuwa kinyume na kanuni ya ulimwengu.

## JE, YESU YU MWANA WA MUNGU ?

Kuna matatizo mengine mengi ya Wakristo kuhusu kumwelewa Yesu asili yake na uhusiano wake na Mungu. Tukichunguza na kuchambua imani ya Kikristo kinachojitokeza ni kwamba kuna Mwana wa Mungu ambaye anazo sifa za mtu mkamilifu na pia zile za mungu mkamilifu. Hata hivyo kumbuka ya kwamba sawa na imani ya Kikristo 'Baba' si sawa hasa na 'Mwana'. Mungu Baba yu Mungu mkamilifu lakini si mtu mkamilifu, ambapo 'Mwana' ni mtu mkamilifu na papo hapo ni mungu mkamilifu pia. Ndiyo kusema kwamba hawa wawili ni dhati mbili tofauti walio na sifa mbalimbali.

Ieleweke ya kwamba sifa hizo haziwezi kubadilishwa. Ziko sifa katika baadhi ya vitu ambazo zaweza kubadilishwa. Kwa mfano, maji yaweza kugeuka kuwa theluji na pia mvuke pasipo kubadilika kitu chenyewe ama asili yake. Lakini tofauti zilizopo katika sifa za Mungu na Kristo, ambapo sifa kadha zinaongezwa kwa mmoja wao, haziwezi kupatanishwa asilani. Haiwezekani kwa mmoja wao kupata mabadiliko hayo na asipambanuliwe na mwenzake. Ni tatizo kubwa kabisa ya kwamba Yesu Kristo alikuwa mungu mkamilifu na mtu mkamilifu. Kama alikuwa na sifa za aina hizo

mbili kwa pamoja, bila shaka yeye alikuwa tofauti na Baba ambaye hakuwa mtu kamili wala mtu asiye kamili. Huo uhusiano ulikuwa wa aina gani? Je, 'Mwana' alikuwa mkubwa kuliko Baba? Kama sifa yake hiyo ya ziada haimfanyi 'Mwana' kuwa mkubwa kuliko Baba, hapo bila shaka sifa hiyo ina dosari. Kwa maana hii 'Mungu Mwana' mwenye kasoro si tu ni kinyume cha madai ya Ukristo bali pia ni kinyume kabisa na Mungu jinsi anavyofahamiwa na watu wote ulimwenguni. Basi mtu anawezaje kuelewa itikadi ya ajabu inayojipinga yenyewe, ambayo inatutaka tuamini kwamba 'Mmoja katika Watatu' na 'Watatu katika Mmoja' ni sawa tu pasipo tofauti yoyote iwayo? Hiyo inaweza kutokea tu iwapo msingi wa imani hauwekwi juu ya hakika bali unawekwa juu ya mawazo ya kuzushwa.

Isitoshe, kuna tatizo jingine tena linalopaswa kutatuliwa, nalo ni hili: Kama Yesu alikuwa 'Mwana wa Mungu' kwa sababu ya kuzaliwa kutoka katika tumbo la Mariamu, basi cheo chake kilikuwa kipi hapo kabla? Na kama yeye alikuwa 'Mwana' siku zote hata bila ya kuzaliwa na Mariamu, ilikuwa haja gani basi, kwamba azaliwe kwa sura ya binadamu? Na kama ilikuwa lazima, hapo sifa ya kuwa Mwana haikuwa ya milele; bali ilipatikana kama sifa ya nyongeza baada ya yeye kuzaliwa na ikatoweka alipotengana na mwili na kurejea mbinguni. Hivyo kuna matatizo mengi yazukayo kutokana na itikadi inayokanushwa na akili na busara. Nawaalikeni kukubali jambo lililo na heshima tena la hakika, la kuzaliwa kwa Yesu aliyeumbwa na Mungu kwa kutumia kanuni fulani za asili zilizofichika machoni mwa watu. Yesu alikuwa mwana wa Mungu kimithali aliyekuwa mpenzi maalum wa Mungu, lakini hata hivyo alikuwa mwanadamu kwa vyovyote. Cheo cha kuwa 'Mwana' alipachikwa miaka mia tatu takriban baadaye ili kuendeleza hekaya yake jambo ambalo litajadiliwa baadaye.

Hali ya uhusiano wa ndoa baina ya Mungu Baba na Mariamu ni swala ambalo mtu anachukia kulijadili waziwazi. Hata hivyo katika jitihada za kuelewa ile kazi ya kati aliyoifanya Mariamu

baina 'Baba' na 'Mwana', hilo linakuwa ni uovu usioepukika. Labda swali hilo hilo lilimuudhi sana Nietzsche hata kwamba mwishowe akaeleza kutoridhika kwake kusikoelezeka kwa maneno yafuatayo:

> "Si muda mrefu baada ya Zarathustra kujikomboa kutoka kwa wachawi, ila alimwona tena mtu ameketi pembeni ya njia aliyokuwa akipita: Mtu mrefu, mweusi mwenye uso uliopauka na kukonda; mtu huyu alimwudhi sana. "Ala", aliwaza moyoni mwake "haya ni mateso yaliyojigeuza", anaonekana kama padri vile; wanataka nini toka himaya yangu? Akasema 'yeyote uwaye ewe msafiri msaidie aliyepotea njia, mzee ambaye huenda amekuja kukudhuru!'
> Dunia hapa ni ngeni na inajitenga nami, ninasikia milio ya wanyama wa mwitu na yule ambaye angeweza kunilinda yeye mwenyewe hayupo tena.
> Nilikuwa namtafuta mcha Mungu wa mwisho, mtakatifu na mtawa aishiye peke yake msituni ambaye hajasikia yote inayoyajua dunia siku hizi?
> Ni nini inachojua dunia sasa? Aliuliza Zarathustra. Ni hivi labda: Mungu yule wa zamani ambaye ulimwengu ulimwamini, hayuko tena.
> Hivyo ndivyo ilivyo, alijibu mzee kwa huzuni. Na nilimtumikia yule Mungu wa zamani hadi saa yake ya mwisho.
> Sasa nimejiuzulu katika huduma, pasipo bwana, hata hivyo bado sijawa huru, wala sina furaha hata kwa saa moja isipokuwa kwa kukumbuka yaliyopita. Ndiyo maana nikapanda katika milima hii ili nisherehekee sikukuu mara nyingine, jinsi anavyokuwa Papa mzee na Padre: kwani jueni mimi ndimi Papa wa mwisho ---- sikukuu ya makumbusho matakatifu na ibada za Mungu.
> 'Lakini sasa yeye mwenyewe amekufa, mtu aliyekuwa mwema sana, yule walii msituni aliyekuwa anamsifu Mungu wake daima kwa kuimba na kunung'unika.'
> Nilipokuta banda lake sikumkuta mle ndani, bali nikawakuta humo mbwa mwitu wawili wakimlilia kifo chake - kwani wanyama wote walimpenda. Kisha nikaondoka hapo haraka.'

Je, nilifika katika misitu hiyo na milima hiyo bure? Ndipo moyo wangu ukaamua kumtafuta mwingine aliye mwema kuliko wale wote wasiomwamini Mungu - kumtafuta Zarathustra!'

'Ndipo akasema yule mzee na kumkazia macho aliyesimama mbele yake; Zarathustra akaushika mkono wa papa mzee na kwa kitambo kirefu akauheshimu kwa kuusifu.'

'Angalia, mheshimiwa,' kasema tena, mkono mrefu na mzuri ulioje huu! Huu ni mkono wa yule ambaye daima aligawa baraka. Lakini sasa huu unamshika kwa nguvu yule unayemtafuta, mimi, Zarathustra.'

'Ndimi mimi, Zarathustra nisiye na Mungu, nisemaye: Ni nani asiye na mungu kuliko miye, ili niweze kufurahia mafundisho yake.'

Ndivyo alivyosema Zarathustra na kutoboa kwa nadhari yake mawazo ya papa mzee na yaliyofichika moyoni mwake. Mwishowe mwingine akaanza:

'Yule aliyempenda sana na kummiliki amemkosa sana pia!:

'Angalia, je, mimi mwenyewe kati yetu si yule asiye na Mungu hivi sasa. Lakini nani angefurahia hayo! Ulimtumikia mpaka mwisho,' kauliza Zarathustra kwa makini, baada ya kiyma kirefu, je, wajua alikufaje? Je, ni kweli wasemayo ya kwamba huruma ilimkwama!

'Ya kwamba alimwona mtu alikitundikwa msalabani wala hakustahamili, mapenzi yake kwa mtu yakawa Jahanamu yake na hatimaye kafa?'

Papa mzee hakujibu, lakini akaangalia upande mwingine kwa haya na kwa uso wa huzuni na uchungu.

'Wacha niende!, kasema Zarathustra baada ya kutafakari sana, na kwa muda huo wote aliendelea kumkodolea macho moja kwa moja mzee huyo.

'Mwache aondoke, yeye amekwisha. Na ijapokuwa ni heshima kwako ya kwamba wewe useme vyema kuhusu mungu huyo mfu, hata hivyo wewe na pia mimi twajua huyo alikuwa nani; na kwamba yeye alifuata njia za ajabu.'

'Iwe siri yetu,' katamka papa mzee akichangamka, ama niseme chini ya macho (kwani alikuwa mwenyewe chongo) 'katika mambo ya roho mimi nina maarifa zaidi kuliko Zarathustra

mwenyewe - na ningeweza kuwa hivyo!
'Mapenzi yangu yalimhudumia kwa miaka mingi, takwa langu likalitii takwa lake. Mtumishi mwema anatambua kila kitu, na mambo mengi pia, ya kwamba bwana wake anajificha kwake mwenyewe.'
'Yeye alikuwa mungu aliyekuwa mafichoni, siri tupu. Kusema kweli, alikuja kwa njia ya mwana tena kisirisiri siyo dhahiri. Kizingitini mwa imani hiyo pana uzinzi.'
Yeyote anayemheshimu kuwa mungu wa upendo hauthamini upendo vya kutosha. Je, Mungu huyo hakupenda kuhukumiwa? Lakini apendaye hupenda pasipo kujali thawabu ama adhabu.'
'Mungu huyo wa mashariki alipokuwa kijana, alikuwa mkali na mwenye kujilipiza kisasi na mwenyewe akatengeneza Jahanamu kwa kuwafurahisha wapenzi wake.'
Lakini mwishowe akazeeka na akawa mpole, laini na raufu zaidi kama babu kuliko baba, zaidi kama bibi mkongwe.'
'Kisha akaketi akikunjamana kwenye kona ya dohani yake, akihuzunika kwa miguu yake isiyo na nguvu, aliyechoka na dunia, hata nia yake ya kutenda ikachoka, na siku moja akakosa hewa kwa huruma yake iliyopita kiasi.'[1]

---

[1]Thus Spoke Zarathustra, utungo wa Friedrich Nietzsche. kurasa 271-273, Tafsiri ya kiingereza ilienezwa na Penguin Books 1969.

## 2 DHAMBI NA KAFARA

Sasa twaelekea kwenye nguzo muhimu ya pili ya imani ya Kikristo. Ningebainisha kwanza ya kwamba Wakristo wote hawaamini neno kwa neno yatakayofuata hapa chini. Hata baadhi ya viongozi wa Kanisa wamekwenda upande na kuachana na msimamo mgumu wa fundisho la imani la Kanisa. Hata hivyo falsafa ya 'Dhambi na kafara' ni kanuni ya msingi ya imani ya Kikristo inayokubalika kwa jumla.

Sehemu ya kwanza ya maana ya Dhambi na Kafara ni kwamba Mungu ni mwadilifu na anafanya uadilifu wa dhati. Yeye hasamehe dhambi pasipo kuadhibu; kwani kusamehe tu dhambi hivi hivi kungekuwa kinyume cha uadilifu halisi. Sifa hiyo ya Mungu inasababisha kafara ilivyoaminiwa na Wakristo kuwa jambo la lazima.

Sehemu ya pili ni kwamba mtu ni mwenye dhambi kwa sababu Adamu na Hawa walitenda dhambi. Matokeo yake ni kwamba wazao wao wakaanza kurithi dhambi, kana kwamba hiyo dhambi ikaingizwa katika vijine (genes) vyao na tangu hapo watoto wote wa Adamu huzaliwa wakiwa wenye dhambi.

Sehemu ya tatu ya itikadi hiyo ni kwamba mwenye dhambi hawezi kutoa kafara ya dhambi ya mwingine: mtu asiye na dhambi pekee ndiye anayeweza kutoa kafara ya dhambi za wengine. Juu ya msingi huu, inakuwa wazi sawa na ufahamu wa Kikristo, ya kwamba Nabii yeyote wa Mungu hata akiwa mwema namna gani ama akiwa karibu sana na ukamilifu hawezi kumtakasa mtu na kumwondolea dhambi na matokeo yake. Akiwa mwana wa Adamu, asingeweza kuepukana na dhambi aliyorithi alipozaliwa.

Huo ndiyo muhtasari wa muradi wa imani nzima ya kafara. Hapa chini pana maelezo yaliyotolewa na wataalamu wa dini ya Kikristo.

**KAFARA KWA MWANADAMU:**

Ili kutatua tatizo lisiloweza kutatulika kidhahiri, Mungu akawaza mpango wa akili sana. Haijulikani kwamba yeye alishauriana na mwana ama hapana; ama wote wawili wakawaza mpango huu wakati mmoja; au uliwazwa na mwana peke yake lakini ukakubaliwa na Mungu Baba. Maelezo ya mpango huu yalifafanuliwa katika zama za Yesu kama ifuatavyo. Miaka elfu mbili iliyopita 'Mwana wa Mungu' aliyeshirikiana na Mungu katika umilele barabara, alipata kuzaliwa tumboni mwa mama wa kibinadamu. Akiwa 'Mwana wa Mungu' yeye akajikusanyia ndani yake sifa kamilifu za kibinadamu na pia za Mungu Baba. Tena tunaambiwa ya kwamba mama mmoja mwema na mtawa, jina lake Mariamu, akachaguliwa kuwa mzazi wa 'Mwana wa Mungu' Mama huyo akashika mimba ya Yesu kwa kushirikiana na Mungu. Ndiyo kusema kwamba Yesu akiwa mwana halisi wa Mungu akazaliwa pasipo kuwa na dhambi, hata hivyo akachukua sifa na sura ya binadamu. Hivyo akajitolea kwa hiari yake kubeba mzigo wote wa madhambi ya wale watu watakaomwamini na kumkubali kuwa mwokozi wao. Kwa njia ya mpango huo wa akili, inadaiwa, Mungu akaepa kuhatarisha sifa yake ya uadilifu halisi.

Kumbukeni ya kwamba sawa na mpango huu pia mtu hatasamehewa dhambi pasipo kuadhibiwa. Bado Mungu ataweza kumwadhibu mwenye dhambi bila ya kuepa sifa yake ya uadilifu. Tofauti yenyewe ni kwamba sasa Yesu ataadhibiwa, siyo wale wana na mabinti wa Adamu waliotenda dhambi. Hiyo ni fidia ya Yesu itakayosababisha kuwaondolea dhambi watoto wa Adamu. Mantiki hiyo hata ikionekana ya ajabu na ya kutatanisha namna

gani, lakini ndivyo ilivyokubaliwa hasa kwamba ilitendeka. Yesu akajitolea mweyewe na akaadhibiwa kwa ajili ya dhambi ambazo hakuzitenda kabisa.

**DHAMBI YA ADAMU NA HAWA:**

Hebu tuchunguze upya kisa cha Adamu tangu mwanzo. Sehemu yoyote ya itikadi hiyo hapo juu haiwezi kukubaliwa na dhamiri ya mtu na mantiki.

Kwanza, tunaambiwa ya kwamba kwa kuwa Adamu na Hawa walitenda dhambi, basi wazao wao wakachafuliwa kwa kudumu na dhambi waliyorithi wakati wa kuzaliwa. Lakini kinyume chake, sayansi ya tabia zirithishwazo inabainisha ya kwamba mawazo na matendo ya mtu, yakiwa mazuri ama mabaya , hata mtu akiwa nayo kwa kudumu maisha mazima, hayawezi kuhamishwa katika mfumo wa tabia za kurithishwa katika kuzaana. Muda wa maisha ya mtu ni mdogo sana kwa kuleta mabadiliko hayo makubwa. Hata maovu ama mema ya taifa, kizazi baada ya kizazi, hayawezi kuingizwa katika wazao yakiwa ni mienendo ya kurithiwa. Labda mamilioni ya miaka inahitajika kuingiza sifa mpya katika vijine (genes) vya mtu.

Hata kama mtu angekubali kutukia jambo hilo la ajabu la kutatanisha kwa kapanua mawazo yake ya kipuuzi yasiyokubalika akilini, basi na angekubali kilicho dhidi yake pia kwa kutumia mantiki kama hiyo. Hiyo itamaanisha ya kwamba kama mtu mwenye dhambi akitubu na akatakasika mwishoni mwa siku, basi hiyo nayo ingerekodiwa katika mfumo wa sifa zile zinazorithishwa na kufutilia mbali kabisa athari ya dhambi ile ya zamani. Kisayansi hiyo haiwezi kutendeka, lakini kwa yakini kuna mantiki zaidi katika picha hiyo inayoonesha pande mbili kwa usawa kuliko kufikiria kwamba maelekeo kwa dhambi tu yanaandikwa katika utaratibu wa sifa za kurithishwa lakini maelekeo ya mema hayaandikwi.

Pili, kwa kujaribu kutatua tatizo la Adamu kwa kutoa shauri ya kuwa dhambi inahamishwa kwa vizazi vijavyo ambavyo vinairithi tangu kuzaliwa, msingi wenyewe unabomolewa ambao juu yake imani ya 'Dhambi na kafara' imejengwa. Kama Mungu ndiye mwadilifu halisi, basi upo wapi uadilifu katika kuwahukumu wazao wote wa Adamu na Hawa kwa dhambi yao waliyotenda mara mmoja tu na kisha wakatubu pia?

Kwa vyovyote, hiyo ilikuwa dhambi ambayo waliadhibiwa vikali kwa sababu yake na wakafukuziliwa mbali katika Pepo kwa fedheha kubwa . Ni aina gani ya uadilifu ya kwamba baada ya kuwaadhibu Adamu na Hawa sana sana kupita kiasi kwa sababu ya dhambi yao, bado hamaki ya kujilipiza kisasi haijapoa na akawahukumu wanadamu wote wapate fedheha ya kuzaliwa tayari wamerithi dhambi? Nafasi gani wanayo wazao wa Adamu kuikwepa dhambi? Kama wazazi wanafanya kosa, kwa nini watoto wao wasiokosea wasumbuke daima kwa sababu ya kosa la wazazi wao?

Kama ni hivyo, basi batilifu iliyoje maana ya uadilifu anayojidaia Mungu na kuifurahia ikiwa Yeye anawaadhibu watu waliopangiwa kutenda dhambi hata wakichukia dhambi namna gani? Dhambi ikafanywa sehemu ya maana sana ya maumbile yao. Hamna kabisa sasa nafasi kwa mtoto wa Adamu kubaki katika hali ya kutokuwa na dhambi. Kama dhambi ndiyo jinai basi ni jinai ya Mwumbaji siyo ya viumbe. Basi, uadilifu gani ungetaka kuwaadhibu wasiokosea kwa jinai za wengine?

Tangazo la Kurani Tukufu ni tofauti kabisa na ufahamu wa Kikristo wa dhambi na matokeo yake. Kurani Tukufu inatangaza:

> Hakuna mbebaji atakayebeba mzigo wa mwingine. (35: 19)

> Mungu haikalifishi nafsi yoyote zaidi ya uwezo wake. (2:287)

Tangazo hilo la Kurani kwa kulinganisha na imani ya Kikristo kuhusu Dhambi na Kafara ndiyo taratibu halisi ya kuituliza roho. Sasa tugeukie maelezo ya Biblia kuhusu yaliyotendeka hasa wakati Adamu na Hawa walipotenda dhambi, na matokeo yaliyofuata nyuma ya wao kuadhibiwa. Sawa na mafunzo ya Mwanzo, Mungu alikubali nusu-nusu udhuru wao na wakapewa adhabu ya kudumu milele inavyoelezwa hapa chini:

> Akamwambia mwanamke, Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa uchungu utazaa watoto, na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala. Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza, nikisema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo kwa hiyo ulitwaliwa kwa maana u mavumbi wewe nawe mavumbini utarudi (Mwanzo 3:16-19)

Wanadamu walikuwapo muda mrefu sana kabla hawajazaliwa Adamu na Hawa. Wanasayansi wa magharibi wenyewe waligundua mabaki ya watu wengi waliokuwepo ardhini katika zama za kale sana na wakawapa majina mbali mbali ya kupambanua. Neanderthal - mtu pengine ndiye anayejulikana zaidi miongoni mwa hao. Wa-Neanderthal waliishi zaidi katika Yoropa, Mashariki ya Karibu na Asia ya Kati, baina miaka 100,000 na 35, 000 mpaka sasa. Maiti ya mtu mkamilifu imenguduliwa ambaye mtu huyo aliishi ardhini miaka 29,000 kabla Adamu na Hawa hawajaanza safari yao fupi huko Peponi. Katika zama hizo wanadamu kimaumbile walikuwa kama sisi na waliishi katika Yoropa, Afrika na Asia, na baadaye mnamo zama za Theluji (Ice Age) walienea hadi Marekani pia. Vilevile huko Australia historia thabiti ya utamaduni wa Waaborijini (Aborigines) inaonesha ulianza miaka 40,000 iliyopita kutoka leo. Waaborijini ni watu wa asili ya Australia.

Kwa kulinganisha na zama za hivi majuzi, mifupa yote ya mwili ikiwa pamoja, ya mwanamke, imepatikana huko Hedar katika Ethiopia ambayo mifupa hiyo ni ya tangu miaka milioni 2.9. Sasa kwa kulingana na matukio ya historia yalivyoelezwa katika Biblia, Adamu na Hawa waliishi karibu miaka 6,000 tu tangu leo. Mtu aweza kuangalia nyuma kwa mshangao taarifa ya historia ya wanadamu, ama Homo Sapiens wanavyoitwa katika istilahi ya Kisayansi.

## MATESO YA BINADAMU YAENDELEA:

Akiisha soma maelezo ya Biblia kuhusu walivyoadhibiwa Adamu na Hawa, mtu hana budi kustaajabu kama kweli uchungu wa kuzaa haukujulikana kwa mwanamke hadi zama za Adamu na Hawa zilipoanza. Mwanasayansi yeyote hawezi kukurubia kuwaza mawazo kama hayo yasiyo ya kweli. Isitoshe, tunao ushahidi mwingi usiyoweza kukanushwa ya kwamba, muda mrefu hata kabla ya Adamu na Hawa hawajapatikana, wanadamu walikuwa wanaishi katika mabara yote ya dunia, hata huko visiwa vya Bahari ya Pasifiki vilivyo mbali kabisa, na daima walijibidiisha sana ili kupona katika hatari. Kwahiyo kusema kwamba Adamu na Hawa walikuwa watu wa kwanza kutenda dhambi kwa sababu hiyo sheria ya kumwadhibu mwanamke kwa uchungu wa kuzaa iliundwa, kumethibitika kwamba ni batili kabisa, hakuna msingi wake, tukitaali maisha ya binadamu. Hata wanyama wa daraja la chini zaidi wanajifungua kwa uchungu. Kama mtu akishuhudia ng'ombe akimzaa ndama, ataona ya kwamba uchungu wake unafanana na uchungu wa mwanamke akizaa. Wanyama wengi sana mno wa aina hiyo twajua walipatikana juu ya uso wa ardhi mamilioni ya miaka kabla ya Adamu na Hawa.

Kuchuma riziki kwa taabu ni jambo la kawaida kwa mtu, lakini haihusikani na wanaume pekee bali hata wanawake pia wanapata taabu kwa kuchuma riziki zao. Tangu zamani kila kiumbe hujipatia riziki yake kwa kujibidiisha na kusumbuka. Hakika hiyo

ndiyo iliyosababisha kuleta mabadiliko na maendeleo katika uhai. Kujibidiisha ili kubaki hai ndiyo pengine kipambanuzi kinachopambanua baina ya kilicho hai na kisichokuwa na uhai. Hiyo ndiyo kanuni ya kawaida isiyohusikana na dhambi.

Kama hiyo ndiyo adhabu iliyotolewa kwa sababu ya dhambi waliyotenda Adamu na Hawa, basi mtu atashangaa itatokea nini baada ya kafara yaani baada ya dhambi hiyo kufutiliwa mbali. Kama Yesu Kristo alikuwa amefutilia mbali dhambi za watu wenye dhambi, je, adhabu iliyotolewa kwa Dhambi ya Adamu na Hawa iliondolewa baada ya tukio la Msalaba? Je, wale wanawake waliomwamini Yesu Kristo kuwa 'Mwana wa Mungu' hawasikii sasa uchungu wakati wa kuzaa? Na je, wanaume waumini wameanza kuchuma riziki zao pasipo kujibidiisha kufanya kazi kwa mikono? Je, tabia ya kutenda dhambi iliishia papo hapo pasipo kuingia ndani ya vizazi vingine na watoto wasio na dhambi wakaanza kupata kuzaliwa? Kama majibu ya maswali yote hayo ndiyo 'Naam', hapo bila shaka kuna sababu kiasi fulani ya kutafakari kwa makini falsafa ya Kikristo kuhusu Dhambi na Kafara yake. Lakini, ole wako, majibu ya maswali hayo yote ni: Hapana, hapana tena hapana! Kama lolote halikupata kubadilika tangu tukio la Msalaba katika ulimwengu wa Wakristo na wasio Wakristo, basi Kafara ina maana gani tena?

Hata baada ya Yesu kusulibiwa, uadilifu unamtuma mtu duniani kote ya kwamba mtu yeyote akitenda dhambi, aadhibiwe yeye huyo tu aliyefanya dhambi hiyo pasipo kuwaadhibu wengine. Wanaume na wanawake wote watasumbuka kwa sababu ya dhambi zao wao wenyewe. Watoto huwa wanazaliwa bila ya dhambi. Kama hiyo siyo sawa, basi uadilifu wa Mungu unatupiliwa mbali.

Sisi tukiwa Waislamu tunaamini ya kwamba vitabu vyote vya Mungu vina msingi juu ya ukweli wa daima wala hakuna awezaye kudai dhidi yake. Tunapoona hitilafu katika kitabu kimojawapo miongoni mwa vitabu vinavyodaiwa kuwa vya Mungu, hatukikani

moja kwa moja bali twashika njia ya kukichunguza kwa uangalifu na kwa upole. Maneno mengi ya Agano la Kale na Agano Jipya tunayoona ni dhidi ya ukweli wa kawaida, hapo kwanza twajaribu kuyachukua hayo kimithali na kimafumbo, ama twayakataa tukifahamu kwamba hiyo sehemu imeingizwa na watu humo ndani wala siyo maneno ya Mungu. Ukristo ukiwa dini ya kweli usingekuwa na upotevu, mambo na itikadi zisizokubalika zilizo dhidi ya kanuni ya ulimwengu. Ndiyo sababu hatukuanzia na uchunguzi wa matini ya Biblia, bali tukaanzia na imani za kimsingi ambazo imani hizo zilikubaliwa na ridhaa ya watu wote kuwa sehemu za lazima za falsafa ya Kikristo. Kitu cha kwanza kabisa katika itikadi hizo ni muradi wa Kikristo wa Dhambi na Kafara. Mimi naamini kwamba mtu fulani wakati fulani katika historia ya Ukristo alielewa vibaya mambo na akajaribu kuyafafanua sawa na ujuzi wake na akawa sababu ya kuvipoteza vizazi vijavyo.

**DHAMBI YA KURITHIWA:**

Hebu tufikirie kwa shabaha ya kuhojiana ya kwamba Adamu na Hawa walifanya dhambi hasa jinsi ilivyoelezwa katika Agano la Kale. Adhabu yake, inavyoelezwa katika kisa, haikutolewa kwao pekee bali hata kwa wazao wao wote. Kama adhabu hiyo ilikwisha amuliwa na kutolewa tayari, ilikuwa haja gani tena ya adhabu nyingine yoyote? Kama adhabu imekwisha tolewa kwa dhambi moja, basi habari ikaisha. Hukumu ikiisha tolewa tayari, mtu yeyote hana haki ya kuendelea kuongeza daima adhabu nyinginezo. Katika kesi ya Adamu na Hawa siyo kwamba walilaumiwa tu vikali sana kana kwamba walitenda jambo lililozidi kuliko dhambi inayotolewa adhabu, bali hata aina ya adhabu waliyotolewa ambayo iliendelea kwa wazao wao pia siyo barabara kabisa. Kuhusu hiyo tumekwisha eleza vya kutosha. Tunalojaribu kulidokeza ni uvunjaji wa uadilifu halisi unaochukiza sana sana. Kuadhibiwa kwa kudumu kwa dhambi

walizotenda babu zetu ni jambo tofauti lakini ni chukizo moja kwa moja kulazimishwa kuendelea kufanya dhambi kwa sababu tu babu wa mtu aliwahi kufanya kosa fulani.

Hebu tufikirie hakika tupu ya majaribio ya mtu na kujaribu kuelewa falsafa ya Kikristo ya dhambi na adhabu kwa kulingana na yale tunayoshuhudia kila siku. Tufikirie hukumu aliyotolewa mvunja sheria ambayo hukumu hiyo ni kali zaidi sana kulingana na dhambi iliyotendwa. Kila mtu mwenye akili atailaumu vikali sana hiyo hukumu isiyolingana kabisa na kosa lililotendwa. Kwa hiyo, twaona ni vigumu kuamini ya kwamba adhabu aliyopewa Adamu kwa dhambi yake ilitolewa na Mungu mwadilifu. Hiyo siyo tu habari ya adhabu kutokulingana na dhambi. Hiyo ndiyo adhabu ambayo sawa na ufahamu wa Kikristo wa mwenendo wa Mungu ikaendelea hata baada ya Adamu na Hawa kufariki na kudumu kupatikana kwa wazao wao kizazi baada ya kizazi. Wazao kupata adhabu ya wazazi wao kwa hakika ni kuuvunjilia mbali uadilifu kupita mipaka. Lakini hatuzungumzii hiyo pia. Kama kwa bahati mbaya tukishuhudia jaji mmoja wa zama hizi katoa hukumu iliyowalazimisha watoto wajukuu na vilembwe na kadhalika wa mvunja sheria fulani na kuwashurutisha kisheria kuendelea na dhambi hiyo na kuhalifu na kuadhibiwa kadhalika daima dawamu, itafanyaje jamii ya kisasa ambayo imekwisha tambua maana hasa ya uadilifu kwa sababu ya utamaduni kupata maendeleo?

Msomaji anapaswa kukumbushwa hapa ya kwamba nadharia hiyo ya dhambi ya kurithiwa imeletwa na Bwana Paulo aliyeeleza vibaya sehemu fulani ya maandiko. Hiyo haiwezi kunasibishwa kwa mafundisho ya Agano la Kale. Upo ushuhuda wa kuelemea katika vitabu vingi vya Agano la Kale ulio kinyume chake kabisa. Mnamo karne ya tano, Augustine, Askofu wa Hippo, aliingia katika mapambano na mwendeleo wa (Pelagian Movement) kuhusu majadiliano juu ya hakika ya Adamu na Hawa kuanguka kwa kufanya dhambi. Bwana Askofu alitangaza ya kwamba wafuasi wa mwendeleo wa Pelagius ndio wazushi kwa sababu

wanafundisha ya kwamba dhambi ya Adamu ilimwathiri Adamu tu pekee siyo kizazi kizima cha Adamu kwa ujumla, na kwamba kila mmoja anazaliwa akiwa hana dhambi na anao uwezo wa kuishi maisha yasiyo na dhambi na kwamba walikuwepo watu waliofaulu kuishi pasipo dhambi.
Waliokuwa sawa wakabandikwa jina 'wazushi' . Mchana ukaitwa usiku na usiku ukaitwa mchana . Uzushi ukawa ukweli na ukweli ukawa uzushi.

**KUHAMISHWA KWA DHAMBI:**
Sasa tuchunguze upya habari hii ya kwamba Mungu hawasamehe wenye dhambi bila kuwaadhibu kwani hiyo ni kinyume cha tabia yake ya uadilifu. Mtu anachukizwa kabisa kujua ya kwamba karne baada karne Wakristo wameamini jambo lisiloeleweka kabisa akilini mwa mtu na ni kinyume cha dhamiri ya binadamu. Mungu angewezaje juu ya uso wa ardhi ama huko mbinguni kumsamehe mwenye dhambi kwa sababu tu asiye na dhambi amejitolea kuadhibiwa badala yake? Pindi Mungu afanyapo hilo papo hapo yeye anavunjilia mbali kanuni ya uadilifu. Mwenye dhambi hana budi aadhibiwe kwa dhambi zake. Kwa kifupi matatizo chungu mbovu ya kibinadamu yatazuka ikiwa adhabu itahamishiwa kwa mwingine asiyetenda dhambi.
Wataalamu wa dini ya Kikristo wameleta hoja ya kwamba kuhamishwa dhambi kwa njia hii hakuvunji kanuni ya uadilifu kwa sababu mtu asiye na dhambi amekubali kwa hiari yake kuadhibiwa badala ya mtu aliyetenda dhambi. Wanauliza, mtasemaje kuhusu habari ya mdeni aliyelemewa na deni kubwa sana asiweze kulipa na mja fulani wa Mungu mfadhili anaamua kumwondolea mzigo wake kwa kumlipia deni lake lote? Jawabu letu ni kwamba tutamshangilia kwa kupaza sauti kwa sababu ya tendo lake hilo la ukarimu, huruma na kujitolea sana. Itakuwaje fikira ya mtu anayetukabili akiuliza kama deni linalotakiwa kulipwa ni mamilioni milioni ya pauni za Kiingereza na pale anajitokeza mfadhili anayetoa mfukoni mwake peni moja akitaka

ya kuwa deni lote lile analodaiwa mdeni lifutwe kwani anatoa hiyo peni badala ya deni hilo lote. Habari ya Yesu Kristo kujitoa ili kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote inachekesha kwani dhabihu yake hailingani kabisa kabisa na dhambi chungu mbovu za wanadamu wote. Isitoshe, hapa hamna mdeni mmoja ama wadeni wote wa kizazi kimoja, twazungumzia mabilioni ya wakosefu waliokwisha zaliwa na wengine wasiozaliwa bado lakini watazaliwa mpaka siku ya kiama.

Lakini hiyo siyo basi tu. Kufahamu dhambi kwa mfano wa anayedaiwa fedha na mtu fulani ni kifafanuzi cha kijinga sana cha dhambi nilichowahi kuambiwa. Mithali hiyo tuliyoambiwa inastahili tuifikirie zaidi kabla hatujashughulikia baadhi ya jiha nyingine za dhambi na adhabu.

Hebu tuchukue habari ya mdeni aitwaye 'A' ambaye anatakiwa kumlipa mwingine 'B' pauni 100,000. Kama mfadhili fulani tajiri akiwa na akili timamu anataka kwelikweli kumwondolea mdeni mzigo wa deni, sheria itamtaka amlipe B yote ile anayodaiwa A. Lakini ufikirie kwa mfano ya kwamba mfadhili huyo wa mithali anajitokeza akiomba ya kuwa ndugu A aondolewe wajibu wa kumlipa B na badala yake yeye huyo mfadhili apigwe kidogo ama atiwe kifungoni kwa siku tatu usiku na mchana kwa wingi. Kama hiyo ingetokea kweli katika maisha hasa ingekuwa tafrija kuona nyuso za jaji aliyeshikwa na butwaa na mdai B aliyefadhaika. Lakini mfadhili huyo bado anataka kutimiza huruma yake. Yeye angependa kuleta masharti akisema: Ee bwanangu, hiyo siyo yote nitakayo badala ya kujitolea kwangu. Ninataka wadeni wote popote walipo katika ufalme walio hai leo au watakaozaliwa baadaye mpaka siku ya kiama waondolewe deni zao kwa sababu ya mimi kusumbuka kwa siku tatu, usiku na mchana hapo roho ya mtu inasita kwa kushikwa na butwaa.

Mtu anawezaje kumshauri Mungu, Mungu mwadilifu, ya kwamba wale walionyang'anywa mali yao waliyochuma kwa kutokwa jasho ama wale walioibiwa akiba zao za maisha mazima, walipwe, kwa uchache, hasara zao kiasi fulani. Lakini yaonekana Mungu

wa Kikristo yu mpole sana na mwenye huruma zaidi kwa wahalifu kuliko kuwahurumia wasio na dhambi waliosumbuliwa na wahalifu. Hiyo ni maana ya ajabu ya uadilifu inayosababisha kuwasamehe wezi, wanyang'anyi, wawatendeao vibaya watoto, wanaowaudhi wasio na dhambi na watendao maovu ya kinyama kinyume cha utu, sharti wapate kumwamini Yesu Kristo saa za kukata roho. Katika deni kubwa mno lisilohesabika, kiasi gani hao wanalazimika kuwalipa wale walioteswa? Je, dakika chache za Yesu kukaa katika Jahanamu zaonekana zinatosha kuwatakasa maisha yao marefu ya maovu yachukizayo yanayoendelea kizazi hata kizazi wala hawajaadhibiwa kwayo?

**ADHABU YAENDELEA KUTOLEWA:**

Tufikirie sasa namna nyingine ya dhambi iliyo kubwa zaidi ambayo tabia ya asili ya mtu haiwezi asilani kukubali ya kwamba hiyo iweze kuhamishwa kwa mwingine. Kwa mfano, mtu fulani anamtendea mtoto bila kumhurumia, bali hata analala naye kwa nguvu na kumwua. Hapo utu wa mtu unavunjiliwa mbali kiasi cha juu sana kisichoweza kuvumiliwa. Fikiria kwa mfano ya kwamba mtu huyo anaendelea kuwasumbua na kuwatesa wengine pembezoni mwake pasipo kukamatwa na kuaadhibiwa. Baada ya kuishi maisha yote ya dhambi bila kukamatwa anakurubia mauti lakini anaamua kuepa hata adhabu kubwa zaidi ya Siku ya Hukumu na mwishowe anakata shauri ghafula na kumwamini Yesu kuwa mwokozi wake. Je, madhambi yake yote yatatoweka mara moja naye ataingia katika akhera akiwa hana dhambi kama mtoto aliyezaliwa sasa hivi? Labda mtu huyo anayeahirisha kumwamini Yesu mpaka wakati wa kifo chake ndiye mwenye busara zaidi kuliko yule anayemwamini mapema katika maisha yake. Kwani anayeamini mapema yuko katika hatari ya kutenda dhambi baada ya kuamini na kuangukia hila za shetani na uchongezi wake. Kwa nini usingoje hadi mauti yakukurubie ili usimpe shetani nafasi ya kukunyang'anya imani yako katika

Yesu? Maisha huru yenye dhambi na anasa juu ya ardhi, na kuzaliwa upya katika wokovu wa daima ni nafuu sana kwa hakika. Je, hiyo ndiyo hekima ya uadilifu wanayonasibisha Wakristo kwa Mungu? Uadilifu wa aina hiyo au Mungu wa aina hiyo hakubaliwi kabisa na dhamiri ya mtu ambayo yeye mwenyewe Akaiumba pasipo kupambanua baina ya sawa na isiyo sawa.

Kwa kuangalia swala hilo katika mwanga wa maarifa ya binadamu na fahamu yake, mtu ana kila haki ya kulaumu hiyo falsafa kwamba haina maana wala haina msingi. Hiyo haina hakika wala nguvu. Maarifa ya binadamu yanatuambia ya kwamba ni haki ya wanaosumbuliwa na wengine kuwasamehe ama kutokuwasamehe. Wakati mwingine serikali kwa kusherehekea siku ya taifa ama kwa sababu nyingine zinatangaza msamaha kwa waliozikosea serikali hizo pasipo kuwabagua. Lakini hiyo hairuhusu kuwasamehe wale waliowadhuru wenzao wasio na hatia kwa madhara yasiyoweza kurekebishwa na kuwasumbua kwa kudumu. Kama serikali kutoa msamaha kwa wote pasipo ubaguzi inajuzu kwa vyovyote na kama hiyo haihesabiwi na wataalamu wa dini ya Kikristo kuwa kinyume cha maana ya uadilifu, kwa nini basi hawamwachilii Mungu haki ya kusamehe jinsi apendavyo na wakati apendapo? Kwa vyovyote, Yeye ndiye Mfalme Mkuu, Mwumbaji na Bwana wa kila kitu. Kama Yeye anasamehe yeyote uovu aliomfanyia mwanadamu mwenzake, Bwana Mkuu anao uwezo halisi wa kumlipia kwa wingi sana yule aliyekosewa hadi akaridhika barabara kwa uamuzi wake. Kama ndiyo hiyo, iko wapi basi haja ya kumtoa mwanaye asiye na dhambi kuwa dhabihu?. Hilo lenyewe ndilo kuudhihaki uadilifu. Sisi tumezaliwa tukilingana na sifa za Mungu.Yeye anatangaza katika Biblia takatifu:

> Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu (Mwanzo 1:26).

Kuhusu habari hiyohiyo Yeye anasema ndani ya Kurani Tukufu:

> Fuateni sifa za Mungu ambazo yeye akawaumba watu juu yake (30: 31).

Itikadi hiyo iliyo sawa baina ya Wakristo na Waislamu inaitaka dhamiri ya mtu kuwa picha bora ya tendo la Mungu katika hali fulani. Tunaona kila siku ya kwamba tunasamehe mara nyingi pasipo kuvunja maana ya uadilifu hata kidogo. Kama mtoto anawaudhi wazazi wake kwa kuwaasi, ama kwa kuharibu kitu fulani chenye thamani cha nyumbani, ama kuwaharibia heshima, hapo yeye amewafanyia dhambi. Wazazi wake wanaweza kumsamehe bila ya dhamiri yao kuwachoma au kuwalaumu kwamba wamevunjilia mbali uadilifu halisi. Lakini kama mtoto wao anaharibu mali ya jirani yao, au anamjeruhi mtoto wa mtu mwingine, wazazi wa mtoto huyo mhalifu wanawezaje kuamua kumsamehe mtoto wao kwa kuwasumbua wengine? Hiyo itaonekana ni kitendo kilicho kinyume cha uadilifu hata sawa na dhamiri yao wenyewe kama watamsamehe hivyo.

Dhambi na adhabu zinahusiana jinsi sababu na matokeo vinavyohusiana, na zinalazimika kulingana kiasi fulani. Jiha hiyo ya uhusiano baina ya dhambi na adhabu imekwisha elezwa kiasi fulani kulingana na mtu mmoja kutumia vibaya mali ya mwingine. Ndivyo ilivyo hali ya dhambi nyingine, bali vibaya zaidi, kama vile kuwajeruhi wananchi wasiofanya dhambi au kuwavunja viungo vyao ama kuwaua ama kuvunja heshima zao kwa namna yoyote. Kadiri itakavyokuwa kubwa dhambi, ndivyo itakavyotazamiwa kuwa kubwa adhabu na namna ya adhabu hiyo. Kama Mungu anaweza kuwasamehe watu wote, na ndivyo niaminivyo kwamba Yeye, tena Yeye peke yake anaweza, basi halizuki kabisa suala la kufutilia mbali dhambi kwa kumwadhibu mtu asiyefanya dhambi. Na kama ni suala la kuhamisha adhabu ya mhalifu kwa mtu asiyefanya dhambi aliyekubali kwa hiari kuadhibiwa, basi uadilifu utalazimisha ya kwamba adhabu nzima

nzima ihamishwe kwa huyo mwingine pasipo kupunguza kiasi kiwacho chochote kile. Kuhusu habari hiyo tumekwisha eleza tayari vya kutosha.
Je, Wakristo wanaamini ya kwamba Mungu Baba alitimiza sharti hiyo ya uadilifu kuhusu habari ya Yesu, Mungu Mwana? Kama ni hivyo, basi itamaanisha ya kuwa adhabu zote za wahalifu wote wale waliokwisha zaliwa katika zama za Yesu na hata waliozaliwa baadaye hadi Siku ya Hukumu, zikarundikana pamoja, zikawa nzito na kali sana sawasawa na Jahanamu hata kwamba taabu ya Yesu Kristo aliyopata kwa siku tatu pekee, usiku na mchana, ikawa sawa na shida ya adhabu zote zile walizojichumia wahalifu waliotajwa juu au walizotazamiwa kujichumia mpaka Siku ya Mwisho. Kama ni hivyo, basi Mkristo yeyote hastahili duniani kuadhibiwa na Serikali ya Kikristo. La sivyo, hicho kitakuwa ni kitendo kilicho kinyume kabisa cha uadilifu. Itakalofanya mahakama baada ya kwisha kumhukumu mhalifu Mkristo kwamba amefanya hatia, ni kumwadhibu huyo mhalifu kwamba amwombe Yesu mwana wa Mungu kumwokoa. Na habari hiyo ingemalizika na kuishia papo hapo. Hiyo itakuwa ni habari ya kuhamisha hesabu ya mhalifu kwenye hesabu ya Yesu.

Ili kutoa mfano, hebu tuchunguze hali ya uhalifu ulioenea katika Amerika. Uhalifu wa ujambazi na mauaji umezidi huko na kuenea sana hata kwamba ni vigumu kuweka hesabu yake. Nakumbuka safari moja nilifungua redio nilipokuwa huko New York. Idhaa niliyofungua ilihusikana na kutoa taarifa ya uhalifu mkuu wa mauaji na kadhalika. Taarifa hiyo ilitisha moja kwa moja. Ilikuwa yenye kuudhi sana hata kwamba sikuweza kuvumilia zaidi ya saa moja. Katika kila dakika tano takriban mtu mmoja aliuliwa katika Amerika na kuripotiwa wakati mwingine pamoja na maelezo ya kuogofya mno na wale walioshuhudia mauaji yalipokuwa yanafanywa. Siyo nia yetu kutoa picha kamili ya uhalifu Marekani, lakini wote wanajua ya kwamba siku hizi Amerika iko mbele katika orodha ya nchi ambamo uhalifu wa

kila aina ni jambo la kawaida sana, hususan katika miji mikubwa kama vile Chicago, New York na Washington. Katika New York uharamia ni jambo la kawaida kama ilivyo kukata mikono, miguu ama viungo vingine vya mwili wa wale wasio na hatia ambao wanajaribu kushindana na hao wahalifu ili kujilinda. Matukio hayo ya kila siku yanaleta picha chafu mno ya kulemaza na kuua kwa manufaa madogo.

Achilia mbali kwa kitambo mwenendo unaoendelea kuzidi wa kutenda maovu duniani kote, kuhusu habari ya Amerika peke yake mtu anashangaa kuona jinsi imani ya Wakristo juu ya dhambi na kafara inavyolingana na maovu yanayotendeka kila siku. Hata wakiweza kuwa mbali sana na khulka za Kikristo kwa kitendo, kwa akali wanayo sifa hii ya kwamba wanaiamini itikadi ya Kikristo ya Dhambi na Wokovu na kwamba Yesu ndiye mwokozi wao, lakini nasikitika hiyo yote ni bure. Wahalifu wengi zaidi katika Amerika ndio wanaojiita Wakristo, ijapokuwa Waislamu na wengineo pia ndio hivyo hivyo. Lakini, je, kwa sababu tu wahalifu hao wanahusikana na Ukristo na wanaamini katika fidia inayosemekana aliitoa Yesu Kristo kwa hiari yake kwa ajili ya waumini wenye dhambi, watasamehewa wote hao na Mungu? Kama ndiyo, kwa njia gani? Mwishowe, asilimia kubwa ya hao wanaweza kukamatwa na kuadhibiwa na sheria ya nchi. Lakini hata hivyo wengi zaidi hawatakamatwa ama wanaweza kupata adhabu kwa sehemu ya madhambi waliyotenda katika muda wa miaka mingi.

Ukristo utawatolea nini hao wanaoadhibiwa na sheria, na utawaahidia nini wale ambao hawakuweza kushikwa hapa duniani? Je, hao wote wa aina mbili watapewa adhabu tofauti ama wataadhibiwa namna moja pasipo tofauti?

Hapa pana mashaka mengine tena kuhusu wokovu wa mhalifu kwa sababu ya yeye kumwamini Yesu Kristo. Mashaka hayo yanasababishwa na hali isiyo wazi sana wala haikupambanuka. Kama, kwa mfano, Mkristo mmoja anamsumbua mtu asiyekosa ambaye si Mkristo, hapo huyo Mkristo atasamehewa kwa sababu

ya baraka za imani yake katika Yesu. Adhabu ya dhambi yake itahamishwa na kuingizwa katika hesabu ya Yesu. Lakini itakuwa nini hesabu ya faida na hasara ya yule maskini aliyekosewa ambaye si Mkristo? Yesu maskini na yule maskini aliyesumbuliwa wakaadhibiwa kwa dhambi wasiyotenda wao.

Akili yetu inafadhaika kama tukijaribu kuwaza wingi ule wa madhambi yaliyokwisha tendwa na watu tangu Ukristo kufika duniani na yataendelea kutendwa mpaka Siku ile ya Mwisho. Je, dhambi hizo zote huingizwa katika hesabu ya Yesu, amani na baraka za Mungu ziwe kwake? Je, Yesu alikwisha adhibiwa tayari barabara kwa madhambi hayo yote katika muda mfupi wa siku tatu, usiku na mchana, inavyosemekana kwamba Yesu akasumbuka kwa huo muda? Bado mtu anashangaa ya kwamba namna gani bahari kubwa kabisa ya wahalifu iliyofanywa kuwa chungu moja kwa moja na sumu ya madhambi, ikawa tamu na kutakaswa kwa kuondolewa mbali matokeo ya madhambi yao kwa sababu tu ya wao kumwamini Yesu. Isitoshe, fikara ya mtu inampeleka nyuma sana katika zama ambapo maskini Adamu na Hawa waliwahi kutenda dhambi yao ya kwanza kwa kukosa kuamua vizuri kwa sababu walidanganywa kwa hila na kutegwa na Shetani. Kwa nini dhambi yao haikuondolewa pia? Je, hawakuwa na imani katika Mungu? Je, ni wema hafifu kumwamini Mungu Baba? Na je, ni kosa lao ya kwamba hao hawakuambiwa habari ya Mwana kuwa na Mungu Baba milele? Kwa nini 'Mungu Mwana' hakuwahurumia hao na kumwomba Mungu Baba amwadhibu yeye kwa dhambi zao badala ya kuwaadhibu wao? Mtu anawezaje kupenda kilichotendeka, kwani ingekuwa rahisi zaidi kuadhibiwa kwa kosa lililofanywa kwa dakika moja pekee na Adamu na Hawa. Kisa kingine kabisa cha binadamu kingepata kuandikwa katika kitabu cha bahati. Ingeumbwa ardhi ya kipeponi na Adamu na Hawa wasingelifukuzwa kutoka Peponi kwa kudumu pamoja na wazao wao wenye majonzi wasiohesabika. Badala yao Yesu angeondoshwa kutoka Peponi kwa muda mfupi wa siku tatu, usiku

na mchana. Basi tu. Ni sikitiko kwamba Mungu Baba hakupata wazo hilo wala Yesu. Angalieni jinsi hakika tukufu ya kupendeza ya Yesu imegeuzwa kuwa kisa cha kuchekesha na jambo la kubuniwa lisiloweza kuaminika.

**UADILIFU NA MSAMAHA:**

Falsafa ya Kikristo ya Dhambi na Adhabu siyo tu inaibumbuaza moja kwa moja akili ya mtu mwadilifu asiyependelea, bali pia inazusha maswali yanayohangaisha sana. Falsafa ya uhusiano baina ya uadilifu na msamaha, inavyothibitishwa na falsafa ya Kikristo ya Kafara, inajaribu kueleza kwa nini Mungu Mwenyewe hakuweza kusamehe. Hiyo inalitegemea wazo kosefu lisilofuata kanuni kuhusu uadilifu. Wazo hilo limechukuliwa kuwa kweli kabisa ya kwamba uadilifu na msamaha haviendi pamoja. Kama ni hivyo, kwa nini, basi, Agano Jipya linasisitiza sana kusamehe pindi uhusiano wa watu wao kwa wao unapozungumzwa? Sijasoma katu katika kitabu cho chote cha Mungu cha dini yoyote duniani fundisho linaloelekea zaidi upande mmoja na kukazania kupita kiasi kusamehe.

Tofauti sana mno iliyoje hilo na ule mkazo juu ya uadilifu unaopatikana katika mafundisho ya Kiyahudi. Jicho kwa jicho; jino kwa jino. Huo ndiyo uadilifu - halisi, usiyo na matata, usiopunguzwa thamani. Ajabu iliyoje kuachana na fundisho hilo na kushikilia fundisho la Kikristo la kugeuza shavu la pili kama shavu moja limepigwa kofi. Nani alifundisha fundisho la pili lililo dhidi ya fundisho la zamani la Torati? Mtu anashikwa na butwaa ya kwamba je, fundisho hilo la zamani lilifundishwa na Mungu Baba lipingwalo moja kwa moja na fundisho la Agano Jipya lililofundishwa na 'Mwana wa Mungu'? Kama ndivyo hivyo, kwa nini 'Mungu Mwana' akahitilafiana vikali sana na Mungu Baba? Je, kupingana huko kuchukuliwe kuwa dosari ya kuzaliwa ama mageuzi ya maendeleo? Au mwenendo huu wa kusamehe moja

kwa moja unaopingana vikali na mkazo wa kujilipiza kisasi sawa na mafundisho ya Kiyahudi unahakikisha mabadiliko katika Mungu Baba? Yeye anaonekana amejuta sana kwa mafundisho aliyompa Musa na watu wa Kitabu na anaonekana kwamba amependa kurekebisha kosa alilowahi kulifanya. Sisi tukiwa Waislam, twashuhudia uhamisho wa huo mkazo, lakini hatuoni tofauti, kwani tunamwamini Mungu ambaye amejikusanyia sifa zote mbili za uadilifu na msamaha bila ya sifa hizo mbili kupingana zenyewe kwa zenyewe. Sisi tunaona kulihama fundisho la Kiyahudi na kuhamia fundisho la Yesu Kristo siyo kwa shabaha ya kulirekebisha fundisho lenyewe la kwanza, bali matumizi yake mabaya na Mayahudi. Kwetu sisi Mungu siye tu Mwadilifu bali Yu Msamehevu, Mrehemevu na Mpaji pia. Kama Yeye akitaka kusamehe hahitaji msaada wa nje ili kumsamehe mwenye dhambi. Lakini sawa na nadharia ya Kikristo hilo ni tatizo kubwa kabisa. Inaonekana kwamba Mungu wa Torati ndiye Mungu anayejua uadilifu pekee asiyetambua huruma na rehema. Kidhahiri yeye hakuwa na uwezo wa kusamehe hata akitaka sana namna gani kusamehe. Kumbe akaja tena Mungu Mwana kumsaidia na kumwokoa katika tatizo baya sana. Yaonekana 'Mungu Mwana' alikuwa mwenye huruma tupu kinyume cha Baba yake Mwenye kujilipiza kisasi siku zote. Huo siyo tu ubovu dhahiri wa busara hiyo ya 'Mwana' inayotatiza dhamiri ya mtu bali huo unazusha mara nyingine swala la upingamizi katika mienendo yao. Yesu haonekani kuwa mwana halisi wa Baba yake. Labda kosa fulani liliingia katika uzazi.

Hapa pana suala jingine la muhimu kuhusu dini nyinginezo za ulimwengu ya kwamba dini hizo zinafikirije dhambi na matokeo yake. Bila shaka Ukristo peke yake siyo dini iliyofunuliwa na Mungu. Wasio Wakristo wanawazidi Wakristo katika idadi. Maelfu ya miaka kabla ya historia ya binadamu inayojulikana, dini nyingi zilizalika na kuimarika baina ya watu katika sehemu mbali mbali za dunia kabla hajaja Yesu Kristo duniani. Je, dini hizo zilizungumzia falsafa ya msamaha hata mara moja kwa

kufungamanisha msamaha na itikadi ya Kikristo juu ya Kafara? Dini hizo zilifundisha imani gani kumhusu Mungu , ama miungu kama ilivyoanza kuaminiwa sasa? Nini imani yao kuhusu mwenendo wa Mungu kwa watu wenye dhambi ?

Miongoni mwa dini mbalimbali, labda dini ya Kihindu ndiyo karibu kiasi fulani na Ukristo kuhusu habari hiyo. Wahindu pia wanamwamini Mungu Mwadilifu Halisi ambaye uadilifu wake unamlazimisha kumwadhibu mwenye kutenda dhambi kwa njia hii au ile. Lakini kulingana kunaishia hapo hapo. Hamna habari ya Mungu Mwana mwenye kuchukua mabegani mizigo ya adhabu za ulimwengu mzima wa watendao dhambi. Hata habari hiyo haijadokezwa katika dini hiyo. Kinyume chake twaambiwa ya kwamba mtu kwa sababu ya kutenda dhambi nyingi anaadhibiwa kwa njia hii ya kwamba roho yake inarudishwa mara kwa mara duniani katika kiwiliwili cha wanyama mbali mbali. Yaani kwa shabaha ya kuadhibiwa, mtu anapokufa anazalika tena duniani kwa mfano wa sura ya mbwa ama kuku au mbuzi na kadhalika. Hiyo inaitwa 'Tanasukhi' au kwa Kiingereza *Reincarnation.* Ndiyo kusema kwamba mtu anatakasika katika dhambi alizowahi kuzitenda kwa kuzalika mara nyingi sana duniani kwa sura ya wanyama mbalimbali hadi hesabu yake ya dhambi inakamilika. Baadhi ya watu wanaweza kufadhaika na habari hiyo na kutatanika; lakini kwa vyovyote ndani ya falsafa hiyo mna uadilifu. Nadharia hiyo bila shaka inaafikiana na imani ya uadilifu halisi.

Kwa kuachilia mbali dini ya Kihindu na nyinginezo zinazoitetea falsafa ya 'Tanasukhi' pamoja na matatizo ya 'sababu' na 'matokeo' yake, hebu tuone msamaha wa Mungu ukoje sawa na mafundisho ya dini zingine kubwa ama ndogo za ulimwengu? Dini hizo zote pamwe na bilioni moja ya wafuasi wa dini hizo kama vile dini ya Kihindu huonekana hawana habari kabisa ya wazo la kubuniwa la Kafara. Hiyo kweli inabumbuaza sana. Alikuwa nani mahali pengine katika dini nyingine aliyewafunulia watu wahyi? Kama siye Mungu Baba ilivyo katika imani ya Kikristo basi je viongozi

wote wa dini zote isipokuwa Yesu Kristo walikuwa wanafunzi wa shetani? Na Mungu Baba alikuwa wapi? Kwa nini hakuja kuokoa wakati watu wengine walikuwa wanapotezwa na shetani kwa jina lake Yeye? Ama watu hao wote wengine waliumbwa na mwingine minghairi ya Mungu Baba? Tena, kwa nini aliwatendea kama baba wa kambo na kuwaachilia wapotezwe na shetani?

Sasa tugeukie suala hilo na kuliangalia sawa na majaribu yetu ya kila siku. Inaweza kuhakikishwa ya kwamba uadilifu na msamaha viko sawasawa na vyaweza kukaa pamoja na kwamba havipingani siku zote. Wakati mwingine uadilifu unataka msamaha utolewe, na pengine unadai kwamba msamaha ukataliwe. Kama mtoto akipata moyo wa kuhalifu zaidi pindi asamehewapo, hapo msamaha unaulanda uhalifu na kwa hiyo ni kinyume cha shabaha ya uadilifu. Kama mhalifu anasamehewa na matokeo yake ni kwamba yeye mhalifu huyo anazidi kufanya matendo ya uhalifu na kuwaudhi watu pembeni mwake na kuwadhulumu eti kwa sababu atasamehewa tena, basi msamaha huo utakuwa dhidi kabisa ya uadilifu na utakuwa sawa na kuwadhulumu raia wasio na hatia. Wako wahalifu wa aina hiyo wasiohesabika wanaositiriwa na kafara ya Yesu. Hiyo yenyewe ndiyo kinyume cha uadilifu. Lakini kama mtoto fulani anajuta, kwa mfano, na mama yake ana hakika kwamba mwanaye hatarudia hilo kosa tena, hapo kumwadhibu huyo mtoto itakuwa kinyume cha muradi wa uadilifu. Mtu mwenye kutubu anapojuta, majuto hayo yenyewe huwa adhabu kwake ambayo wakati mwingine ni kali zaidi kuliko ile adhabu ambayo yeye angeweza kupewa. Wenye dhamiri hai siku zote husumbuka rohoni baada ya kufanya dhambi. Na mtu akijuta na kuudhika rohoni mara kwa mara kwa sababu ya makosa yake na moyo wake unachomwa sana mno, aweza kufikia hali fulani hata kwamba Mungu anamwonea huruma huyo mja wake mnyonge akoseaye siku zote na kutubu kila mara. Hilo ndilo somo katika uhusiano baina ya uadilifu na msamaha wanalopata wenye akili nyingi na wale wenye fahamu ya kawaida kwa usawa kwa kushuhudia yanavyofanyika maishani. Wakati umewadia sasa

kwamba Wakristo wazinduke katika usingizi wa kuamini itikadi ya Kikristo pasipo kuihoji hekima yake.
Kama wakichunguza upya itikadi ya Kikristo kwa kutumia akili na hoja, bado wanaweza kubaki kuwa Wakristo wema lakini wa aina nyingine na wapendao hakika zaidi. Hapo watakuwa na imani zaidi na mapenzi na kujitolea zaidi kwa Yesu akiwa binadamu halisi kuliko Yesu wa kuzushwa na mawazo yao asiye zaidi ya kitu cha kubuniwa. Adhama ya Yesu haimo katika kisa chake cha kubuniwa bali katika dhabihu yake kuu akiwa mwanadamu na Mtume. Dhabihu yake inaathiri moyo kwa nguvu sana mno kuliko kisa chake cha kubuniwa cha kufa msalabani na kufufuka katika wafu baada ya kukaa motoni kwa saa chache za kutisha.

**YESU HAWEZI KUWA KAFARA :**
Jambo la mwisho lakini la maana ni kwamba Yesu angewezaje kuzaliwa akiwa hana dhambi ilhali alikuwa na mama wa kibinadamu? Kama dhambi ya Adamu na Hawa ilikwisha kichafua kizazi cha hao wawili wenye bahati mbaya, basi matokeo yake ni kwamba wazao wao wote wa kiume na wa kike walirithi maelekeo ya kufanya dhambi katika kuzaliwa kwao. Labda wanawake wakarithi zaidi shauku ya kutenda dhambi kwa sababu Hawa ndiye aliyetumiwa na shetani ili kumbembeleza Adamu kutenda dhambi. Kwahiyo, Hawa anahusika na dhambi moja kwa moja kuliko pengine Adamu. Katika habari ya kuzaliwa Kristo, binti wa Hawa alihusikana zaidi. Swali linalozuka kwa nguvu sana ni kwamba je, Yesu alirithi kromosom zenye vijine, (genes) kutoka kwa mamake binadamu ama hapana? Kama ndiyo, hapo haikuwezekana kwa Yesu kuepukana na dhambi ya lazima ya kurithiwa. Kama hakuirithi kromosom yoyote kutoka kwa mamake wala kwa Mungu Baba, hapo kuzaliwa kwake kutakuwa mwujiza maradufu. Mwujiza pekee yake unaweza kuzalisha mwana asiyehusikana na baba yake wala mamake. Jambo

lisiloeleweka ni kwamba kwa nini kromosom za Hawa hazikumtilia mwanaye Yesu maelekeo ya kiasili ya kutenda dhambi. Tukidhani kwamba ilikuwa hivyo kwa vyovyote na Yesu alikuwa safi asiye na dhambi - jambo ambalo ni lazima ili kujichukulia dhambi za wanadamu sharti wamwamini, hapo swali jingine litazuka: Walikuwaje, mtu aweza kuuliza, waliokufa miongoni mwa wazao wa Adamu na Hawa kabla haujafika Ukristo? Mabilioni mangapi ya watu hao waliwahi kutawanyika duniani kote katika mabara matano kizazi baada ya kizazi. Lazima waliishi na wakafa pasipo kutumaini bali pasipo uwezekano wa kusikia habari ya Kristo, Mwokozi wao, ambaye alikuwa hajazaliwa. Kwa hakika wanadamu wote waliokuwapo baina ya Adamu na Kristo wanaonekana waliangamia kwa kudumu. Kwa nini hao hawakupewa nafasi walau hafifu sana ya kusamehewa? Je, hao watasamehewa na Yesu Kristo kwa kutumia kanuni ya kafara kwa waliopita kabla ya kanuni hiyo kuundwa? Kama ndiyo, kwa nini?

Katika sehemu nyingine za dunia zilizo kubwa zaidi kuliko Uyahudi ilivyo ndogo sana, haikupata kusikika habari za Ukristo hata katika zama za uhai wa Yesu Kristo; watu hao watakuwaje? Maana hawakuamini 'Uana' wa Yesu Kristo wala hawangeweza. Je, wataadhibiwa kwa madhambi yao ama hapana na kwa hoja gani? Walikuwa na nafasi gani kwa vyovyote? Walikuwa hoi kabisa. Maana mbovu iliyoje hiyo ya Uadilifu!

**KUTOA DHABIHU PASIPO KUPENDA :**

Sasa na tugeukie kuchunguza tukio la msalaba. Hapo twalikabili tatizo lisiloweza kutatulika. Tunavyoambiwa kwa kusisitiza ni kwamba Yesu alijitolea kwa hiari yake mbele ya Mungu Baba na akasukumiziwa madhambi ya wanadamu wote sharti wamwamini kwanza. Lakini saa ya upendo wake kukubaliwa unaposogelea karibu na mwanga wa tumaini la wanadamu wenye dhambi

unapoanza kumulika kama mapambazuko ya alfajiri, twamgeukia Yesu tukitazamia kushuhudia uchangamfu wake na furaha yake na shangwe yake ya hali ya juu sana katika wakati wa muhimu kabisa katika historia ya binadamu, tunasikitikaje sana na kuvunjika moyo moja kwa moja! Badala ya kumkuta Yesu akingojea saa ya furaha kuu, twamwona akilia na kupaza sauti na kuomba na kumsihi Mungu Baba ili kimwepuke kikombe cha mauti. Yeye akamkaripia vikali sana mwanafunzi wake mmoja alipomkuta akisinzia baada ya kupitisha mchana mrefu wa hatari na kusumbuka usiku wa majonzi ambao ukamchosha vibaya yeye na bwana wake. Biblia inasimulia habari hiyo kama ifuatavyo:

> Kisha Yesu akaenda pamoja nao mpaka bustani iitwayo Gethsemane akawaambia wanafunzi wake, ketini hapa hata niende kule nikaombe. Akamchukua Petro na wale wana wawili wa Zebedayo, akaanza kuhuzunika na kusononeka. Ndipo akawaambia, Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa; kaeni hapa, mkeshe pamoja nami. Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe. Akawajia wale wanafunzi, akawakuta wamelala, akamwabia Petro: Je, hamkuweza kukesha pamoja nami hata saa moja? Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu. Akaendelea tena mara ya pili, akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa, mapenzi yako yatimizwe. Akaja tena akawakuta wamelala; maana macho yao yamekuwa mazito. Akawaacha tena, akaenda, akaomba mara ya tatu, akisema maneno yaleyale. (Mathayo 26: 36- 44).

Ni masikitiko, kinavyotoboa kisa hiki cha Kikristo, ya kwamba kurongaronga kwa Yesu wala kwa wanafunzi wake hakukubaliwa na Mungu Baba, na japo akateta sana lakini akasulubishwa shingo upande. Je, huyo ndiye yule yule mfalme asiyekosa, na upeo wa mwisho wa dhabihu, aliyejitolea mhanga sana ili kubeba mizigo ya madhambi ya wanadamu wote mabegani pake, ama yu mtu tofauti? Mwenendo wake, ilipowadia saa ya kutundikwa

msalabani na wakati aliposulubishwa, unatia shaka sana kwamba aliyesulubishwa kweli alikuwa Yesu au kwamba kisa chenyewe hicho kweli ni sawa kilichobuniwa kumhusu yeye. Lakini hilo tutalijadili baadaye. Wakati huu tugeukie pale tulipoacha uchunguzi wetu.

Maswali mengine yanayozuka kutokana na kilio cha mwisho cha Yesu katika hali ya kuteswa ndiyo haya: Ni nani aliyetamka hayo maneno ya kutia majonzi na kuhuzunisha? Alikwa Yesu-mtu ama Yesu 'Mwana'?

Kama huyo alikuwa ni Yesu mtu aliyeachwa (Mungu wangu, Mungu wangu mbona umeniacha) basi kaachwa na nani? Na kwa nini? Kama alikuwa Yesu mtu, hakuna budi basi ya kwamba yeye alikuwa hadi mwisho nafsi ile ile moja inayojitegemea aliyeweza kufikiria na kuhisi mwenyewe pasipo kizuizi chochote kiwacho. Je, yeye alikufa wakati roho ya Yesu Mwana wa Mungu ilipotengana na mwili wa aliokuwa ameuchukua yeye? Kama ndiyo, kwa nini na kwa namna gani? Kama ni hivyo, na ilikuwa ni kiwiliwili cha mtu kilichokufa baada ya roho ya Mungu kukitoka, basi swali linazuka hapo ya kwamba nani alifufuka katika wafu pindi roho ya Mungu ilipouingia mwili huo huo baadaye.

Tena, habari hiyo itatuongoza kuamini ya kwamba siye Yesu 'Mwana' aliyekuwa anasumbuka, bali ni Yesu mtu aliyepaza sauti katika hali ya kuteswa na ndiye aliyeudhika ilhali Yesu 'Mwana' aliangalia tu akitepetea asijali. Hapo anawezaje kudai ya kwamba yeye akiwa 'Mwana' alisumbuka kwa ajili ya wanadamu wala siye yeye akiwa mtu?

Naam, kama tukidhani ya kwamba alikuwa ni Yesu 'Mwana' aliyepaza sauti ya kilio ilhali 'mtu' ndani yake pengine akitumaini kuanza maisha mapya akaangalia tu akitazamia pasipo hakika ya kwamba pamoja na Yesu 'Mwana' kutoa dhabihu, yeye Yesu mtu naye atachinjwa, apende asipende, pamoja na mwenzake asiyekosa. Uadilifu gani ulimhimiza Mungu kupata shabaha mbili kwa hila moja? Hiyo labda ni siri nyingine.

Kama huyo alikuwa Yesu 'Mwana', na kweli alikuwa huyo kwa kulingana na maoni ya makanisa ya Kikristo, hapo litazuka swali jingine kutokana na jawabu la swali la kwanza ya kwamba alikuwa nani ambaye Yesu alizungumza naye (Mathayo 26:39, 42). Twaweza kuchagua rai mojawapo katika rai mbili:

Ya kwanza ni kwamba 'Mwana' alikuwa anaongea na Baba akilalamika kwamba ameachwa katika wakati wa haja. Hiyo haina budi kutuongoza kuamini ya kwamba hao walikuwa wawili mbali mbali wasiokuwapo pamoja katika dhati moja wakishirikiana kwa usawa katika sifa zote na kuzitumia kwa pamoja kwa usawa. Mmoja katika hao anaonekana kuwa mwamuzi mkuu, mweza, mwenye nguvu ya mwisho ya kutoa hukumu. Na mwingine yule 'Mwana' maskini, anaonekana amenyimwa kabisa ama pengine akaondolewa kwa muda ile tabia ya kupiga ubwana aliyokuwa nayo Baba. Kiini cha habari kinachotakiwa kuzingatiwa ni kwamba matakwa yao na matilaba yao yanayopingana hayaonekani yakizozana na kuhitilafiana zaidi kuliko yalivyokuwa wakati wa kitendo cha mwisho cha kisa cha msalaba.

Swali la pili ni kwamba je, hao wawili mbalimbali, wakiwa na maoni tofauti, khulka tofauti na sifa tofauti wataona taabu na udhia wakiwa 'wawili katika mmoja' ama 'mmoja katika wawili'? Basi swali jingine litahitaji maongezi marefu baina ya wataalamu wa dini ya kwamba je, upo uwezekano wa Mungu kupata kusumbuka na kuadhibiwa? Hata kama upo uwezekano huo, Mungu nusu tu ataudhika ilhali nusu nyingine ya Mungu hataweza kupata taabu kwa sababu pengine kwa mpango maalum ama kwa sababu ya kulazimika kwa tabia yake ya asili. Na tunaposogelea mbele katika ulimwengu huu wa wasiwasi wa falsafa hiyo iliyopotoka, mwanga unaanza kufifia zaidi na zaidi na tunakuta bumbuazi juu ya bumbuazi.

Lipo tatizo jingine tena. Kristo alikuwa anaongea na nani kama yeye mwenye alikuwa Mungu?. Alipoongea na Baba, yeye mwenyewe alikuwa sehemu isiyotenganishwa na Baba; ndivyo tuambiwavyo. Basi alikuwa anasema nini na kumwambia nani?

Swali hilo linatakiwa lijibiwe kwa dhamiri huru pasipo kuikimbilia itikadi. Hiyo inakuwa itikadi hapo tu ambapo haiwezekani hiyo kufafanuliwa sawa na akili ya kibinadamu. Kwa kulingana na usemi wa Biblia, Yesu alipokuwa atoe roho yake akalia akimwambia Mungu Baba: Mbona umeniacha? Nani alimwacha nani? Je Mungu alimwacha Mungu?

## NANI ALITOLEWA KUWA DHABIHU ?

Tatizo jingine tunalokuta ni kwamba 'mtu' katika Yesu hakuadhibiwa wala asingeweza kuadhibiwa kwa mantiki yoyote kwani yeye hakujichagulia kubeba mzigo wa dhambi za wanadamu wote. Hiyo habari mpya kuingia katika mjadala inatuongoza kwenye hali maalum ambayo hatukuizungumzia hapo kabla. Mtu analazimika kushangaa juu ya uhusiano wa 'mtu' katika Yesu akiwa na maelekeo ya kutenda dhambi tangu kuzaliwa ambayo maelekeo hayo yanapatikana kwa kizazi chote cha Adamu na Hawa. Kwa wingi mtu anaweza kujielekeza kuamini ya kwamba katika uwili wa 'Mungu Mwana' na 'mtu' wakiwa ndani ya kiwiliwili kimoja 'Mungu Mwana' peke yake ndiye asiyekuwa na dhambi. Lakini ikoje hali ya 'mtu' aliyekuwepo pamoja naye? Je, yeye naye alizaliwa kutokana na vijine (genes) vya Mungu na sifa zake? Kama ndiyo, basi yeye analazimika kutenda kama Mungu katika Yesu na udhuru wowote hautakubalika kama akilegea au akiwa ajizi asitende kama Mungu eti kwa sababu alikuwa binadamu. Kama hakuwa na sifa yoyote ya Mungu, yaani yule 'mtu' aliyekuwa ndani ya Yesu hakuwa na sifa yoyote ya Mungu, basi hatuna budi kukiri ya kwamba yeye alikuwa binadamu wa kawaida tu, au labda binadamu nusu. Hata hivyo 'mtu' huyo akiungamana na Yesu atalazimika kuwa
binadamu wa kutosha kurithi tabia ya kutenda dhambi. Kama hapana, kwa nini hapana?

Ni wazi ya kwamba haifai kusema kuwa yeye akiwa 'mtu' tofauti na mwenzake Mungu, atakuwa amefanya dhambi kwa kujitegemea akimtupia lawama yote huyo 'mtu' ndani yake. Mfululizo huo wa matukio hautakamilika pasipo kumwona Yesu 'Mwana wa Mungu' akitoa roho siyo sana bila ubinafsi, wala siyo kwa ajili ya wanadamu wote, bali shabaha yake kubwa pengine ndiyo nduguye mama mmoja, yule 'mtu' ndani yake.
Hiyo yote ni vigumu kufahamu kama si haiwezekani kabisa. Lakini nadharia yetu haizushi matatizo ya aina hiyo. Kwani huyo alikuwa Yesu binadamu asiyekosa, pasipo kuwa na uwili ndani yake, aliyepaza sauti kudhihirisha mshangao na udhia.

## MASHAKA YA YESU

Ningeeleza tena ya kwamba simkatai Yesu bali ninamheshimu sana akiwa Mtume wa Mungu aliyetoa dhabihu maalum. Namwamini Yesu kuwa mja mtakatifu aliyepatwa na jaribio kubwa. Lakini masimulizi ya tukio la Msalaba yanapoanza kufafanuka na yanapoishia, hapo tunakuwa hatuna njia yoyote isipokuwa kuamini ya kwamba Yesu hakujitolea kwa furaha ili afe msalabani. Usiku wa kuamkia siku ambayo maadui zake walijaribu kumwua msalabani twamkuta akiomba usiku kucha pamwe na wanafunzi wake, kwani ukweli wake ulikuwa hatarini. Imesemwa katika Agano la Kale ya kwamba yule mwongo anayemzushia Mungu maneno Asiyomwambia yeye, mwongo huyo atatundikwa mtini na kufa hapo kifo cha laana.

> Lakini nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulinena, au atakayenena katika jina la miungu mingine, nabii yule atakufa. (Kumbukumbu la Torati 18:20).

> Akiwa mtu ametenda dhambi ipasayo kufa, akauawa, nawe ukamtundika juu ya mti; mzoga wake usikae usiku kucha juu ya mti; lazima utamzika siku hiyo hiyo; kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu. (Kumbukumbu la Torati 21:22-23).

Yesu alijua kwamba kama akifa Msalabani, Mayahudi watafurahia kwa shangwe sana kifo chake na kudai yu mlaghai ambaye uwongo wake mwishowe umethibitika pasipo shaka yoyote kulingana na hukumu ya Maandiko Matakatifu. Hiyo ndiyo sababu ya kwamba yeye alikuwa na kiherehere ya kuwa kikombe hicho kichungu kimwepuke; si kwa sababu ya woga, bali kwa kuhofia isije watu wakapotoka na wakashindwa kutambua ukweli wake akifa msalabani. Usiku kucha aliomba kwa huzuni pasipo kujiweza hata kwamba kusoma jinsi alivyoudhika na kusumbuka kunahuzunisha sana mno. Lakini kisa hiki cha kweli kinapokurubia mwisho wake, upeo wa kuudhika kwa maono yake, majonzi yake na ushinde wake, vinaelezeka kikamilifu katika kilio chake cha mwisho: Eloi, Eloi, lama sabakthani? yaani Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? (Mathayo 27:46).

Mtu anapaswa kuzingatia ya kwamba haukuwa udhia tu uliodhihirishwa katika kilio hicho bali huo ulichanganyikana na mshangao uliopakana na hofu kubwa. Baada ya yeye kuzinduliwa na kupata fahamu kwa kusaidiwa na baadhi ya wanafunzi wake halisi waliojitolea kwake ambao walipaka marahamu juu ya majeraha yake ambayo marahamu hiyo walikuwa wameitayarisha mapema kabla ya tukio la msalaba ambamo mlikuwa na dawa za kutuliza maumivu na kuponya jeraha, hakuna budi atakuwa ameshangaa sana akifurahi na imani yake katika Mungu Mpenzi Mkweli ikarejea na kuimarika upya kwa namna ambavyo mtu hakuwahi kushuhudia wingi wake na wasaa wake.

Habari hii ya kwamba marahamu ilikuwa imetayarishwa mapema ndiyo uhakikisho madhubuti wa kuthibitisha ya kwamba wanafunzi wa Yesu walitazamia sana ya kuwa Yesu ataondolewa msalabani akiwa hai akihitaji sana kutibiwa.

Kutokana na maelezo ya hapo juu, inabainika ya kwamba itikadi ya Dhambi ya Asili na kusulubiwa inao msingi juu ya dhana na fikara ya kitamaa waliyozusha baadaye wataalamu wa dini ya Kikristo. Inawezekana sana ya kwamba mawazo hayo yalizalika

kutokana na visa vya kubuniwa vya kabla ya ujaji wa Ukristo, ambavyo visa hivyo vikawashawishi wataalamu hao Wakristo kuona kwamba hivyo vinafanana-fanana na hali alizopata Yesu basi wakabuni itikadi hiyo. Kwa vyovyote, hiyo iwe siri ama jambo linalojipinga lenyewe, tulionavyo, lakini hamna ushuhuda wowote uwao wa kuhakikisha ya kwamba falsafa ya Dhambi na Kafara inalitegemea lolote lililotamkwa na Yesu ama likatendwa au likafundishwa naye. Yeye asingeweza kuhubiri kilicho dhidi ya akili ya mtu na kinachopingana na fahamu ya binadamu.

## JE, MUNGU BABA NAYE ALISUMBUKA?

Tukifikiria asili ya 'Mwana', hatuwezi kuamini kwamba yeye alitupwa motoni, kwani hiyo ingepingana kiundani naye yeye mwenyewe. Tukirejea kwenye imani ya msingi ya Kikristo tunaona ya kwamba Mungu na 'Mwana' ni wawili lakini wenye tabia ya asili ile ile moja. Haiwezekani katu mmojawapo apitie hali fulani pasipo wa pili kushirikiana naye katika hali hiyo. Twawezaje kuamini ya kwamba nafsi moja ya Mungu, yaani, 'Mwana' alisumbuliwa ilhali Mungu Baba akabaki pasipo kuudhika? Kama yeye hakuudhika, basi hiyo itamaanisha kuvunja Umoja wa Mungu. 'Watatu katika Mmoja' inazidi kutokufahamika kwani hali ilizopata kila nafsi mojawapo ya utatu ni tofauti kabisa na mbali mbali hata kwamba inaonekana haiwezekani Nafsi moja ya Mungu iungue katika moto wa Jahanamu ilhali Nafsi zingine mbili zibaki nje zisiguswe katu na moto. Hakuna hiari kwa Wakristo wa leo isipokuwa watengane na imani katika Umoja wa Mungu na waamini miungu watatu, kama wanavyoamini Mapagani wa kabla ya Ukristo kama vile Warumi na Wagiriki, ama wabaki waaminifu na kuamini Mungu ni Mmoja hivi kwamba hali mbili za Mungu haziwezi kupinzana zenyewe kwa zenyewe. Mtoto anaposumbuka, mama hawezi kutulia na kukaa kimya. Lazima yeye naye atasumbuka, bali pengine zaidi kuliko mtoto mwenyewe. Mungu Baba alikuwaje wakati yeye alipomsumbua

'Mwanaye' katika Jahanamu kwa siku tatu? Na nini ilimsibu Mungu Mwana? Je aligawanyika katika wawili wenye hali na asili tofauti? Mmoja akiungua katika Jahanamu na mwingine akiwa nje kabisa asisumbuke asilani. Na kama Mungu Baba alikuwa anasumbuka, basi kulikuwa na haja gani ya kumwumba 'Mwana'? Maana Mungu Baba mwenyewe angeweza kusumbuka. Basi hili ni suala hasa ya kwamba kwa nini Yeye mwenyewe hakuchukua jukumu la kusumbuka? Kwa nini akaunda mpango huo mgumu kwa kutatua tatizo la msamaha?

**ADHABU YA MOTONI:**

Hapa suala la Jahanamu alimotiwa Yesu kulingana na imani ya Kikristo linapaswa kuchunguzwa vizuri zaidi. Jahanamu hiyo ilikuwa ya aina gani? Je, hiyo ilikuwa ile ile Jahanamu iliyoelezwa katika Agano Jipya kama hivi:

> Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. (Mathayo 13:41-42).

Kabla hatujaendelea mbele yatupasa kutambua ya kwamba Agano Jipya linamaanisha nini lisemapo 'adhabu ya moto' ama 'adhabu ya Jahanamu'? Je, huo ni moto unaoounguza roho ama ni moto wa kimwili unaoteketeza mwili na kwa njia hiyo unaitesa roho? Je Wakristo wanaamini kwamba tutarejea kwa mwili huo huo ambao wakati wa kufa roho iliuacha ili kuchanganuka katika vumbi na majivu? Au je, kila roho itaumbiwa mwili mpya na mtu aliyefufuliwa atapata maisha mapya?

Kama huo ni moto wa kimwili na ni adhabu ya kuutesa mwili, basi mtu anaweza kufikiria sana hadi uwezo wake wa kufikiria uishe ya kwamba ilikuwa imetendeka nini kwa Yesu Kristo. Kabla

ya kutupwa Motoni, je, roho yake iliingizwa tena katika mwili wa 'mtu' ilimokaa muda wote katika maisha yake juu ya ardhi, ama ilitiwa kwa njia fulani ndani ya mwili wa kiroho? Kama roho yake ilipewa mwili wa kiroho, hapo mwili huo wa kiroho usingeliweza kufikiwa na moto wa kimwili wa Jahanamu ili kuumiza, kuuadhibu ama kuuangamiza. Na kama tukikubali ya kwamba mwili ule ule wa 'mtu' alimokaa Yesu duniani utaundwa upya kwa ajili ya Yesu ili kwa njia ya mwili huo Yesu apate kuudhika katika Jahanamu, hapo hatuna budi kushuhudia msiba mwingine kwa uadilifu wa Mungu. Mtu maskini kwanza alitiwa nguvuni kwa maisha mazima na roho ngeni, tena kama malipo ya 'ukarimu' wake aliolazimishwa kuonyesha aungue katika Jahanamu pasipo dhambi aliyotenda. Lakini heshima ya kutoa fidia hiyo akajichukulia moja kwa moja huyo mgeni aliyekaa ndani ya huyo mtu. Tena ikoje hali ya roho ya mtu huyo mwenyewe? Pengine alikuwa hana roho yake mwenyewe. Kama ni hivyo, basi hapo mtu katika Yesu na Mungu katika Yesu ndiye yule yule mmoja na kwa hiyo dai la kusema kwamba Yesu wakati mwingine akatenda kibinadamu na pengine ki-mungu litakuwa ni maneno ya kilinge. Kanuni ya pekee inayokubaliwa na akili ni kwamba roho moja na mwili mmoja hufanya mtu mmoja. Roho mbili na mwili mmoja ni wazo la upuuzi linaloweza kukubaliwa na wale tu ambao wanaamini watu kupagawa na pepo na mizuka na kadhalika.

**KUJITOA NA KUFURAHIA KIROHO:**

Kama inakubalika zaidi kwa wataalamu wa dini ya Kikristo ya kwamba roho pekee ya Yesu iliingia Jahanamu na Jahanamu hiyo nayo ilikuwa ya kiroho, basi hapaonekani sababu yoyote ya kuikatalia shauri hiyo kuwa upuuzi. Lakini jahanamu ya kiroho humaanisha kuudhika dhamiri na kuyajutia makosa. Na hayo yote mawili hayalingani na hali ya Yesu. Unapokubali kutozwa kwa

ajili ya uhalifu wa mwingine, wewe mwenyewe ukiwa huna hatia, hapo dhamiri yako haiudhiki bali matokeo ni dhidi yake. Roho ya mtu huyo inapaswa kufurahia kujitoa kwake kwa fikara ya wema na uungwana, jambo ambalo ni kama Pepo ya roho kuliko kuwa kama Jahanamu.

Sasa twageukia suala la mwili alimokaa Yesu na maana ya kifo kulingana na mwili huo na kufufuliwa pia. Tujuavyo sana ni kwamba mwili wa Yesu unalazimika kuwa sehemu isiyoweza kutengwa na Yesu akiwa Mwana wa Mungu. La sivyo, hapatakuwa na nafasi ya uungu wake na ubinadamu wake kuunganika pamoja na kutenda matendo tofauti waziwazi katika hali mbalimbali. Wakati fulani tunamwona mtu akishika hatamu ya mambo sharti akiwa na roho tofauti, na wakati mwingine twashuhudia Mungu akijitokeza na kutawala fikara na maono ya mtu. Twakazania hapo ya kwamba hayo yanaweza kutendeka hapo tu ambapo dhati moja akiingiwa na nafsi mbili mbalimbali.

**MAANA YA KIFO KULINGANA NA YESU:**

Baada ya kwisha kuzingatia vizuri hiari mbalimbali kuhusu matendo aliyotenda 'Mungu' na 'Mtu' ndani ya Yesu, twajaribu sasa kuelewa matumizi ya neno 'kifo' na maana yake kamilifu kumhusu yeye.

Kama yeye alikufa kwa siku tatu, usiku na mchana, basi kifo kitamaanisha roho kutengwa na mwili na kuuaga. Na maana yake ndiyo kwamba roho haina budi kuuaga mwili na kukata kabisa uhusiano wake na mwili hata kwamba mwili usio na roho unabaki nyuma. Mpaka hapo, sawa. Yesu mwishowe akapata faraja kutokana na kifungo chake katika mwili wa udongo wa mtu. Lakini kupata uhuru katika kifungo hicho kusichukuliwe katu kuwa ni adhabu. Marejeo ya roho ya kiungu ya 'Mwana' kwenye hali tukufu ya kuwepo hayawezi kuhesabiwa kwa vyo vyote sawa

na kifo cha kawaida cha binadamu. Kifo cha mtu kinaogofya si kwa sababu roho inatengana na mwili na kukata uhusiano wake nao kwa kupata ufahamu mpya, bali hofu za kifo ni kwa sababu ya mtu kutengwa kwa kudumu na wapenzi wake hapa ardhini na kuacha nyuma mali yake na mambo mengine anayopenda. Mara nyingi twaona mtu ambaye hana kitu cha kuishia anapendelea kufa badala ya kuishi maisha matupu.

Yesu asingeweza kujuta na kuhuzunika wakati wa kufa, kwani kifo kilimfungulia njia moja tu ya kupata faida siyo hasara. Kwa nini kuugua mwili kuhesabiwe kuwa jambo la kuhuzunisha na kusumbua? Tena kama yeye alikufa hasa mara moja, siyo kimfano, na kukata roho, wanavyotaka Wakristo kwamba tuamini, hapo kurejea tena katika mwili huo ni hatua isiyo na busara kabisa inayonasibishwa kwake. Je, alizaliwa upya aliporejea katika mwili aliouacha pindi alipokufa? Na kama kurejea kwake katika mwili huo kwamaanisha kwamba alihuika au kufufuka, hapo hata mwili huo ungekuwa wa kukaa milele. Lakini tunayosoma katika Biblia ni kisa kingine tofauti kabisa. Sawa na kisa hicho Yesu alifufuliwa kwa kuingia katika mwili huo huo uliokuwa umesulubishwa na hiyo ikaitwa kuhuika. Kama ni hivi, kuuacha kwake mwili mara nyingine kutamaanisha nini? Je, hiyo itakuwa ni sawa na mauti ya pili?

Kama kuuaga mwili mara ya kwanza ndiyo kifo, basi hakuna budi alipouacha mwili mara ya pili atangazwe alikufa kwa kudumu. Roho inapouacha mwili mara ya kwanza, mwaita kifo, na roho inaporejea katika mwili huo, mwasema kuhuika baada ya kufa. Lakini mtaisemaje ikiwa roho inauacha mwili huo mara nyingine pasipo kuurejea abadan? Je, hiyo itaiwa kifo cha milele ama uhai wa milele kwa kulingana na istilahi ngumu za Kikristo? Haikosi hiyo ndiyo kifo cha milele wala haina maana nyingine. Kujipinga juu ya kujipinga. Ni jambo la kuchosha na kuhuzunisha kweli!

Kama ifikiriwe kwamba mwili haukuachwa mara ya pili, hapo tutakabili hali ya ajabu ambamo Mungu Baba huwepo akiwa nafsi

isiyo na mwili, isiyo na mipaka ilhali 'Mwana' hudumu kunaswa katika eneo fupi lenye kukabili mauti.

**ADHABU YA KIASI KWA DHAMBI ISIYO YA KIASI :**
Yaweza kusemwa ya kwamba siyo kila mara maumivu ya dhamiri ndiyo yanayosababisha kusumbuka roho na moyo kwa wale wasioweza kuvumilia makosa yao. Bali huruma nyingi kwa kuona taabu za wengine pia yaweza kumwudhi mtu ambaye hana dhambi kabisa ama hana dhambi sana, lakini anayo tabia njema ya kusumbuka kwa kuona mateso ya wengine. Hali hiyo nayo itazalisha namna ya jahanamu kimfano. Kina mama wazazi husumbuka kwa ajili ya watoto wao wanaougua. Imeshuhudiwa ya kwamba wakati mwingine maisha mazima ya mama hugeuka kuwa jahanamu kwa ajili ya mwanaye aliyelemaa kwa kudumu. Kwa nini basi tusikubali sifa hiyo njema kupatikana ndani ya Yesu iliyomfanya asumbuke kwa ajili ya wengine? Bila shaka twapaswa kukubali. Lakini kwa nini kwa siku tatu, usiku na mchana pekee? Kwa nini si kwa muda wote wa kukaa ardhini bali na hata kabla yake na baadaye pia? Waungwana hawasumbuki kwa muda mfupi sana wa saa ama siku chache. Nyoyo zao hazitulii hadi waone kwamba shida zimetulia ama zimeondolewa kabisa. Ile jahanamu tunayozungumzia haimhusu tu mzungupule asiye na dhambi, bali hata wanyama wa mwituni nao wanashirikiana katika sifa hiyo njema na wanasumbuka kwa ajili ya wanyama wenzao.

Nikiisha sema maneno machache nitaiacha habari hiyo kushughulikia, lakini ninalo jambo moja la muhimu nitakaloligusia kidogo. Adhabu aliyohukumiwa Yesu kupata ilidumu kwa siku tatu tu, mchana na usiku, ilhali wale wenye dhambi ambao yeye alisumbuka kwa ajili yao walitenda dhambi chafu sana tena kwa muda mrefu kabisa na kulingana na Biblia

adhabu yao ilikuwa kuungua katika jahanamu milele. Mwadilifu gani huyo Mungu ambaye alitaka kuwaadhibu viumbe wake wasiokuwa wana wake na mabinti zake kwa adhabu ya kudumu milele? Lakini alipotakiwa kumwadhibu mwanaye mwenyewe kwa ajili ya dhambi alizojitolea kwa hiari yake kuadhibiwa, mara adhabu ikapunguzwa. Ikawa siku tatu tu, usiku na mchana.
Adhabu hizo mbili hazilingani, hazifanani hata kidogo. Kama huo ndio uadilifu, afadhali usiwepo tena. Mungu ataonaje mwenendo wa wanadamu aliowaumba kwa mkono wake wa kuume wakifanya uadilifu walivyojifunza kutoka kwake Yeye wakitumia vipimo mbalimbali kwa watoto wao wenyewe na watoto wa watu wengine? Je, Mungu Baba ataangalia mwigo huo mwaminifu kwa furaha kuu na hofu kubwa? Hakika ni vigumu mno kujibu swali hilo.

**KAFARA ILILETA BADILIKO GANI?**

Kuhusu matokeo ya Yesu Kristo kusulibishwa tumekwisha hakikisha ya kwamba imani katika Yesu haikupunguza adhabu ya dhambi kwa namna yoyote iliyotolewa na Mungu kwa Adamu na Hawa na wazao wao. Wanawake wote bado wanazaa kwa uchungu na wanaume bado wanachuma riziki yao kwa jasho la uso wao. Twaweza kuliangalia jambo hilo kwa jiha nyingine, kwa kulinganisha ulimwengu wa Kikristo na ulimwengu wa wasiokuwa Wakristo kuanzia zama za Yesu Kristo. Katika kipindi chochote cha historia waumini wa Kikristo hawawezi kuonesha badiliko lolote maalum kwa wanawake wao kwamba wanazaa bila uchungu, wala kwa wanaume wao kwamba wanachuma riziki yao bila kutokwa jasho. Hawawezi kuonesha tofauti yoyote iwayo baina ya Wakristo na Wasiokuwa Wakristo.

Kuhusu maelekeo ya kutenda dhambi twashuhudia ya kwamba hayo hayakufutika kabisa baina ya waumini wa Kristo kwa athari ya kafara ya Yesu. Aidha, mtu anashangaa kweli kwa nini imani katika Mungu imehesabiwa kuwa hafifu kuliko imani katika 'Mwanawe'. Hiyo inahusika hasa na zama kabla haijatobolewa siri hii kubwa ya kwamba Mungu anaye Mwana. Naam, walikuwapo watu zamani waliokuwa na imani katika Mungu na Umoja wake. Vilevile watu wengi wasiohesabika walizaliwa tangu wakati wa Yesu katika dini mbalimbali na nchi mbalimbali hapa ardhini waliomwamini Mungu na Umoja wake. Mbona imani katika Mungu haikuathiri dhambi za wanadamu na adhabu zao? Tena kwa nini Mungu Baba hakudhihirisha wema wake na kusumbuka kwa ajili ya wenye dhambi ambao wema huo ukaoneshwa na 'Mwana' aliyekuwa na daraja dogo kuliko Baba? Kwa yakini 'Mwana' anaonekana anayo khulka bora zaidi (Mungu apishe mbali) kuliko Baba asiye mstaarabu sana. Je, Uungu unakua na bado unaendelea kukua ili kufikia ukamilifu wake, mtu aweza kuuliza?

## 3 KAZI YA ROHO MTAKATIFU

Mpaka sasa tumezungumzia suala la Yesu, anayefanywa kuwa Mwana, na suala la Mungu anayedhaniwa kuwa Baba halisi wa Yesu. Lakini bado kuna nafsi ya tatu, jina lake Roho Mtakatifu, ambaye japo anayo dhati tofauti peke yake lakini ameunganika kikamilifu daima na 'Baba' na 'Mwana' hata kwamba muungano wa hao watatu umezalisha umoja katika utatu. Sasa twageukia kuchunguza ya kwamba je, Roho Mtakatifu anajitambua kuwepo kwake mbali na Mungu au Yesu, ama wote watatu wanashirikiana katika kujitambua kuwepo kwao kwa pamoja? Kujitambua kuwepo ama kujijua kuwepo kwa mtu kunamaanisha kuelewa kwamba mtu anakuwepo peke yake pasipo kuwa sehemu ya mwingine. Utambuzi huo wa mtu kwamba anayo dhati yake binafsi mbali na dhati za wengine unazalisha 'mimi' na 'yangu' na 'ya kwangu', na 'wewe'na 'yako'.

Tukichunguza sehemu tatu za Mungu twalazimika kuamua kwamba je, kila mmoja anajitambua kuwepo kwake mbali na kuwepo kwa wengine wawili ama hapana. Kama kila mmoja wao hana utambuzi wa kuwapo kwake mbali na utambuzi wa wengine kuhusu kuwapo kwao, hapo kunasibisha kwao dhati mbalimbali hakutafahamika. Kila mmojawapo hata akimkurubia mwenzake sana namna gani hana budi kujijua kwamba anakuwapo peke yake na anayo dhati yake mbali na wengine.

Itikadi rasmi ya makanisa mengi iko wazi sana na imefafanuliwa vizuri nayo ni kwamba kila nafsi katika nafsi tatu za Mungu ni dhati halisi tofauti na nyingine mbili. Kwahiyo hapa hatuna 'Tatu katika moja' bali 'Watatu katika Mmoja'. Uchungu aliopata Yesu

alipoyakabili mauti na matokeo yake ya hatari haikosi Roho Mtakatifu pia alishirikiana katika hayo yote kwa usawa pamwe na Yesu. Na vilevile hakuna budi yeye naye akashirikiana na Yesu katika kujitolea. Aidha lazima akasumbuka pia katika jahanamu pamoja na Yesu na Mungu Baba. Kama hapana, hapo mtu hana budi kuamua ya kwamba hao watatu siyo kwamba ni watatu mbali mbali tu bali hata maono yao, fikara zao na kadhalika, pia ni mbalimbali.

Tukijaribu kupata mwanga zaidi juu ya utatu, twapaswa kutambua uhakika wa watatu kuunganika pamoja ama kuwapo kwa hao watatu kama mmoja tu kwa sababu ya hao kufungamana pamoja kwa kudumu milele. Mpaka sasa tumeshidwa kufahamu jinsi ya kufungamana kwao katika maono na mawazo.

Kilichobaki ni kufahamu ya kwamba waliunganika pamoja katika mwili tu mmoja. Hiyo yatukumbusha habari ya yule joka kuu aliyetajwa katika hadithi za kubuniwa za Kigiriki, ambaye alikuwa na vichwa vingi ambavyo vikikatwa vinaota tena. Ni sawa mtu hawezi kutambua hasa alivyo Mungu na jinsi sifa zake zinavyofanya kazi humo ndani, lakini ni rahisi sana kuamini katika dhati pamoja pasipo sehemu zake mbalimbali kama vile kichwa, moyo na figo na kadhalika. Lakini habari ya mawazo na maono maalum ya mmoja inahitilafiana kulingana na hali iliyoelezwa juu ya dhati moja. Hiyo inatoa picha ya Mungu isiyoweza kuaminiwa na kufahamika kwa binadamu ambao wengi wao waliishi muda mrefu wakiamini itikadi hiyo ya Kikristo bila ya kuipinga na wakafumba macho yao wasiangalie yanayoipinga akili ya mtu ambayo iliumbwa na Mungu Mwenyewe.

## USHIRIKIANO WA ROHO MTAKATIFU KATIKA UUMBAJI:

Hatuoni kazi yoyote iliyoshughulikiwa na Roho mtakatifu au Yesu Kristo katika mpango wa uumbaji:

Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. (Mwanzo 1:1)

Hakuna shaka kwamba katika Agano la Kale Mungu Baba ndiye ametajwa aliyeumba mbingu na nchi pasipo hata kudokeza habari ya Kristo ama Roho mtakatifu. Zama zote za kabla ya Ukristo, miongoni mwa Mayahudi ,walioliamini Agano la Kale na bila shaka waliwahi kusikia mstari huo hapo juu mara malaki kwa malaki, hakuna hata mmoja aliyeweza kulisoma jina la Kristo au la Roho Mtakatifu katika kisa cha uumbaji wa ulimwengu. Katika Injili ya Yohana Mtakatifu 'Neno' limetumika kwa ajili ya Yesu. Ni la ajabu ya kwamba habari ya muhimu kabisa imezungumzwa na Injili moja peke yake; tena na yule ambaye hata hakuwa mwanafunzi wa Yesu.[1] Hata mtu akikubali usemi wake kuwa neno la Mungu, hata hivyo huo utamaanisha kuwa Takwa la Mungu; hilo ni wazo linalopatikana katika dini nyingine vile vile katika habari ya uumbaji.

Ni mshangao mkubwa ya kwamba siri ya zamani sana ya Kristo na Roho Mtakatifu kushirikiana pamoja katika uumbaji ikabaki kuwa siri hata kwa Yesu mwenyewe. Hatusomi hata mara moja ya kwamba Yesu Kristo alidai kuwa Neno. Hivyo, Yesu wala Roho Mtakatifu hawakuwa na sehemu yoyote ya kazi ya kufanya katika uumbaji. Tena twaambiwa ya kwamba alikuwa ni Mungu Baba peke yake aliyemfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi kwa mikono yake mwenyewe. Sijasoma kabisa katika maandiko yoyote ya Kikristo ya kwamba mikono hiyo miwili ilikuwa ya Yesu na Roho Mtakatifu. Basi Mungu aliumba vitu vyote pasipo kusaidiwa hata kidogo ama kushirikiana na Yesu ama Roho Mtakatifu. Je, hao walikaa tu na kuangalia wakikubaliana kwa jumla na aliyokuwa anafanya Mungu ama walishirikiana naye hasa? Kama wataalamu wa Kikristo wanapendelea kukubali ya

---

[1] Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. (Yohana 1:1).

kwamba hao wawili nao walishirikiana katika uumbaji, basi haraka swali litazuka ya kwamba je, kila mmoja kati yao alikuwa na uwezo wa kuumba bila kusaidiwa na wengine, ama walikuwa na uwezo huo wakiwa pamoja?

Isitoshe, kama wote watatu walihitajika kutoa mchango wao kwa kuumba, hapo je, wote wakatoa mchango kwa usawa ama mmoja wao akalazimika kutoa sehemu kubwa zaidi katika mpango wa uumbaji? Je, kila mmoja katika hao watatu alikuwa na namna na kiasi cha uwezo tofauti ama uwezo wa kila mmoja ulikuwa sawa na uwezo wa mwenzake?

Mtu hata akikiri hii au ile analazimika kukubali ya kwamba kila mmoja katika Utatu hana uwezo wa kuumba chochote peke yake. Kama hoja hiyo itumiwe kwa kazi nyinginezo za Mungu, swali hilo hilo litawasumbua wataalamu wa Kikristo. Na mwishowe Wakristo watalazimika kukiri ya kwamba wao hawaamini dhati moja ya Mungu mwenye jiha na sura tatu za nguvu kuu na utukufu. Bali wanaamini sehemu tatu za Uungu zilizo mikato mitatu ya mwili wa Mungu. Hapo swala la sehemu zote kuwa sawa ama si sawa halitakuwa na uzito zaidi.

Kwa mfano, chukueni sifa ya uadilifu na msamaha. 'Mwana' anaonekana kuwa na huruma zaidi ilhali Mungu Baba anaonekana Mwadilifu kidogo kuliko Roho Mtakatifu ambaye hakushirikiana na Mungu Baba katika dhuluma yake.

Uwezekano wa pili tuliozungumzia ulikuwa kwamba pengine Yesu na roho Mtakatifu walikaa tu pasipo kushirikiana kwa kitendo katika shughuli za uumbaji na kuendesha kanuni za ulimwengu. Kama ni hivi, hapo yatazuka maswali mengi mengine. Kwanza kabisa, hao washiriki wawili wa Mungu walipewa kazi gani katika kutekeleza wajibu wao wa Kiungu? Kama hao ndio washiriki wa kukaa tu kimya kama washiriki katika biashara wanaokaa tu pasipo kushughulikia kazi kwa kitendo, hapo wamekwisha punguziwa hadhi yao na kupewa daraja la pili ambako wanakuwapo pamoja na Mungu lakini bila ya kushirikiana naye hususan katika madaraka yake. Wazo hili la

Mungu kuwa na nyongeza mbili zisizo na kazi ni jambo la kutatanisha kusema kwa uchache. Nashangaa, wazo hilo linaweza kuwatuliza kina nani. Hiyo haiwezi kukubaliwa kiakili wala haiafikiani na imani ya Kikristo ya 'Watatu katika Mmoja' na 'Mmoja katika Watatu'. Watatu hawawezi kuwa na Umoja wala haiwezekani kuwaza umoja huo pasipo hao watatu kuunganika kikamilifu katika nia, madaraka na mengine yote yanayoweza kudhaniwa katika maisha ya mmoja.

Ama Roho Mtakatifu akiwa dhati peke yake, asipofungamana kikamilifu kwa kudumu na wengine wawili akitengana na nafsi yake, hakuna tumaini kujitokeza kwa Mungu mwenye vichwa vingi akiwa na fikara moja nia moja na mwili mmoja.

**SIRI AMA HITILAFU:**

Inakubaliwa ya kwamba mtu aliamini jambo asilolifahamu kikamilifu kwa sababu kuna ushuhuda usioweza kukataliwa kulihakikisha hilo. Kwa mfano, wapo watu wengi wasioelewa namna zinavyofanya kazi radio na televisheni kwa kutuletea sauti na picha kutoka mbali sana, lakini hata yule mtu asiyejua kabisa kusoma na kuandika anaamini katika uhakika wa kuwepo kwa radio na televisheni. Kadhalika wengi kati yetu hawajui namna kompyuta zinavyofanya kazi, hata hivyo hakuna atakayekataa kupatikana kwa kompyuta kwa sababu hiyo tu. Mambo hayo yanaweza kuhesabiwa katika fungu la 'siri', lakini hakuna swala la kuyakatalia kuwapo kwa hayo ama kuwadhihaki wanaoyaamini hayo sharti yanahakikishwa na ushahidi usioweza kukatalika.

Pia tunakubali kulegeza kamba na kuamini siri nyingi zinazohusikana na itikadi za kidini. Watu wengi sana wanaamini itikadi kama hizo bila kuweza kufahamu ama kuweza kuzieleza. Wanaonekana wamerithi imani hizo kizazi hata kizazi na kuzichukua kuwa ni sawa hasa. Lakini mambo yanayojipinga na

kuhitilafiana yanapojiingiza katika itikadi za kidini, hapo udhuru wowote haukubaliwi kuziamini eti kwa sababu siri za kushangaza zinakubaliwa basi na hayo yanayojipinga na kuhitilafiana pia nayo yakubaliwe. Hapo ndipo swala linaleta matatizo. Naweza kuliamini nisilolifahamu, lakini siwezi kulikubali linalojipinga lenyewe wala sitoamini kwamba mtu yeyote mwenye fahamu aweza kuliamini. Kwa mfano, sijui namna inavyotengenezwa saa. Mpaka hapo ni sawa. Lakini sina haki ya kuamini papo hapo kwamba saa ni mbwa anayelia na kupiga mateke. Maana hiyo haitakuwa fumbo bali ni jambo linalojipinga lenyewe.

Pindi unapokuwa upingamizi baina ya sifa mbili au zaidi za Mungu, ama maneno ya Mungu na matendo ya Mungu yanapopinzana, hapo mipaka ya siri huwa imekwisha rukwa tayari sana na mtu anaondoka katika eneo la siri akaingia katika ulimwengu wa mawazo yasiyo na msingi. Ikithibitika hivyo, hapo waaminio katika yanayojipinga wanapaswa kurekebisha itikadi zao na hatimaye kunyoosha imani yao. Lakini ni bahati mbaya ya kwamba katika maongezi yetu twawakuta mapadre kushikamana na maoni ya kwamba hamna upingamizi katika kumwamini Yesu kuwa Mingu na binadamu wakati ule ule mmoja. Pia hawaoni hitilafu yoyote katika hili ya kwamba mtu mmoja anaweza kuwa watu watatu pasipo kutokea tofauti yoyote katika mwenendo wao. Wanakazania ya kwamba ni fumbo tu wala hamna hitilafu katika kumwamini Mungu mmoja na papo hapo kuamini Mungu mwenye jiha tatu aliyefanyika na Mungu, Roho Mtakatifu na 'Mwana' wanafumba macho yao wasione hitilafu katika dai lao ya kwamba Mungu anakuwa dhati moja tu ingawaje ni hakika ya kwamba Mungu Baba ni tofauti kabisa na Yesu,-'Mwana' na Roho Mtakatifu. Tunapowaashiria katika mshangao wetu ya kwamba twazungumzia watatu wala siyo jiha, hali na sifa za mmoja, na kwamba Mungu akiwa 'Mmoja katika Watatu' na 'Watatu katika Mmoja' siyo fumbo bali ni hitilafu, wanatikisa kichwa kutuhurumia na kutuambia kwa upole tuingie tu katika hitilafu zinazoonekana katika majadiliano yetu.

Wanatutaka tuamini kwanza lisiloaminika na kisha kuanza kuendelea mbele kutoka hapo kuzoea kuyaamini yanayopinzana, ama yaliyo mafumbo kama wapendavyo kuyaita. Hivyo, asiye Mkristo hawezi

kutambua hitilafu za itikadi za Kikristo, na ili kufahamu asiloweza kuliamini yeye analazimika kuamini bila kulielewa. Huo ndiyo ulimwengu wa mawazo yasiyo na msingi tunamosihiwa kuingia sisi tusio Wakristo. Lakini zulia hilo la ki-uchawi lirukalo linakataa kuruka ikiwa analipanda asiye mwaminio.

# 4 KUSULUBIWA

Kabla sijaeleza matukio kuhusu Yesu na kusulibiwa kwake jinsi yalivyoelezwa ndani ya Biblia, ningeonelea kufafanua kwa kifupi tunavyoelewa sisi Waislamu Waahmadiyya yale yaliyotendeka wakati Yesu alipotundikwa msalabani na baadaye pia. Nitaigusia tu kidogo habari hii hapa kwa kifupi, maelezo zaidi yatafuata baadaye.

Tunaamini ya kwamba kumwamba Yesu msalabani kulikwa ni jaribio la kumwua yeye jinsi ya kujaribu kumwua mtu yeyote mwingine. Kumwamba msalabani ilikuwa ni njia tu ya kutaka kumwua. Lakini jaribio hilo la kumwua msalabani lilishindwa. Tusemapo hayo, twamaanisha kabisa jinsi tutakavyosema kuhusu jaribio la kumwua mtu yeyote mwingine. Kama mtu fulani anafanyiwa njama ili akauawe, lakini jaribio hilo linashindwa, huwezi kusema kwamba aliyefanyiwa njama amekwisha uawa tayari. Kwa mfano, kama mtu fulani ameshambuliwa kwa upanga lakini jaribio hilo likashindwa, hapo hutaweza kusema kwamba mtu huyo ameuawa na upanga. Basi sisi Waislam Waahmadiyya tunaamini ya kwamba Yesu alifanyiwa njama ili auawe, msalaba ukawa njia tu ya kujaribu kumwua. Baada ya saa chache za taabu kubwa sana juu ya msalaba, kabla hajafa, akaondolewa kutoka msalabani katika hali ya kuzimia sana ambako katika hali hiyo yeye akapona na kupata fahamu tena. Kwa kuwa serikali yoyote haiwezi kumpa ulinzi mtu aliyehukumiwa kuuawa lakini akapona kwa njia hii au ile, na ndivyo ilivyokuwa pia katika sheria ya Kirumi, kwahiyo Yesu asingeweza kuachiliwa baada ya kupona

msalabani. Basi hiyo ilikuwa ni sababu ya kutosha sana kwa Yesu kuukimbia utawala wa Kirumi na kuikimbilia nchi ya usalama na uhuru. Lakini yeye pia alitakiwa kutimiza wajibu wake fulani na kutimiza utabiri mmoja. Kulikuwa na kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea, ambao baada ya kuvamiwa na Wababiloni na Warumi wakatoka nyumbani mwao na kutawanyika katika nchi nyingi za mashariki. Hao walikuwa wanamngojea yeye. Na hiyo ilikuwa sababu nyingine madhubuti kwa Yesu kuihama Uyahudi na kuzikimbilia nchi nyingine ambako walikaa Wayahudi kwa karne nyingi. Kwa wakati huu kiasi hicho kinatosha kuelezwa.

Ningependa kuwabainishia wale wanaotudaia uhakikisho wa Yesu kufa ajali baada ya kupona juu ya msalaba, hao wanatusukumia mzigo wao pasipo sababu yoyote. Zipo kanuni za ulimwengu zijulikanazo kwa watu na zinaeleweka kikawaida. Tunajua ya kwamba umri wa mtu juu ya ardhi hauzidi miaka mia na hamsini hivi; kwa vyovyote hauwi miaka elfu au zaidi. Ndivyo tunavyoshuhudia kwa jumla kuhusu muda wa mtu kuishi juu ya uso wa ardhi. Kama kuna mtu anayedhania kuwa kinyume cha kanuni hiyo kimetendeka, hapo itakuwa wajibu wake kuhakikisha tofauti hiyo iliyotendeka, wala katu si faradhi ya mwenzake anayeamini katika kanuni ya kawaida ilivyo ahakikishe ya kwamba haikutendeka kinyume chake. Hoja hiyo inapaswa kutumiwa kuhusu habari ya uhai na mauti ya Yesu Kristo. Wale wanaoamini ya kwamba yeye hakufa hawana budi kuleta uhakikisho wa madai yao. Lakini wanaodai ya kwamba yeye lazima amekwisha kufa wanafuata tu kanuni za kawaida za ulimwengu, wala haina maana kuwadaia uhakikisho wa habari hiyo. La sivyo, mtu yeyote anaweza kudai ya kwamba babu wa babu wa babu.... yake hajafa bado, na kama mtu anakataa habari hiyo alete hoja ya kuhakikisha kwamba mzee huyo kweli amekufa. Watu watamfikiriaje huyo mtu? Maana mtu anawezaje kuleta uhakikisho ya kwamba mzee wa zamani sana aliyeishi miaka mamia amekwisha kufa. Uhakikisho wenyewe ni kanuni yenyewe ya kawaida ambayo inahusikana na kila mtu. Basi kama mtu fulani

anadai kinyume chake, mtu huyo analazimika kuthibitisha madai yake hayo. Hilo ni jibu la kwanza, lakini nitajaribu kubainisha habari hiyo kwa jiha nyingine.

Pasipo kujali uhusiano wake na Mungu, je, ilikuwa kinyume kabisa Yesu Kristo kufa? Wakristo wenyewe wanakubali ya kwamba alikufa. Kama kufa ilikuwa kinyume cha tabia yake, hapo asingelikufa hata kidogo. Hata hivyo sote twakiri kwamba kwa akali alikufa mara moja. Kilichobaki ni kuchunguza alikufa lini. Je, alikufa msalabani ama baadaye wakati mwingine?

## ISHARA YA YONA:

Twaweza kuhakikisha kutoka katika Biblia ya kwamba Mungu hakumwacha na akamlinda asife kifo cha laana juu ya msalaba. Habari hiyo inaweza kuchunguzwa kwa kutalii mambo kadha yaliyotukia kabla ya tukio la msalaba, na yaliyotukia alipokuwa juu ya msalaba na yale yaliyotukia baada ya tukio la msalaba, jinsi yalivyoelezwa katika Agano Jipya.

Muda mrefu kabla ya tukio la msalaba, Yesu aliahidi ya kwamba watu hawataonyeshwa ishara yo yote isipokuwa ishara ya Nabii Yona. Hebu someni:

> Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakisema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako. Akajibu, akawaambia: Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa ishara, ila ishara ya Nabii Yona. Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi. Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona. (Mathayo 12: 38-41).

Kwahiyo kabla hatujahakikisha yaliyotendeka kwa Yesu twalazimika kuelewa yaliyotendeka kwa Yona, kwani Yesu alidai ya kwamba mwujiza huo huo utarudiwa. Ilikuwa nini Ishara ya Yona? Je, alikufa tumboni mwa nyangumi na kisha akafufuka baadaye? Wakristo, Wayahudi na Waislamu wote kwa neno zima wanakubali ya kwamba Yona hakufa tumboni mwa nyangumi.Yeye alikaa katika hali ya hatari baina ya kufa na kupona na akaokolewa kimwujiza katika hali hiyo, ilhali mtu yeyote mwingine angekufa katika hali kama hiyo. Hata hivyo baadhi ya kanuni zisizoelezeka kwa urahisi zilifanya kazi chini ya amri ya Mungu ili kumwokoa katika mauti. Kumbukeni hatuzungumzii habari hii ya kwamba jambo hilo linawezekana ama hapana. Tunaloashiria ni kwamba Yesu aliposema ya kwamba yatatendeka kwake mfano wa yale yaliyotendeka kwa Yona, alimaanisha ya kwamba yaliyotendeka kwa Yona yatatendeka kwake yeye pia. Katika ulimwengu mzima wa Wayahudi wakiwa katika Uyahudi ama popote walipo Wayahudi duniani walipokaa baada ya kutawanyika, hamna hata Myahudi mmoja aliyefahamu maana tofauti ya usemi huo wa Yesu. Wote hao waliamini ya kwamba Yona kimwujiza ama kwa njia nyingine alipona katika hatari kwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi wala hakufia humo hata kwa dakika moja. Naam, sisi tunahitilafiana kidogo kuhusu habari hiyo. Kisa cha Yona kilivyoelezwa katika Kurani hakielezi popote ule muda wa siku tatu mchana na usiku aliokaa Yona katika tumbo la nyangumi. Lakini twaiachia habari hiyo hapa, bali twarejea tuliyokuwa twazungumzia na twajaribu kufafanua mambo yanayofanana katika visa vya Yona na Yesu jinsi alivyotabiri Yesu. Yafananayo ni kupona katika hatari kubwa kabisa kwa muda wa siku tatu mchana na usiku, wala siyo kufufuka baada ya kwisha kufa. Yesu anadai ya kwamba yatatendeka kwake hayo hayo.

**AHADI YA YESU KWA NYUMBA YA ISRAELI:**
Ushuhuda muhimu wa pili ni kwamba Yesu aliwaambia watu wake ya kwamba kondoo wa nyumba ya Israeli wanaoishi katika Uyahudi na pembeni mwake siyo tu kondoo ambao yeye alitumwa kwao, bali kuna kondoo wengine pia ambao si wa zizi hili ambao ninapaswa kuwaleta pia:

> Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja. (Yohana 10:16)

Sasa, tujuavyo ni kwamba katika muda ulio baina ya yeye kutoa ahadi hiyo na kutundikwa msalabani, yeye hakuondoka Uyahudi kuelekea mahali pengine. Hapa lazuka swali: Kama Yesu alipaa mbinguni, je, na kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea nao walipaa mbinguni mapema zaidi? Wakristo wanaamini ya kwamba baada ya Yesu kuteremshwa kutoka msalabani akiwa mfu akafufuka baada ya siku tatu hivi na kisha akaonekana akipaa katika mawingu na kupotea katika sehemu za ndani za mbinguni na kufikia Kiti cha Enzi cha Baba yake na kuketi upande wake wa kuume daima. Kama hiyo ndiyo sawa, basi tunalikubali tatizo kubwa kabisa kweli. Tutalazimika kuchagua jambo mojawapo katika mawili: Moja lililoshikwa na Yesu mwenyewe na jingine na wafuasi wake. Na hayo mawili yanapinzana kiasi hiki kwamba kila moja linalifutilia mbali jingine. Kama Yesu alikuwa sawa, na twaamini alikuwa sawa, basi kabla hajapaa mbinguni alitakiwa kukumbuka ahadi yake na kumwomba Mungu Baba muhula wa kukaa zaidi hapa ardhini ili aende kwa nchi zile ambako makabila mengi ya Israeli yalikuwa yamehamia na kukaa huko. Yeye asingalipaa mbinguni pasipo kuvunja ahadi yake na uaminifu wake, akitia dosari na kujiharibia picha yake ya kuwa mungu mkamilifu, mtu mkamilifu. Na kama, kinyume chake tukikubali wataalamu wa Kikristo kuwa sawa, na inakubaliwa ya kwamba Yesu kwa hakika alisahau wajibu wake kuhusu nyumba ya Israeli

na akaenda mbinguni moja kwa moja, hapo basi tutakubali shingo upande kwamba watalaamu wa Kikristo wako sawa, lakini ole wenu, Ukristo unathibitika kuwa wa uwongo.
Kwani, kama Yesu akithibitika kuwa mwongo, basi Ukristo hauwezi kuwa wa kweli.
Sisi twakubali ya kwamba Yesu alikuwa Nabii mkweli wa Mungu wala asingeweza kufanya ahadi ya uwongo. Alichomaanisha kwa kauli yake ya kondoo waliopotea ni makabila kumi ya Israel ambayo mapema yaliihama Uyahudi na kutawanyika huko katika nchi za mashariki. Basi ahadi yake ilikuwa kwamba yeye hatauawa msalabani bali atajaaliwa umri mrefu ili kuufuatia wajibu wake na kwamba yeye hakuwa nabii kwa makabila mawili tu yaliyoishi pembeni mwake, bali kwa ajili ya Waisraeli wote popote walipo. Shuhuda mbili za hapo juu zikiwa pamoja zinaashiria moja kwa moja nini kilitakiwa kutendeka kwa Yesu baada ya tukio la Msalaba.

**MAMBO YAHUSUYO TUKIO LA MSALABA:**
Jambo jingine linalolingana na habari hiyo ni ule wakati maalum na tarehe iliyowekwa na Pilato kwa kuwambwa Msalabani. Hata kabla hajaweka tarehe na wakati twasoma habari za baadhi ya mambo ambayo mtu asiwe na shaka ya kwamba yaliathiri uamuzi wa mwisho. Kwanza kabisa twajua kutokana na Agano Jipya ya kwamba mkewe Pilato hakupendezwa asilani na Pilato kumhukumu Yesu kwa sababu ya kuathirika na ndoto aliyoiota usiku wa kuamkia siku ya kusikilizwa kesi ya Yesu.
Mama huyo alitishika sana na ndoto hiyo iliyomtia imani ya kwamba Yesu hana kosa hata kwamba akaonelea kuingilia kusikilizwa kwa kesi na kumpelekea mumewe ujumbe wa ndoto yake (Mathayo 27:19). Labda ilikuwa ni utetezi huo wa mkewe uliomfanya Pilato ajitenge na kumhukumu Yesu:

> Basi Pilato alipoona ya kuwa hafai lolote, bali ghasia inazidi tu, akatwaa maji, akanawa mikono yake mbele ya mkutano, akasema, Mimi sina hatia katika damu ya mtu huyu mwenye haki; yaangalieni haya ninyi wenyewe. (Mathayo 27:24).

Hiyo inamaanisha ya kwamba yeye alikiri ya kuwa Yesu alikuwa hana kosa na kwamba hukumu kali aliyotoa ilikuwa kwa sababu yeye alishurutishwa. Ni wazi kabisa kutokana na Agano Jipya ya kwamba jamii ya Kiyahudi iliunganika pamoja dhidi ya Yesu ikanuia kabisa kwamba Yesu lazima apate kuadhibiwa. Hivyo, hukumu yoyote kinyume cha matakwa ya Wayahudi ingeweza kuchafua amani nchini. Hali hiyo ndiyo ilimbana asiweze kitu na akadhihirisha kulazimika kwake kwa njia ya kitendo chake cha kunawa mikono yake.

Pilato alifanya jaribio jingine tena ili kumwokoa Yesu. Yeye akawapa hiari makutano hao wenye hasira kumwokoa mmojawapo kati ya Yesu au Barabbas, mhalifu mashuhuri. Na hiyo ndiyo dalili kubwa ya kuonesha hali ya moyo wa Pilato katika wakati huo. Ni dhahiri shahiri kwamba yeye hakuwa na wazo la kumhukumu Yesu. Katika hali hiyo ya kisaikolojia yeye aliweka kusulibiwa kwake siku ya Ijumaa saa za jioni. Hiyo inadokeza uwazi kwa ya kwamba yeye alifanya kusudi, kwani Sabato haikuwa mbali kutoka jioni ya Ijumaa, na Pilato akiwa msimamizi wa sheria alitambua habari hii zaidi kuliko mtu yeyote mwingine ya kwamba kabla halijatua jua mwili wa Yesu unatakiwa kuondolewa kutoka msalabani. Na ndivyo kabisa ilivyotendeka. Kwa kawaida muda wa siku tatu mchana na usiku ulitakiwa kumwua mtu kwa kuteseka sana juu ya Msalaba, lakini Yesu akakaa saa chache tu juu ya Msalaba. Mtu hana budi kushangaa ya kwamba mtu kama Yesu ambaye maisha magumu yalikuwa yamemfanya kuwa mgumu kafa kweli katika muda huo mfupi.

Je, huo siyo ufumbuzi wa siri ya tukio la Yona? Kwa kuwa mtu aliyehukumiwa kwa hatia alikuwa kwa kawaida anatundikwa

msalabani kwa siku tatu mchana na usiku, basi hilo linamkumbusha mtu mithali ile ya Yesu kujifananisha na Yona ambayo imekwisha tajwa kabla. Yona pia anafikiriwa kukaa katika tumbo la nyangumi kwa siku tatu, mchana na usiku. Pengine yeye naye akatolewa katika saa tatu kwa mpango wa Mungu badala ya siku tatu. Basi kilichotendeka katika kisa cha Yesu ndicho kioo cha kuonesha kilichotendeka kwa Yona.

Sasa twageukia yaliyofanyika katika muda aliokaa Yesu Msalabani. Hata katika dakika ya mwisho Yesu alikuwa imara kudakuliza: Eloi, Eloi, lama sabachtani? (Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?) Huzuni kubwa iliyoje hiyo, na yenye kuumiza mno iliyoje hali hiyo ya kukata kwake tamaa! Kilio chake hicho chaashiria kwa uwazi kwenye ahadi ya zamani na matumaini ambayo pengine Mungu alikwisha mpa. La sivyo, kilio chake hicho hakina maana asilani. Hicho kinakataa katakata nia yake na upendo wake wa kujitwisha kwa hiyari mzigo wa dhambi za watu wengine, na kinakanusha moja kwa moja wazo hili ya kwamba yeye alitazamia kufikiwa na saa ya mauti wakati huo. Kwa nini kilio hicho cha maumivu ikiwa yeye mwenyewe alidai kuadhibiwa hivyo? Kwa nini kumlaumu Mungu ama kumwomba aokolewe? Maneno ya Yesu yanapaswa kuzingatiwa kutokana na yaliyofanyika hapo kabla. Yeye alikuwa akimwomba Mungu wakati wote kwamba kikombe kichungu kimwepuke.

Sisi Waislamu Waahmadiyya twaamini ya kuwa Yesu alivyokuwa mwema na mtukufu akamfanya Mungu asikatae maombi yake. Bila shaka alikwisha ambiwa ya kuwa dua yake imepokelewa tayari. Siamini katu ya kwamba yeye alitoa roho yake juu ya msalaba. Kwangu mimi hamna hapa hitilafu bali yote yanalingana na kuafikiana. Alihesabiwa kuwa mfu kwa sababu ya maoni ya mtazamaji fulani ambaye hakuwa daktari wala hakupata nafasi ya kumkagua. Mtazamaji tu mmoja aliyekuwa anamwangalia kutoka mbali akihangaika na kufadhaika isije Bwana wake mpendwa akafa, akaona tu kichwa chake kilichochoka sana kikainama na kikaegemea kifuani pake, basi akapaza tu sauti:

Lo, ametoa roho yake. Lakini tulivyosema mapema, hiki si kitabu cha kujadili ukweli wa maelezo ya Biblia na kuchunguza ya kwamba maandishi ya Biblia yanaweza kutegemewa ama hapana, au kubishana kuhusu maelezo yoyote yanayonasibishwa kwake. Hapa shabaha yetu ni kukagua tu mantiki na busara ya falsafa na itikadi ya Kikristo. Jambo ambalo limethibitika barabara ni kuwa Yesu alizimia au alikufa lakini kwa vyovyote mshangao wake unahakikisha ya kuwa yeye alitazamia kinyume kabisa cha kilichotendeka. Kama ni kifo alichotaka, basi mshangao wake aliodhihirisha hauna maana kabisa. Maelezo yetu sisi Waislamu Waahmadiyya ni kwamba Yesu alishangaa kwa sababu yeye aliahidiwa usiku mmoja kabla alipofanya maombi mbele ya Mungu ya kwamba ataokolewa katika kifo cha Msalabani. Lakini Mungu alitimiza ahadi yake kwa mpango wa kumfanya azirai ili walinzi waamini kwamba amekufa na wakamkabidhi Yusufu wa Arimathaya mwili wake ili kuwatolea jamaa zake. Mshangao wa Yesu tunaouona katika kauli yake ya mwisho, hata Pilato alishirikiana katika mshangao huo. Maana alipopashwa habari ya kifo cha Yesu, Pilato akasema kwa mshangao: 'Amekwisha kufa' (Marko 15:44). Haikosi yeye Pilato alitambua kwa sababu ya kazi yake hiyo ya kuwa Gavana wa Uyahudi kwa muda mrefu ya kwamba mtu hawezi kufa haraka hivyo juu ya msalaba. Alielewa sana ya kwamba mtu kupata kufa juu ya msalaba katika muda mdogo wa saa chache ni kinyume cha kawaida. Hata hivyo akakubali ombi la kutoa mwili katika hali hiyo kwa siri. Ndiyo sababu yeye analaumiwa siku zote kwamba alifanya mpango wa kumwokoa Yesu. Inasemekana ya kwamba kwa sababu ya kushawishiwa na mkewe alipanga kumtundika msalabani katika wakati ulio karibu sana na Sabato. Pili aliruhusu kutoa mwili ilhali ripoti ya kifo cha Yesu ilikuwa na shaka shaka. Uamuzi huo wa Pilato uliwahangaisha sana Wayahudi waliomlalamikia na kueleza shaka yao kuhusu kifo cha Yesu. (Mathayo 27:62-66).

Pia tunaona kutokana na Biblia ya kwamba mwili wake ulipoondolewa kutoka Msalabani, miguu yake haikuvunjwa, ilhali miguu ya wale wevi wawili waliowambwa pamoja naye msalabani ilivunjwa ili kuhakikisha kwamba wamekwisha kufa (Yohana 19:31-32). Kumwachilia Yesu hamna budi kulisaidia kumzindua katika hali ya kuzirai. Haiwezekani kukanusha uwezekano moja kwa moja ya kwamba walinzi waliagizwa na baadhi ya wajumbe wa Pilato wasimvunje Yesu Miguu yake. Pengine hiyo ilifanywa kama alama ya kumheshimu yeye na jamii ya Kikristo wasioelewa.
Kulingana na Biblia ubavu wake ulipochomwa mkuki ikabububujika damu na maji:

> Lakini walipomjia Yesu na kuona kuwa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu; lakini askari mmojawapo alimchoma ubavu kwa mkuki, na ikatoka damu na maji. (Yohana 19:33 -34)

Kama yeye alikwisha kufa na moyo wake uliacha kufanya kazi, isingeweza kububujika damu kwa wingi, damu iliyovilia na maji yake vingetoka pole pole. Lakini hiyo siyo picha iliyotolewa na Agano Jipya; bali linasema ya kwamba damu na maji vikabubujika (vikatoka kwa nguvu), ama 'vikatoka damu na maji mara moja'. (Hasa soma Biblia ya Kiingereza). Msishangae kuhusu 'maji' pia kutoka kwani Yesu alipata kuugua ugonjwa wa ngozi laini ya nje ya mapafu kwa sababu ya kusumbuliwa na kuudhika katika saa za kuadhibiwa juu ya msalaba. Pia shida ya kuwambwa msalabani inaweza kuleta maradhi hayo ya mapafu yanayoitwa kwa Kiingereza Pleurisy ambamo majimaji yanakusanyika kama vifuko vya maji. Hali kama hiyo kwa hakika huwa ya hatari sana na ya kuumiza kweli, lakini inaonekana hiyo ikamfaa Yesu kwani alipochomwa mkuki vifuko hivyo vya majimaji vilifanya kazi ya mto ili kumlinda sehemu zake muhimu za kifuani zisipate kuumia na mkuki. Maji yakichanganyika na damu yakatoka haraka kwa sababu ya moyo kufanya kazi barabara.

Kuna ushuhuda mwingine ninaoandika hapa chini. Sawa na maelezo ya Biblia, mara mwili ulipotolewa kwa Yusufu wa Arimathaya, ulipelekwa mahali pa siri ili kuzikwa katika kaburi lililofukuliwa katika mwamba ambamo mlikuwa na nafasi ya kutosha si kwa Yesu pekee bali na kwa wahudumu wawili pia ili kumwangalia na kumtunza:

> Basi wale wanafunzi wakaenda zao tena nyumbani kwao. Lakini Mariamu alikuwa akisimama karibu na kaburi, nje yake, analia. Basi akilia hivi aliinama na kuchungulia ndani ya kaburi. Akaona malaika wawili, wenye mavazi meupe, wameketi, mmoja kichwani na mmoja miguuni, hapo ulipolazwa mwili wa Yesu. (Yohana 20:10-12)

Si hivyo tu basi, bali pia twaambiwa katika Agano Jipya ya kwamba Yesu alipakwa juu ya majeraha yake marhamu iliyokuwa imetayarishwa mapema kwa kazi hiyo. Marhamu hiyo iliyotayarishwa na wanafunzi wa Yesu ilikuwa na dawa za kuponya jeraha na kutuliza maumivu na kadhalika. Mahangaiko ya nini hayo kwa kushughulikia kazi ngumu ya kutafuta madawa kumi na mawili yanayopatikana kwa nadra ili kutengeneza marhamu hiyo? Madawa hayo yametajwa katika vitabu vya zamani vya madawa kama vile kitabu mashuhuri cha kufundisha udaktari kiitwacho Al-Kanun kilichotungwa na Bu Ali Sina (Tazameni 'Nyongeza' kwa orodha ya vitabu vya aina hiyo). Kulikuwa na haja gani ya kupaka marhamu kwa maiti? Hiyo itakuwa na maana hapo tu ambapo wanafunzi walikuwa na sababu imara ya kuamini kwamba Yesu ataondolewa msalabani akiwa hai. Yohana Mtakatifu ndiye mtume wa pekee aliyediriki kutoa maelezo kwa nini marhamu ilitengenezwa na kupakwa kwa mwili wa Yesu. Hiyo inatia nguvu tena habari hii ya kwamba kupaka marhamu kwa mwili wa maiti ni kitendo kilicho kinyume kabisa na kawaida, kisichoweza kueleweka kwa wale waliomwamini Yesu kuwa mfu wakati wa kupakwa marhamu. Ndiyo maana Yohana alichukua jukumu la kutoa maelezo yake. Anasema kwamba marhamu ilipakwa kwa sababu Mayahudi walikuwa na

desturi ya kupaka marhamu ama dawa kwa maiti zao. Hapa pana jambo la muhimu sana kuzingatia ya kwamba, wataalamu wote wa kisasa wana rai moja ya kwamba Mtakatifu Yohana hakuwa wa asili ya Kiyahudi, na akisema hayo amehakikisha ukweli wa rai ya wataalamu hao. Inatambulikana pasipo shaka ya kwamba Wayahudi ama wana wa Israeli katu hawapaki marhamu yoyote kwa miili ya maiti zao. Kutokana na hilo watalaamu wakashikilia kwamba Yohana hana asili ya Kiyahudi, la sivyo asingelikuwa jahili asijue desturi za Kiyahudi. Basi kulikuwa na sababu nyingine ya kupaka marhamu.

Marhamu ilipakwa ili kumwokoa Yesu katika kifo. Sababu ya pekee ndiyo hii ya kwamba Yesu hakutazamiwa na wanafunzi wake kuwa atakufa wala kwa hakika hakufa juu ya msalaba. Mwili ulioteremshwa haikosi ulionesha alama halisi za uhai kabla ya kupakwa marhamu, waila kitendo cha waliopaka marhamu kitaonekana cha kipuuzi, kisicho cha akili na kisicho na maana. Haielekei ya kwamba waliotengeneza marhamu hiyo mapema sana wakafanya hivyo bila ya kuwa na ishara madhubuti ya kwamba Yesu hatakufa msalabani, bali ataondolewa akiwa hai akiwa na majeraha ya hatari na atahitaji dawa yenye nguvu kubwa ya kuponya.

Itambulikane ya kwamba eneo la kaburi alimolazwa Yesu liliwekwa katika hali ya siri kubwa waliyojua wanafunzi wake wachache tu. Hiyo ilikuwa kwa sababu dhahiri ya kwamba yeye alikuwa hai na bado alikuwa katika hali ya hatari ya kushikwa.

Ama yaliyofanyika humo kaburini, hilo ni jambo la kujadiliwa kwa jiha nyingi; wala haliwezi kuthibitika kwa uchunguzi mkali, na pia haiwezekani kuhakikika ya kwamba yule mtu aliyetoka katika kaburi alikuwa kweli amekufa na akafufuka kutoka wafu. Tunao ushuhuda wa pekee wa imani ya Wakristo ya kuwa Yesu aliyetoka humo kaburini alikuwa na mwili uleule uliokuwa umesulibiwa, ukiwa na alama zilezile na majeraha yaleyale. Kama alionekana akitoka na mwili huo huo, basi natija ya kiakili ndiyo tu ya kwamba yeye hakufa asilani.

Ushuhuda mwingine wa kuhakikisha kuwa Yesu alikuwa bado hai wala hakufa ndiyo ufuatao: Baada ya siku tatu, mchana na usiku, watu wa kawaida hawakumwona isipokuwa wanafunzi wake tu. Au tuseme akijitokeza mbele ya wale tu aliowategemea. Yeye hakuonana nao katika mwanga wa mchana bali katika giza la usiku. Mtu anaweza kutambua kutokana na maelezo ya Biblia ya kuwa Yesu anataka kuondoka katika hali ya hatari haraka sana na kwa kujificha. Pana swali hapa: Kama yeye alikuwa amejaaliwa uhai mpya wa milele baada ya kifo chake cha kwanza wala asingeweza kufa tena, kwa nini alijificha asionekane mbele ya maadui, yaani wajumbe wa serikali na watu wa kawaida? Ilimpasa kujitokeza mbele ya wajumbe wa serikali ya Kirumi na Wayahudi pia na kuwaambia: 'Nipo hapa nikiwa na uhai wa milele. Jaribuni kuniua tena kama mtaweza, lakini hamtaweza kamwe'. Lakini alihitaji kujificha. Siyo kwamba rai ya kujitokeza hadharani hakupewa; bali kinyume chake alishauriwa waziwazi ajidhihirishe kwa ulimwengu, lakini akakataa na akaendelea kwenda mbali ya Uyahudi ili mtu yeyote asiweze kumsaka:

> Yuda (siye Iskariote) akamwambia, Bwana imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu? (Yohana 14:22)

> Wakakikaribia kile kijiji walichokuwa wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele. Wakamshawishi wakisema, kaa pamoja nasi, kwa kuwa kumekuchwa, na mchana umekwisha. Akaingia ndani kukaa nao. (Luka 24:28-29).

Hilo linahakikisha ya kwamba yeye alikuwa mtu mwenye kufa asiye mbali na kufikiwa na mauti ama majeraha. Hiyo inayonesha tu ya kwamba Yesu alikuwa hajafa katika maana hii ya kwamba akaondolewa ule ubinadamu uliokuwamo ndani yake, bali akabaki kabisa kama alivyokuwa wala kifo hakikutokea kumtenganisha na mwili wa zamani na kumpa mwili mpya. Ndiyo kusema kwamba aliendelea kuishi pasipo kufa.

Roho inayohusikana na ulimwengu mwingine kabisa haitendi jinsi alivyotenda Yesu wakati alipokutana na marafiki na wafuasi wake kisiri saa za usiku katika giza.

Suala la Yesu kuwa roho limekataliwa katakata na Yesu mwenyewe. Yeye alipojidhihirisha kwa baadhi ya wanafunzi wake, hao wanafunzi hawakuweza kuficha hofu yao kwani walimwamini kwamba huyo siye Yesu mwenyewe bali ni roho yake. Yesu Kristo akitambua tatizo lao akafutilia mbali hofu yao kwa kukataa kwamba yeye siye roho bali yu Yesu yuleyule aliyekuwa amesulubiwa, hata akawakaribisha wachunguze wenyewe majeraha yake ambayo bado yalikuwa mabichi (Yohana 20:19-27). Kudhihirika kwake kwa wanafunzi na wengineo hakuhakikishi kwamwe ya kwamba yeye alifufuka katika wafu. Kilichothibitika ni kwamba yeye alipona katika uchungu wa mauti.

Yaonekana ili kuwaondolea shaka waliyokuwa nayo bado nyoyoni mwao, yeye akawauliza walikuwa wanakula nini. Na alipoambiwa kwamba walikuwa wanakula mikate na samaki, akawaomba apewe yeye pia kwani alisikia njaa na akala (Yohana 24:41-42). Hilo pasipo shaka yoyote ndilo hakikisho dhidi ya yeye kufufuka katika wafu, yaani kurejea ile hali ya asili ya mtu aliyekwisha kufa na kuhuika tena. Matatizo yazukayo kutokana na kuhuika huko yatakuwa mara dufu.

Kama Yesu bado alikuwa kitu kama mungu-mtu, jinsi inavyodaiwa alikuwa kabla ya kusulubiwa, basi alikuwa bado hajaepukana na 'mtu' ndani yake. Hilo linazusha hali ngumu ya kutatanisha. Kifo kilimfanya nini ama kiliwafanya nini, yaani yule 'mtu' ndani ya Yesu na yule 'mungu' ndani yake? Je, roho za wote wawili, 'mtu' na 'mungu', zilitoka na zikarejea ndani ya mwili huo huo wa udongo, baada ya kukaa katika jahanamu ile ile pamoja, ama hiyo ilikuwa roho ya mungu ndani ya Yesu iliyorejea katika mwili wa kibinadamu bila ya kufuatana na roho ya mtu? Roho hiyo ya mtu ilipotea wapi? Mtu anashangaa. Je, safari yake kwenda katika jahanamu iliishia mumo humo pasipo kurejea,

ilhali roho ya mungu ndani yake ilikaa tu humo kwa siku tatu mchana na usiku? Na Je, Mungu alikuwa baba wa Yesu-mtu ama Yesu mwana? Suala hilo linapaswa kutatuliwa kwa kutupatia picha safi. Je, mwili wa Yesu ulikuwa nusu wa Mungu na nusu wa mtu?

Fikara kumhusu Mungu tunayopata kutokana na Agano la Kale na Agano Jipya ni kwamba hana mwili, tena ameenea mahala pote, dhati yake siyo ya kiwiliwili. Tukiisha zingatia hiyo, hebu sasa tugeukie nyuma kumwangalia Yesu ambapo alikuwa anapita katika hali mbalimbali za kukua akiwa mimba ndani ya tumbo la uzazi la Mariamu. Kitu alichoumbika nacho Yesu kilitolewa chote na mama wa kibinadamu, hata sehemu sawa na punje ya haridali haikutolewa na Mungu Baba. Naam, Mungu angeliweza kumwumba kimuujiza. Lakini kulingana na maoni yangu, kiumbe ni kiumbe tu hata akiumbwa kikawaida ama kimwujiza. Twaweza kumkubali mtu kuwa baba wa mwanae hapo tu mwana huyo anapoumbika kutokana na mwili wa baba na mwili wa mama kwa usawa au kwa uchache sehemu walau ndogo sana wa mwili wa baba ipatikane katika uumbaji wa mwana.

Kutokana na maelezo hapo juu inapaswa kubainika kwa msomaji ya kwamba Mungu hakufanya kazi yoyote ya baba kabisa katika mimba kushikwa. Na kiwiliwili kizima pamoja na taratibu kuhusu moyo, kupumua, na utaratibu wa mwanzo na kuhusu ufa katika ini, mpango wa seli na taratibu ya neva, vyote hivyo viliumbika kutokana na mama wa kibinadamu pekee bila ya kusaidiwa na mwingine yeyote awaye. Basi iko wapi sehemu ya 'Uana' katika Yesu ambaye alikuwa ni chombo cha kuwekea roho iliyoumbwa na Mungu tu? Ufahamu huo mpya wa uhusiano baina ya Mungu na Yesu unaweza kuelezwa kiakili kwa namna lakini siyo kama uhusiano wa baba na mwana.

# 5 KUHUIKA AU KUFUFUKA

Habari ya Yesu kuhuika katika wafu inaleta matatizo mengi. Baadhi ya matatizo miongoni mwa hayo yamekwisha elezwa katika mlango uliopita. Sasa tunageukia baadhi ya sababu nyingine na matatizo mengine.

Tunachokusudia ni asili ya 'ubongo' wa Yesu kabla hajasulubiwa na baada ya kufufuka katika wafu. Ubongo wake ukahuishwa baada ya kuacha kufanya kazi kwa siku tatu mchana na usiku. Swali lenyewe ni kwamba mtu anapokufa ubongo unakuwaje hasa? Kuhusu jambo moja wataalamu wa matibabu walio Wakristo na wasio Wakristo wanapatana. Na jambo lenyewe ni ya kwamba ubongo ukifa kwa zaidi ya dakika chache unakufa kwa kudumu hauhuiki tena. Damu ikatikapo tu, ubongo huanza kuchanganua.

Kama Yesu alikufa juu ya msalaba, hiyo inamaanisha kuwa moyo wake ulikoma kufanya kazi na kuacha kupeleka damu kwenye ubongo wake na kwa hiyo ubongo wake ukafa haraka baadaye. Basi utaratibu mzima wa kusaidia uhai kubaki ukakoma kufanya kazi, la sivyo yeye asingeweza kuchukuliwa kwamba amekufa. Kama ni hivi, twakabiliwa na tatizo la kukanganya kuhusu ufahamu wa uhai na mauti ya Yesu Kristo.

Kifo cha Yesu Kristo, ilivyoelezwa nyuma, kinamaanisha kuondoka mwili wa kiroho, ama roho, katika kizimba cha mwili wa kibinadamu. Kama ni hivi, basi kuhuika kwake kutamaanisha kurejea mwili huo huo wa kiwiliwili aliouacha siku tatu kabla. Kurudi roho hivyo kutaanzisha upya uhai wa kiwiliwili. Na ili kutendeka hilo hakuna budi seli zilizokufa za ubongo zihuike ghafla na hali ya kuchanganuka haraka irudishwe nyuma kabisa.

Habari hiyo italeta matatizo mengi ambayo yatawadaia milele wanakemia Wakristo kuyatatua. Kueleza kurudi nyuma kabisa kuchanganuka na kuoza utaratibu wa kati wa ki-neva ni jambo lisiloweza kuwazwa na mwanasayansi. Kama kwa vyovyote ilifanyika, basi itakuwa ni mwujiza tu ukigongana na Sayansi na kuzidhihaki kanuni zilizoundwa na Mungu Mwenyewe; lakini itakuwa ni mwujiza ambao bado utashindwa kutatua tatizo lililoko mbele yetu.

Kuhuika hivyo siyo tu kuhuika seli za utaratibu wa kati wa ki-neva, bali kwa hakika kuziunganisha pamoja hadi zikawa kitu kimoja. Hata kama seli zilezile za zamani ziundwe tena na kuhuishwa kabisa zilivyokuwa hapo kabla, hata hivyo kwa hakika huo utakuwa utaratibu mpya wa seli usiokuwa kabisa na kumbukumbu ya zamani. Hizo hazitakuwa na budi kuundwa mara nyingine na kujazwa humo mambo yote yaliyolingana na maisha ya Yesu ambayo yalifutiliwa mbali katika ubongo wake baada ya kufa kwake.

Tujuavyo, uhai huwa na ufahamu unamojazwa taarifa mbalimbali zinazopatikana katika mabilioni ya neva zilizomo katika ubongo. Taarifa hiyo tena inagawanyika katika sehemu ndogondogo ngumu kufahamika zinazohusiana zenyewe kwa zenyewe za taarifa zilizohesabiwa ki-kompyuta zinazopokelewa kutoka katika kila nguvu miongoni mwa nguvu tano za kuona, kusikia, kunusa, kuonja na kugusa. Kama taarifa hizo zikifutika basi na uhai wenyewe unafutika. Kwahiyo, kuhuika kwa ubongo wa Yesu kunamaanisha kufanyiza kompyuta mpya ya ubongo pamoja na taarifa mpya kabisa na kadhalika humo ndani. Matatizo hayo yatahusika pia na kemia ya sehemu nyingine za mwili wa Yesu Kristo. Ili kuhuisha mwili kazi kubwa ya kufanyiza upya itaanzishwa baada ya kukomboa vilivyokwisha oza na kupotea. Mwujiza huo wote ukisha fanyika tayari, swali zitazuka nani alihuika na matokeo yake ni nini? Je, ni 'mtu' ndani ya Yesu aliyehuika, ama ni 'mungu' aliyekuwamo ndani yake? Ndiyo maana sisi tukasisitiza kuelewa vizuri uhakika wa dhati ya Yesu.

Wakati wowote Yesu anapoonekana amekosea na ameshindwa kudhihirisha nguvu zake kubwa akiwa Mwana wa Mungu, Wakristo wanajikinga kwa kudai ya kwamba yeye alikosea akiwa mtu siyo akiwa mungu. Kwahiyo tunayo kila haki ya kuuliza na kujua waziwazi sehemu gani ndani yake ilikuwa mtu na ipi mungu. Kukaa kwa mtu ndani ya Yesu kunataka ubongo wa 'mtu' mbali na ubongo wa 'mungu' ndani yake. Ubongo ulipohuika basi 'mtu' ndani ya Yesu alihuika, kwani Uungu wa Yesu hauhitaji ubongo wa kiwiliwili ili kumsaidia. Ubongo huo wa kiwiliwili uliingiwa tu na mungu alipokuwa ardhini mara ya kwanza, jinsi inavyokuwa katika mambo ya roho kwamba kitu fulani kinakuwa chombo ama njia ya kudhihirisha onyesho la kiroho. Basi kuhuika Yesu kutamaanisha kuhuika mtu ndani ya Yesu, kwani pasipo kuwa hivyo haiwezekani roho yake kurejea ndani ya mwili huo. Kama jambo hilo halikubaliwi, hapo tutalikabili tatizo jingine la kukubali kwamba Yesu alikuwa na bongo mbili mbalimbali za kujitegemea pindi alipokuwa duniani humu: Ubongo mmoja wa 'mtu' na mwingine wa 'mungu', zote mbili zikikaa mahali pamoja, lakini hazikulingana bali kila mmoja unajitegemea. Kama ni hivyo, basi suala la kuhuika lichunguzwe upya ili uhakika wake hasa utambulikane. Basi hamna haja tena ya kufikiria ubongo wa kibinadamu kufanyizwa upya ili kuipatia dhamiri mahali pa kukalia. Bali twahitaji kufikiria kwamba Yesu analitembelea tena fuvu la kichwa cha mtu aliyekuwa mwenyeji wake wa zamani, ambamo ndani ya fuvu hilo mna masazo ya ubongo yaliyooza.

Kadiri tunavyochunguza kwa uangalifu zaidi suala hilo, ndivyo yanavyojitokeza matatizo zaidi katika kila daraja la uchunguzi. Mtu anahitaji ubongo kuwa chombo cha mfuatano wa fikira. Kuhusu kazi zinazofanywa na mwili wa kiwiliwili ni kwamba kama tukiamini kuwa dhamiri inakuwapo peke yake na inaishi kwa kujitegemea, basi hiyo itamaanisha kwamba dhamiri na roho ni kitu kilekile kimoja. Waweza kuita dhamiri ama roho lakini inaishi peke yake hata kama uhusiano wake na ubongo wa mtu unakatika. Lakini kama dhamiri au roho inahitajika ili kuutawala

mwili wa mtu ama inaathirika na yanayotokea katika ufalme wake wa kiwiliwili, hapo bila shaka unahitajika ufungamano madhubuti baina ya dhamiri na ubongo ama roho na ubongo. La sivyo, hivyo (roho na ubongo) haviwezi kabisa kuathiri, kuhimiza au kutawala mafuatano ya kimwili na ya kiakili ama ya ki-maono katika mtu. Naona hilo halina haja ya kujadiliwa.

Hilo linatuongoza kwenye tatizo jingine kubwa zaidi: Je, anayefanywa kuwa Mwana wa Mungu anahitaji kuutawala ama kusimamia mwili kwa njia ya ubongo? Na je, yeye anautegemea ubongo wa kiwiliwili kwa mfuatano wa fikra zake? Kama yeye anavuka mipaka yote ya kibinadamu, na kama yeye anao mfumo wa kujitegemea wa mfuatano wa fikira ambao ni wa pekee kwake usiyo na kifani katika ulimwengu mzima aliouumba, hapo kurejea roho ya Mungu katika mwili wa mtu pamoja na dhamiri ya mtu kunaleta natija isiyolingana na akili yaani kupatikana kwa dhati iliyo na mifuatano miwili ya fikra inayopingana, kwani haiwezekani kwa dhamiri na roho ya mtu kulingana kikamilifu na dhamiri na dhati ya Mungu. Kutakuwa na upinzani wa kudumu baina ya mifuatano hiyo miwili utakaosababisha mapambano ya kusumbua baina ya mawimbi ya ubongo. Mwenye shida hiyo anafaa kutibiwa na mtaalamu wa utibabu wa maradhi ya roho mwenye uwezo zaidi ya mtu. Huo pengine ndiyo ugonjwa mpya wa roho uitwao *schizophrenia* kwa Kiingereza.

Baada ya kueleza hayo, tuliangalie jambo hilo kwa jiha nyingine. Nikiisha taali Ukristo mpaka undani wake kadiri fulani, nimetambua kwamba baadhi ya istilahi na matumizi yake havikueleweka barabara wala hapakutambulikana matokeo ya istilahi hizo zisipotumika mahali panapofaa. Nadharia ya Kikristo haieleweki vizuri akilini kwa sababu ya matatizo hayo na kutumia istilahi hizo pasipohusikana. 'Kuhuika upya' ni istilahi mojawapo na 'kufufuka' ni nyingine, ambazo zina muradi tofauti. Mpaka sasa tumetumia kusudi istilahi ya 'kuhuika' upya wakati wa kuzungumzia Yesu kupata uhai mara ya pili. Tulivyokwisha ona kutokana na maelezo ya hapo kabla, kuhuika upya kunamaanisha

kurejea kwa hali ambamo mwili wa kibinadamu unaanza kufanya kazi zote tena baada ya kufa. Lakini 'kufufuka' ni kitu kingine kabisa.

Kwa bahati mbaya Kanisa duniani kote linahusika na kuleta mpasuo katika mioyo ya Wakristo kwa kutumia vibaya istilahi hizo, kwa kuiweka mojawapo mahali pa ya pili, au kwa uchache kuinasibisha maana ya mojawapo kwa ile nyingine. Wakristo wengi wanafahamu kufufuka Yesu ni kuhuika kwa mwili huo huo wa kiwiliwili aliouacha wakati alipokufa wanavyofikiri. Naam, sisi hatuafikiani nao bali tunayo haki ya kuieleza hali hiyo kuwa kuzimia siyo kufa.

Kama maneno 'kufufuka kwa Yesu' yakifahamika sawasawa na kutumika vizuri, hayo hayawezi kumaanisha roho yake kurejea ndani ya mwili huo wa kibinadamu aliouacha wakati wa kufa. Kufufuka ndiyo istilahi ambayo inamaanisha tu kuumbika mwili mpya wa kiroho. Mwili huo asili yake ni ya kiroho na unafanya kazi kama chombo ambamo mna roho nyepesi zaidi. Huo unaumbwa ili kuendeleza maisha baada ya kufa. Baadhi ya watu wanauita mwili huo mwili wa nyota au *athma.* Hata ukiupa jina gani maana yake ni hiyohiyo moja. Ufufuo unatumika kwa uumbaji wa mwili mpya kimbinguni ama wa kiroho ambamo roho inakaa, siyo, twarudia, siyo kurejea ndani ya mwili uleule uliokwisha changanuka na kuoza ambao roho iliuondoka hapo kabla.

Mtakatifu Paulo amezungumzia ufufuo wa Yesu Kristo kabisa katika maana hiyo. Yeye aliamini katika ufufuo wa si Yesu tu bali na ufufuo kwa ujumla wa wale wote wanaokufa nao wanastahili machoni mwa Mungu kujaliwa kuwapo kupya na namna mpya ya maisha. Roho inakuwa hiyohiyo lakini makazi yake yanabadilika. Sawa na usemi wa Paulo Mtakatifu, hiyo ni kanuni ya kawaida ambayo haina budi ikubaliwe, la sivyo, Ukristo ama dini haitakuwa na maana.

Nyaraka za Paulo mtume kwa Wakarintho zinapaswa kusomwa kwa makini kwani hizo zina maana sana kuhusu suala hilo.

Hizo haziachi nafasi yoyote ya shaka, angalau kwangu mimi, ya kwamba wakati wowote yeye alipozungumzia Yesu kuonekana hai baada ya kusulibiwa, alizungumza waziwazi pasipo shaka kuhusu kufufuka tu kwa Yesu, wala haikupitia moyo wake kwamba roho ya Yesu imerejea katika mwili wake ule ule wenye kufa na akahuika kimwili baada ya kufa katika maana ya kawaida. Kama baadhi ya wataalamu wa Wakristo hawakubali nilivyoelewa kuhusu Paulo Mtakatifu, basi hapo hawatakuwa na budi kukubali ya kwamba Mtakatifu Paulo alijipinga kwa uchache katika baadhi ya maelezo kuhusu maisha mapya ya Yesu kuwa yeye alifufuka wala siyo kwamba mwili wake ulihuika ambamo roho yake inasemekana ilikuwa imefungwa.

Hapa chini kuna baadhi ya maneno yake yanayolingana na swala hilo yanayojieleza yenyewe:

> Naye Mungu alimfufua Bwana, na tena atatufufua sisi kwa uweza wake. (1Wakorintho 6:14).
>
> Kadhalika na kiyama ya wafu. Hupandwa katika uharibifu, kufufuliwa katika kutokuharibika; hupandwa katika aibu, kufufuliwa katika fahari; kupandwa katika udhaifu, kufufuliwa katika nguvu; kupandwa mwili wa asili, kufufuliwa mwili wa kiroho. Ikiwa uko mwili wa asili, na wa roho pia uko. (1Wakorintho 15:42-44).
>
> Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanada ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutakubalika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa. Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, mauti imemezwa kwa kushinda. (1 Wakorintho 15:52-54).
>
> Lakini tunao moyo mkuu; nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana. (2 Wakorintho 5:8).

Suala linalobakia kutatuliwa linazuka kutokana na Mtakatifu Paulo kutaja maelezo ya Wakristo wa kale kuhusu jinsi alivyoonekana Yesu akiwa hai katika mwili wake mara baada ya kusulibiwa. Kama Mtakatifu Paulo alifahamu ya kwamba Yesu alifufuka, yeye anaweza kuwa sawa, na yeye kumwona Yesu au kuongea naye kwaweza kuelezwa kwa sura ya ufufuo jinsi roho ya mtu aliyekufa inavyokuja kutoka ulimwengu mwingine ikijichukulia mzuka anayefanana sana na sura aliyokuwa nayo kabla ya kufa. Lakini hapa panaonekana habari hiyo imevurugika kwa sababu ya kuchanganya ushuhuda wa aina mbili. Kwanza twatakiwa kufikiria ushuhuda wa mwanzoni wa wanafunzi wake na wale waliompenda na kumheshimu ingawaje hawakuingia katika Ukristo kama desturi. Ushuhuda huo haikosi Mtakatifu Paulo akauelewa vibaya kwani huo unahakikisha kwamba Yesu alionekana katika sura ya binadamu ndani ya mwili wake wa kiwiliwili, jambo ambalo haliwezi kumaanisha ufufuo.
Ili kuthibitisha jambo hilo, mtu anapaswa kurejea habari ya Yesu kuwashangaza wanafunzi wake:

> Wakashtuka, wakaogopa sana, wakidhani ya kwamba wanaona roho. Akawaambia, mbona mnafadhaika? na kwa nini mnaona shaka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikeni-shikeni, muone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo. Na baada ya kusema hayo aliwaonyesha mikono yake na miguu yake. Basi walipokuwa hawajaamini kwa furaha, huku wakistaajabu, aliwaambia, mna chakula chochote hapa? Wakampa kipande cha samaki wa kuokwa. Akakitwaa, akala mbele yao.
> (Luka 24:37-43).

Tukio hilo linakanusha kabisa wazo la ufufuo na linaeleza ya kwamba Yesu alikusudia waziwazi kuwa yeye alikuwa mtu yule yule pamoja na mwili uleule wala hakuwa roho, wala siye mtu ambaye sasa hahitaji chakula ili kuishi. Hiyo inaonesha tena kuwa Wakristo wa kale walikuwa wakizungumzia mambo mawili tofauti. Kila walipozungumzia Yesu kuhuika na walipokabiliwa

na mashaka kuhusu wazo hilo la kipuuzi, wakakimbilia wazo la ufufuo ambalo wazo hilo linaweza kuelezwa kifalsafa na kimantiki. Waraka wa kwanza kwa Wakorintho hususan unatoa nafasi nzuri ya kutaali mashaka ya kukanyaga katika mashua mbili wakati mmoja.

Hatimaye, tukirejea kwa ushuhuda wa Wakristo wa kale kukutana na Yesu Kristo, hatubakiwi na njia yoyote isipokuwa kuamini ya kwamba yule Yesu aliyeonekana kwa wanafunzi wake wengi na marafiki zake mara baada ya kusulibiwa, na akaongea nao na akakaa nao na taratibu akaondoka kule alikosulibiwa zaidi katika giza la usiku, hakuwa kabisa mtu aliyefufuka bali alikuwa mtu ambaye pengine alihuika tu kimwili ama hakufa asilani bali akaokolewa kimwuujiza katika hali iliyokurubia sana kifo. Yeye alikuwa karibu kabisa na kifo hata kwamba hali yake inafanana na hali ya Yona katika tumbo la Nyangumi. Hatuna shaka ya kwamba kinachoweza kukubalika hasa ndiyo hali hiyo iliyoelezwa mwishoni.

Ili kuwarahisisishia Wakristo kuelewa nadharia yetu ningeonelea kuweka mbele yao mfano mmoja wa kukisia. Mathalan, mtu mmoja anawambwa msalabani kwa shabaha ya kumwua pale na anachukuliwa kuwa alikufa msalabani. Baadaye mtu huyo huyo anaonekana akitembea pamoja na baadhi ya marafiki zake. Hao wanashuhudia ya kwamba mwili wake unayo makovu yaliyosababishwa na majeraha aliyoyapata kwa ajili ya kuwambwa msalabani. Yeye anakamatwa tena na serikali na kuletwa mbele ya mahakama kwa mashtaka ya kwamba kwa kuwa yeye amepona katika mauti kwa sababu hii au ile hivyo asulubiwe tena ili kutimiza alivyohukumiwa. Lakini mtu huyo anajitetea akidai kwamba kwa kweli alikufa mara moja, kwahiyo shabaha ya sheria imekwisha timia tayari, na sasa kwa kuwa yeye amehuika kwa amri maalum ya Mungu kwahiyo hukumu ile ya zamani ya kumuua haiwezi kutekelezwa kwa mara ya pili, kwani sasa yeye amepata muda mpya tena wa kuishi ambamo katika muda huu yeye hajafanya uhalifu wa sheria.

Kama mahakama ikikubali hoja yake, ni dhahiri kwamba yeye hataadhibiwa mara nyingine kwa uhalifu ambao amekwisha adhibiwa.

Kama tukio la namna hiyo likitukia katika mahakama katika nchi ya Kikristo, jaji akiwa Mkristo, na baraza la Wakristo, msomaji anafikiriaje kuhusu mtu huyo ya kwamba watamhukumuje ama wanapaswa kumhukumuje? Kama hoja ya mtu anayechunguzwa inakataliwa na anahukumiwa kunyongwa tena, hiyo itakuwa sawa kwa msingi gani?

Ni dhahiri ya kwamba jaji yeyote mwenye akili, akiwa Mkristo au si Mkristo, na pia baraza la watu wenye akili timamu hawatakubali hata kidogo ya kwamba mshtakiwa huyu amehuika baada ya kwisha kufa. Hukumu ya aina hiyo haina upendeleo wa kimtaa, dini, taifa, ama kabila. Bali inahusikana na watu wote wala hamna mtu mwenye akili yake timamu awezaye kuwaza hukumu nyingine yoyote iwayo. Hivyo, shauri ya watu wote wenye akili na fahamu ni kukataa dai la kuhuika, bali kumhukumu kwamba alipona tu kifo. Ndivyo ilivyotendeka katika habari ya Yesu Kristo. Hakuhuika wala hakufufuka bali inavyoamua akili alipona mauti juu ya msalaba.

Kuhuika Yesu kimwili ni jambo la muhimu kabisa kabisa kwa Ukristo hata kwamba mtu anapaswa kuchunguza sababu zake. Kwa dhahiri hamna mantiki katika jambo hilo zima. Kwa nini anayehesabiwa kuwa Mwana wa Mungu akajichagulia kurejea tena katika kitundu cha mwili wa binadamu baada ya kwisha pata uhuru katika hicho? Na habari hiyo inawezaje kuwa hoja pasipo shaka ya kwamba yeye alikufa hasa na kisha akahuika tena? Hiyo habari imekwisha elezwa kiasi kadhaa nyuma wala sina nia ya kuikazania hapa tena, lakini ningependa kumwelekeza msomaji mwenye swali jingine la muhimu linalolingana na habari hiyo.

Kwa nini fikra hiyo ya kipuuzi ikaimarika katika dini ya Kikristo ambayo polepole katika muda wa karne chache baada ya Yesu ikawa nguzo mojawapo ya imani ya Kikristo ambayo pasipo nguzo hiyo jengo zima la theolojia ya Kikristo linabomoka?

Sisi tutajaribu kujitia katika dhamira za Wakristo wa kale waliokabili tatizo lisiloweza kutatulika, na tutaanza kuleta hali zile ambamo Ukristo ulipewa sura kinyume cha uhakika halisi. Kwa njia hiyo pengine itakuwa rahisi kufahamu hasa kuumbika na kuumbuka kwa Ukristo. Ukweli halisi unaotakiwa kuzingatiwa sana ndio huu ya kwamba ikiwa Yesu, amani iwe kwake, kweli amekufa msalabani, hana budi ataonekana machoni mwa Wayahudi kuwa nabii mwongo, mdanganyifu.

**MANENO MAKALI DHIDI YA WATUKUFU:**

Ilivyoelezwa hapo kabla, maandiko yalitabiri kuwa mdai mwongo aliyenasibisha chochote kwa Mungu asichosema Yeye, atatundikwa mtini. Kwahiyo kifo cha Yesu msalabani ndiyo sawasawa na kifo cha Ukristo. Ndiyo sababu maandiko yanayotegemewa ya dini ya Kiyahudi yanafurahia mno kifo cha Yesu juu ya msalaba. Alihesabiwa kwamba alithibitishwa kuwa mwongo pasipo shaka yoyote na maadui zake Wayahudi wa zama zake sawa na uamuzi huo maalum wa Biblia. Walikosa hata kumtaja kwa heshima na wakatumia maneno machafu mno ya kumtukana hata kwamba kuyasoma hayo hawezi kuvumilia yeyote anayempenda Yesu kama vile sisi tumpendao akiwa mtume mkweli mtukufu wa Mungu. Mtu anaweza kutambua kusumbuka na kuudhika mno kwa Wakristo wa kale waliomjua Yesu kuwa mtu mtukufu na Mjumbe mkweli wa Mungu aliyejaaliwa heshima maalum ya kuwa Masihi. Wakristo hao wangejiteteaje dhidi ya matusi hayo machafu ambayo yakisomwa leo katika mazingira ya siku hizi yanaleta moyoni picha chafu ya kitabu kiovu cha Salman Rushdie kiitwacho 'Satanic Verses'?
Kukosa adabu kabisa kwa wote hao inaonekana kumezuka kwa sababu ya kudharau sana ubinadamu. Maneno yafuatayo yatamsaidia kidogo msomaji kuelewa kwamba hulka bora za mtu zinapoteaje ambapo maadui wenye wazimu wa watu watukufu

wanapochagua kuwafanya shabaha ya kichaa chao kipotofu pasipo kuona haya.

Talmudi kilicho kitabu cha dini kinachoeleza kikamilifu mambo na imani za Wayahudi kilifundisha ya kwamba si tu ya kuwa Yesu alizaliwa kwa njia ya haramu bali kuzaliwa huko ni kubaya mara dufu kwa kusabibishwa na ndoa ya kishetani ya Mariamu iliyofungwa wakati yeye alipokuwa katika siku zake za hedhi. Kitabu hicho kilifafanua pia ya kuwa yeye alikuwa na roho ya Esau, na alikuwa mjinga, mpunga pepo, mtongozi na aliuawa msalabani na kuzikwa katika jahanamu na akafanywa sanamu ya kuabudiwa na wafuasi wake tangu wakati huo. Maneno yafuatayo yamechaguliwa kutoka kitabu 'The Talmud Unmasked', utungo wa Reverend I.B. Pranaitis.

> Yafuatayo yamesimuliwa katika Chuo *Kallah,* Ib (18b): "Safari moja wazee walipokuwa wameketi Langoni, vijana wawili waliwapitia, mmojawapo akifunika kichwa chake. Mwingine alikuwa kichwa wazi. Mwalimu Akibah akasema ya kwamba huyo mwenye kichwa wazi ndiye mwana haramu. Mwalimu Jehoschua akaongeza kusema kwamba huyo ndiye *ben niddah,* yaani mama yake alishika mimba yake alipokuwa mwezini. Mwalimu Akibah akasema tena kwamba huyo alikuwa na mabaya yote hayo mawili. Ndipo wengine wakamwuuliza Mwalimu Akibah kwa nini yeye anajasiri kuwapinga wenzake. Akajibu kuwa yeye anaweza kuthibitisha aliyosema. Basi akamwendea mama mzazi wa kijana huyo aliyekuwa ameketi akiuza mboga sokoni, na akamwambia: Binti yangu, kama ukinijibu sawasawa nitakayokuuliza sasa hivi, ninakuahidi utaokoka katika Akhera. Mama huyo akamtaka kwamba ale kiapo kwamba atatimiza ahadi, na Mwalimu Akibah akaitikia kwa kutikisa midomo tu, kwani moyoni alitangua kiapo. Hapo Mwalimu Akibah akamwuliza: 'Niambie mwanao huyu ni wa namna gani?' Mama akamjibu: 'Siku niliyoolewa nilikuwa mwezini, na kwa sababu hiyo mume akaniacha. Lakini ikaja roho moja chafu ikalala nami na huyo mtoto ndiyo akazaliwa kwa sababu ya ile roho chafu kuingiliana nami'. Basi ikathibitika ya kwamba kijana huyo hakuwa tu mwanaharamu bali pia akazaliwa kwa sababu ya mama yake kuingiliwa katika siku zake za hedhi. Na waulizaji wake waliposikiliza hayo wakatamka: 'Hakika Mwalimu Akibah ndiye mkuu alipowasahihisha wazee wake!' Na wakapaliza sauti: Mwenye mibaraka ndiye Mungu

> wa Israel aliyemfunulia siri Mwalimu Akibah mwana wa Yusufu!'" Jambo hili kwamba Wayahudi wanairejeza habari hiyo kwa Yesu na mama yake Mariamu, inaonekana wazi katika kitabu chao *Toldath Jeschu* - Uzazi wa Yesu - ambamo uzazi wa Mwokozi wetu umeelezwa takriban kwa maneno kama hayo.[1]

Uzuri wowote uliomo katika mtu unauchukia kabisa uchafu unukao uliorundikwa juu ya jina tukufu na heshima ya Yesu katika vitabu vya maadui zake wenye uhasama. Naam, mama mwema mtukufu Bi Mariamu alishika mimba ya Yesu wala hakuna chochote kiwacho kilichoshughulikia mimba hiyo kushikwa isipokuwa uwezo wa Mungu wa kuumba usio mipaka. Wazo la kushikwa mimba kwa sababu ya shetani kuingiliana katika hali ya hedhi inaafikiana zaidi na moyo uliodhania uovu huo wa kupita kiasi. Ole wao wapotevu ambao wake watukufu wa watu watukufu wala mama zao hawakuachiliwa na ndimi zao wala kalamu zao wanaotema sumu na ubaya kwa usawa. Haina tofauti kama mwenye wazimu wa aina hiyo kaishi miaka elfu mbili tangu leo ama akazaliwa katika zama zetu hizi. Ni la kushangaza sana jambo hili ya kwamba hata jamii zilizostaarabika mno za zama hizi zinaweza kufumba macho zisione unyama huo bali pengine zinatoa kibali kwa uhalifu mbaya sana eti kuna uhuru wa kusema na kuandika.

Lugha aliyotumia Salman Rushdie, kwa mfano kuwakashifu wake watukufu wa Mtume Mtukufu wa Islam siyo tofauti na lugha iliyotumika kumkashifu mama mtukufu wa Kristo:

Imesimuliwa pia katika *Sanhedrin,* 67a:

'

> 'Hayo ndiyo waliyotenda kwa mwana wa Stada katika Lud, na wakamsulubisha jioni ya Pasaka. Kwani mwana huyo wa Stada alikuwa mwanaye Pandira. Maana Mwalimu Chasda anatuambia ya kuwa Pandira alikuwa mume wa Stada aliyekuwa mamake, na yeye aliishi katika zama za Paphus mwana wa Jehuda.'

---

[1]The Talmud Unmasked, by Rev I. B. Pranaitis, Chap. 1 P. 30

Mwandishi wa 'The Talmud unmasked', Rev I.B. Pranaitis akifafanua maneno hayo juu akasema:

> 'Hayo yanamaanisha ya kwamba Mariamu ndiye aliyeitwa Stada, yaani malaya, kwani sawa na ilivyofundishwa hapo Pumbadita yeye alimwacha mumewe na akafanya uzinzi. Hayo pia yameandikwa katika Jerusalem Talmud na Maimonides'.
> 'Siwezi kusema ya kwamba wanaouamini uwongo huo wa kishetani wanastahili kuchukiwa sana ama kuhurumiwa.'

Hicho ni kilio cha uchungu kilichotoka katika moyo wa aliyeteswa asiyejiweza ambaye amehuzunishwa kwa sababu ya Bwana wake mpendwa kufanyiwa dhihaka kupita kiasi. Bila ya shaka Wakristo wa kale walisumbuka zaidi sana na kuudhiwa mno kwa sababu ya dhihaka ya Wayahudi wa zama hizo. Walilazimika kusumbuliwa na shutumu zilizotolewa dhidi ya yule ambaye si kwamba kumbukumbu lake lilisahaulika zamani, bali ukumbuko wake wa kupendeza bado ulikuwa mpya, ambaye alipendwa sana sana na wale waliowahi kumwona na kukaa naye muda fulani katika maisha. Haikosi hao waliudhika mara mbili, kwani haikuwa dhihaka ovu sana tu iliyowahuzunisha, bali na Yesu Kristo aliposumbuliwa wakati wa kuhukumiwa na kutundikwa msalabani kwa nia ya kuuawa hilo likaongeza dharau katika jeraha.

Mimi ningependa kwamba dhamiri ya nchi huru za Magharibi kwa uchache ijaribu kuzingatia uchungu na udhia wa bilioni ya Waislam ambao bila shaka wanasumbuka na kuudhika hivyo hivyo pindi lugha chafu ya kinyama inapotumika kumtukana Bwana wao mpendwa na Masahaba zake.

Wakristo wa kale walilazimika kuudhika ijapokuwa walijua sana ya kuwa Yesu alikuwa hai na walikuwa na ushuhuda usioweza kukanushwa ya kuwa Yesu hakufia msalabani jinsi Wayahudi walivyojigamba. Wao wenyewe walimtibu majeraha yake. Wakamwona akizinduka kimwujiza kutoka kwenye hali ya kuzirai sana ambayo katika hali hiyo walikabidhiwa mwili wake, na

wakamshuhudia wenyewe kwa macho yao siyo kwa sura ya mzuka au roho, bali katika mwili huo huo dhaifu wa kibinadamu uliosumbuka kwa ajili ya ukweli na ukapona kifo kimwujiza. Waliongea naye, na wakamwona akitembea hatua kwa hatua, usiku hadi usiku, katika hali ya siri kupakimbia alipotundikwa msalabani.

**KUPAA KWAKE:**

Habari ya Yesu Kristo kupaa haikutajwa na Mt. Mathayo na Mt. Yohana katika Injili zao. Kutokutaja habari hiyo ya muhimu kabisa kunashangaza mtu.

Katika Injili tatu zinazofanana katika kusimulia mambo, Injili mbili tu za Marko[2] na Luka[3] zinataja habari za kupaa kwa Yesu. Hata hivyo uchunguzi wa kisayansi na wa kitalaamu wa kisasa umethibitisha ya kuwa maneno ya kupaa kwa Yesu ndiyo nyongeza ya baadaye iliyofanywa katika Injili hizo mbili. Mistari hiyo haikuwamo katika matini ya asili. Codex Sinaiticus ndiyo Biblia ya zamani zaidi, ya tangu karne ya 4, ambamo mna Agano la kale na Agano Jipya kikamilifu takriban.[4] Biblia hiyo inashuhudia ya kwamba mistari kuhusu Yesu kupaa haimo katika Marko na Luka, bali iliongezwa baadaye na mwandishi fulani kwa upendo wake. Katika Codex Sinaiticus, Injili ya Marko inaishia kwa mstari wa 8 wa Mlango wa 16. Uhakika huo umekwisha tambuliwa katika baadhi ya chapa za kisasa za Biblia pia.[5]

---

[2] Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu. (Marko 16:19)

[3] Ikawa katika kuwabariki, alijitenga nao; akachukuliwa juu mbinguni. (Luka 24: 51)

[4] Uk 18 wa Jesus the Evidence, mwandishi Ian Wison (1984)

[5] Uk 1024 wa The Holy Bible, New International Version (1984), Imeenezwa na International Bible Society.

Vile vile Injili ya Luka ya (24: 51) ndani ya Codex Sinaiticus hamna maneno haya: 'akachukuliwa juu mbinguni' Sawa na mchunguzi wa maneno yaliyopata kuandikwa hivi au hivi, jina lake C.S.C. Williams, kama kweli mistari hiyo inakosekana katika Codex Sinaiticus, basi hamna tena habari ya Yesu kupaa katika matini halisi ya Injili.[6]

Hata mashahidi wa Jehovah wanaoamini sana Yesu kuwa 'Mwana' na kwamba yeye alipaa kwa Mungu Baba wamekiri mwishowe ya kwamba mistari hiyo ya Marko na Luka ndiyo nyongeza katika matini ya asili bila msingi wowote[7]

**ILITENDEKA NINI KWA MWILI WA YESU ?**

Uchunguzi mkubwa zaidi kwa kutumia busara na akili unadhihirisha mambo mengine tena yasiyo na maana yaliyomo katika tukio la Msalaba na kupaa jinsi Wakristo wa siku hizi wanavyoeleza. Ama kuhusu kurejea kwa Yesu katika mwili wa kibinadamu, tumekwisha sema vya kutosha. Hapa twapenda kuongeza kile kilichoweza kutokea kwa mwili huo ambapo Yesu alipaa mwishowe, kama kwa vyovyote alipaa.

Wakati wa kulikabili suala la kuwa mwili wa Yesu ulikuwaje, baadhi ya Wakristo wanasema yeye alipopaa kwa Babake wa mbinguni hapo kiwiliwili chake cha udongo kikachanganuka na kikapotea katika mwako. Habari hiyo inazusha swali la msingi: Kama kaondoka Yesu katika mwili wa kibinadamu kulikuwa ni tukio la kulipuka hivyo, kwa nini halikufanyika hilo wakati alipokufa mara ya kwanza inavyosemekana?

---

[6] The Secret of Mount Sinai, the story of finding the world's oldest Bible Codex Sinaiticus; by James Bently uk 131.

[7] New World Translation.

Habari ya kifo cha Yesu twasoma ndani ya Biblia mara tu wakati alipokuwa bado ametundikwa msalabani na Mt. Mathayo anaripoti akisema: Akaitoa roho yake. Ni dhahiri ya kwamba haikutendeka kitu isipokuwa tu roho yake ikatoka taratibu. Je twatazamiwa kuamini ya kuwa yeye hakufa basi juu ya msalaba, kwani kama angeliuacha mwili, mwili huo ungelipuka vivyo hivyo hata wakati huo? Kwa nini hiyo ilitendeka mara ya pili tu Yesu alipouacha mwili wake? Katika hali kama hiyo njia mbili tu ziko wazi ili kuendelea mbele:

1. Ya kwamba Yesu hakubaki akifungwa ndani ya mwili wa kibinadamu kwa kudumu baada ya roho yake kurejea mle ndani yake na kwamba wakati alipokuwa akipaa mara ya pili akauacha mwili wake wa kibinadamu na akapaa akiwa roho halisi ya Mungu.

Lakini hiyo hailingani na uhakika hasa wala haingii akilini, kwani hiyo itaongoza kwenye kichochoro kilichozibwa cha kuamini kwamba Yesu alikufa mara mbili, kwanza juu ya msalaba, na pili alipopaa.

2. Ya kwamba yeye alidumu milele akifungwa katika kiwiliwili cha kibinadamu.

Hiyo haiwezi kukubalika kwani inachukiza sana na ni kinyume kabisa cha heshima na utukufu wa Mungu.

Upande mwingine sisi tunayo nadharia inayolingana na busara: 'Itakuwa ni kosa kufahamu kupaa kwa Yesu kuwa safari ya kale ya angani, na mbingu kuwa mahali palipo nyuma ya jua, mwezi na magalaksi.' Ukweli hauko hapa wala pale.[8] Kisa hicho cha kuchekesha kilibuniwa kwa hakika kwa sababu ya tatizo lisilotatulika walilolikabili Wakristo wa zamani ambapo Ukristo ulikuwa unachimbuka. Yesu alipotoweka machoni pa watu, bila shaka swali lilizuka kwamba imefanyika nini kwake.

---

[8] The lion Handbook of Christian Belief, Lion, London (1982) uk 120.

Wakristo wa kale wasingeweza kutatua tata hilo kwa kutangaza hadharani ya kwamba kwa kuwa yeye hakufa asilani hivyo hakuna tena suala la mwili wake kuachwa nyuma na kwamba kwa hakika mwili wake umekwenda pamoja naye alipohama. Kwa njia hiyo suala la kutoweka mwili lingeweza kutatuliwa kwa urahisi. Lakini ilikuwa haiwezekani kukiri hilo. Wale ambao wangejasiri kukubali kwamba Yesu alionekana akiwa hai akiondoka taratibu kisirisiri nchi ya Kiyahudi wangejitia katika hatari ya kuhukumiwa na sheria ya Kirumi kwamba hao ndio waliomsaidia katika uhalifu wa kutoroka hukumu.

Kukimbilia kisa cha kubuniwa cha kupaa kwa Yesu hata kikiwa kinyume kabisa cha akili kulikubaliwa kwani kilikuwa cha kuwaletea usalama zaidi. Lakini hata hivyo kilikuwa cha uwongo. Twalazimika kuwasifu wanafunzi wa kale kwa maadili yao ambayo juu ya kuwa katika hatari hawakujitafutia usalama katika maneno ya kuongopa. Waandishi wote wa Injili walinyamaa kuhusu habari hiyo kuliko kujificha nyuma ya wingu la moshi la kuongopa. Hamna shaka walisumbuka kwa kuchekwa na maadui zao, lakini walikubali kuudhika wakikaa kimya.

Kimya kisichoelezeka cha hao waliojua habari hiyo kilisababisha kupanda mbegu ya shaka katika nyoyo za vizazi vya baadaye vya Wakristo. Hamna budi walishikwa na butwaa kwamba kwa nini habari ya mwili wa Yesu aliouacha nyuma haikutajwa baada ya yeye kukata roho? Mwili huo ulipotea wapi na ulikuwaje? Kwa nini roho ya Yesu iliuerejea mwili huohuo kama ulirejea? Maswali hayo ya muhimu yawezekana yalizusha maswali mengine pia. Kama kuhuika kunamaanisha kurejea roho yake katika mwili huohuo, ilifanyika nini kwa Yesu baada ya kipindi chake cha pili kufungwa ndani ya kiwiliwili hicho? Je, alipata kufungwa katika hicho milele pasipo kuachiliwa tena?

Upande mwingine, kama roho ya Yesu iliuwaga mwili huo mara ya pili, je, kuhuika huko kulikuwa kwa muda ama kwa milele? Kama yeye hakudumu kuwamo humo, ulikuwaje mwili wake baada ya kifo cha mara ya pili? Ulizikwa wapi na je, habari hiyo

imetajwa katika taarifa ama historia ya zamani ?
Inaonekana kwamba maswali hayo, hata kama hayakuzuka zamani zaidi, haikosi yalizuka katika karne za baadaye wakati ambapo wataalamu wa dini ya Kikristo walijishughulisha kwa bidii zao zote kufikiria falsafa na hekima ya fumbo kuhusu Yesu na mengine yote kulingana na hiyo.Yaonekana kwamba mwandishi fulani mpotofu alijaribu kujiokoa katika mushkili huo akaongeza mistari 12 ya mwisho katika Injili ya Mt. Marko na akanasibisha kwake kauli hii ya kwamba Yesu alionekana mara ya mwisho akipaa mbinguni katika mwili huo huo.
Mzushi huyo hakuiachilia mbali hata Injili ya Luka ambamo nyongeza yake ya kiujanja ya maneno haya 'akachukuliwa juu mbinguni' (24:51) yalimsaidia shabaha yake. Kwa njia hiyo yeye mwandishi huyo akaziba njia ya maulizo yoyote moja kwa moja. Kwa uchache tatizo moja la itikadi ya Kikristo likatatuliwa. Lakini, ole wao, kwa hasara gani? Kwa hasara ya kupoteza mambo mema halisi yaliyohusikana na dhati tukufu ya Yesu Kristo. Uhakika halisi wa Yesu ulitolewa dhabihu juu madhabahu ya uwongo na uzushi. Tangu hapo Ukristo uliendelea kusonga mbele katika safari ya kutoka kwenye hakika yake kuelekea kwenye ngano.
Twajua sana ya kwamba Wayahudi hawakuwa na furaha na walihangaika walipoukosa mwili wa Yesu Kristo.[9] Walitaka kuwa na hakika ya kwamba Yesu amekufa, na kwahiyo walihitaji thibitisho la kifo linalokubaliwa na watu wote, yaani kuwapo kwa maiti yake. Malalamiko yao mbele ya Pilato yanadhihirisha waziwazi kwamba walikuwa na wasiwasi wa mwili wake kutokomea.[10]
Jawabu halisi la kawaida limo katika uhakika huu ya kwamba kwa kuwa Kristo hakufa jinsi walivyoamini, hivyo swala la mwili kupotea halina maana, na tena sawa na ahadi yake yeye lazima

---

[9] Mathayo 28:11-15

[10] Mathayo 27:62-64

angeondoka Judea kwenda kutafuta kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea. Ni dhahiri yeye asingeweza kuonekana hapo tena.

**MAONI YA WAISLAM WAAHMADIYYA:**
Maoni ya Waislam Waahmadiyya kuhusu mwili wa Yesu kwamba ulikuwaje yako wazi, yanalingana na akili na ndiyo kweli kabisa. Jumuiya yetu inaeleza habari za Yesu na ilitendeka nini kwake katika mwanga wa ukweli ukizingirwa na utukufu wake. Hakika halisi ya Yesu Kristo ni nzuri sana kiasi hiki ya kwamba haina haja ya kuipamba kwa kuizulia fumbo la aina hiyo. Uhakika wake unazizingira taabu alizovumilia maisha yote kwa ajili ya wanadamu wenye dhambi ambazo zilifikia upeo wake alipotundikwa msalabani; na kuokolewa katika kifo cha msalabani ilivyoahidiwa na Mungu Mrehemevu Mkarimu Mwenye uwezo wote, na hatimaye akahama pale kwa kutafuta makabila kumi yaliyopotea ya Israeli.
Hivyo basi, yeye si tu aliyafikishia ujumbe wa Mungu makabila mawili aliyozungumza nayo kabla hajatundikwa msalabani bali na akayaendea vilevile makabila mengine ya Israeli na kwa njia hiyo akatimiza shabaha ya ujaji wake. Hapo ndipo akamalizia matilaba ya kazi yake ya dini. Hizo ndizo hakika bora na tukufu za maisha ya Yesu.
Mwanzilishi ya Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian alitangaza miaka mia moja takriban hapo kabla ya kwamba Yesu, Nabii mkweli wa Mungu, alipona kifo juu ya msalaba jinsi ilivyoelezwa katika maongezi hapo kabla. Mara ya kwanza katika historia ya Islam, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad akiongozwa na Mwenyezi Mungu akaondolea mbali pazia la mafumbo kwenye hakika zing'aazo za maisha ya Yesu . Yeye ndiye aliyetangaza akikabili hasira ya Waislam wengi wakali wa kufuata desturi zao ya kwamba Yesu

hakufia msalabani wala hakupaa mbinguni, bali akaokolewa kimwujiza akiwa hai pasipo kufia msalabani sawa na ahadi ya Mungu. Ndipo yeye Yesu akahama hapo ili kuwatafuta kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea jinsi alivyoahidi yeye mwenyewe.

Kwa kufuata njia inayoelekea yaliyoipita makabila ya Israeli mtu anaweza kukisia vizuri ya kuwa Yesu haikosi alisafiri nchini Afghanistan akielekea Kashmir na sehemu nyingine za India ambako iliripotiwa Waisraeli wanakaa.

Kuna ushuhuda madhubuti wa kihistoria ya kwamba Waafghanistani na Wakashimiri ndio vizazi vya makabila ya Kiyahudi yaliyohamia nchi hizo. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad alifichua siri hii ya kuwa Yesu hatimaye alifariki na akazikwa mjini Srinagar, Kashmir.

Waahmadiyya, maelezo hayo ya kuvutia na ya kweli kwa kufafanua kupotea kwa mwili wa Yesu katika nchi alimozaliwa, mara nyingine wanakataliwa ya kwamba hata kama Yesu hakufia msalabani bali aliondolewa akiwa hai, hata hivyo ni kubahatisha tu ya kwamba yeye alifunga safari ya hatari kutoka Judea kuelekea Kashmir. Wakisikia majibu hayo Waahmadiyya wanashangaa kwamba safari ipi ni ndefu zaidi, ile ya kutoka Palestino kuelekea Kashmir ama ile ya kutoka ardhini kuelekea sehemu za mwisho za mbinguni. Isitoshe, Waahmadiyya wanashangaa ilikuwaje ile ahadi ya Yesu Kristo ya kuwa yeye hana budi awaendee kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea. Kama yeye aliondoka moja kwa moja Palestina kuelekea kule kukaa upande wa kuume wa Baba yake, je alisahau wajibu wake ama haikuwezekana kwake kutimiza ahadi yake? Haikosi alisahau ahadi yake ama kama tulivyoshauri hapo kabla, je, yapasa kutazamiwa ya kuwa kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea walikwisha tangulia mapema zaidi kupaa mbinguni ambako Yesu alikwenda kuwafuata?

**MIFANO YA KUPONEA CHUPUCHUPU:**

Kwa wale ambao bado wanaona ni mushkili kuamini kwamba Yesu anaweza kupona kifo juu ya msalaba, twawaelekeza kwenye mifano ya baadhi ya watu katika historia waliopona kifo katika hali ya hatari kabisa kabisa. Na kwa kuona mifano hiyo, habari ya Yesu jinsi tulivyofafanua siyo ya kipuuzi wala siyo kwamba haiwezekani kuikubali. Kuna mifano mingi ya watu waliothibitishwa baada ya uchunguzi wa kidaktari kuwa karibu sana kufa, wakapona mauti katika hali ambamo mtu hawezi kusalimika kwa kawaida.

Mfano unaohakikishwa kwa maandiko ya kiserikali wa *maharaja* (sultani) wa eneo fulani katika India kabla ya kugawanyika Bara Hindi unafaa utajwe hapa. Maharaja huyo alipatwa na shida kubwa mno ambayo kwa kawaida ilikuwa haiwezekani kupona mauti. Maharaja huyo alilishwa sumu na mkewe na akaonekana amekufa. Sawa na desturi yao mwili wake ulipokuwa unachomwa moto uliokuwa unawaka sana mara ikavuma dhoruba kali kabisa. Matokeo yake, yeye si tu akapona kifo bali baada ya kupigania kesi yake katika mahakama ya sheria akarudishwa katika cheo chake cha kuwa maharaja. Kisa chenyewe ni kama hivi:

> Ramendra Narayan Roy alikuwa mwanamfalme wa eneo la Bhowal ambalo makao makuu ya Baraza yake ya hukumu yalikuwa Joydevpur. Ilidaiwa kwamba yeye alipewa sumu na akatangazwa kuwa maiti. Mwili wake ukawekwa pale pachomwapo maiti panapowaka moto, mnamo mei 1909. Mambo kadha yalielekeza kwamba mkewe ndiye alijaribu kumwua. Mvua kubwa ya radi kabla haujakamilika mchomo ikawafanya waliohusika kuchoma maiti kuondoka haraka pale na kuacha maiti. Mvua ilizima moto. Kundi moja la ma-Sadhu (watawa wa dini ya Hindu) likapitia hapo ambapo walimkuta mtu akiwa hai. Hivyo yeye akaokolewa. Keshoye ilipogunduliwa na wale waliokuwa wamekula njama kwamba mwili umetokomea pale wakachoma maiti ya mtu mwingine ili kudhihirisha kwamba kweli mwanamfalme amekwisha chomwa tayari.
>
> Masadhu hao waliomwokoa wakamchukua na kumpeleka mahali mbali mbali. Hiyo hali ya mwanamfalme kuwa karibu sana na mauti

> ilimwondolea uwezo wa kukumbuka mambo, Lakini pole pole akaanza kupata uwezo na akatembelea mji wa Joydevpur baada ya kupita miaka kumi na miwili. Mazingira ya mji wake yalimkumbusha mambo yote na akapata uwezo wa kukumbuka kikamilifu. Yeye alipodai katika mahakama ya kwamba yeye ndiye mrithi na mwenyewe wa Bhowal Estate, mkewe na wengineo wakateta sana na kukaidi. Kila kundi katika hayo mawili lilipigania vikali kesi hiyo. Mashahidi zaidi ya elfu moja walitoa ushahidi kwa ajili ya mwanamfalme na mia nne wakamtolea ushahidi mkewe. Tatizo hasa lilikuwa ni kuhakikisha kwamba bwana huyo ndiye yuleyule mwanamfalme kwani watu wote walitambua kwamba huyo alikufa miaka kumi na miwili iliyopita.
> Mwanafalme akashinda kesi, kwani aliweza kueleza baadhi ya alama katika mwili wa mkewe ambazo alama hizo asingeweza mtu kuzijua isipokuwa mumewe tu. Basi akakabidhiwa usultani wake.[11]

Malaki ya mifano kama hiyo pengine ilitukia bila kuripotiwa. Twashukuru kwamba siku hizi zipo njia za kisasa za utibabu na vyombo vya kueneza habari, basi mamia ya matukio ya aina hiyo yanapata kuripotiwa na kurekodiwa. Kama hiyo ndiyo kweli kuwahusu watu wa kawaida wa aina zote za jamii na kuhusu watu wa dini na khulka mbalimbali, kwa nini isiwezekane kumhusu Yesu?

Kama mtu yeyote ana nafasi ya kupona katika hali ya hatari kabisa ambamo kwa dhahiri haiwezekani kusalimika, basi Yesu alikuwa na nafasi hiyo zaidi kwa sababu ya ile hali maalum alimokuwamo yeye. Ni la kushangaza ya kwamba wenye mashaka wanayakanusha maoni ya kwamba Yesu alipona kifo juu ya msalaba. Lakini mara moja wanakubali jambo lisilowezekana zaidi, la kipuuzi lisilo la kawaida kwamba yeye alipata kuhuika baada ya kufa kabisa, na akaendelea kuwa maiti kwa siku tatu mchana na usiku, waaminivyo.

---

[11] The Bhowal Case, wakusanyaji: J.M.Mitra na R.C. Chakravarty, iliyoenezwa na Peer & Sons, Calcutta.

Uchunguzi wa kitabibu pia umevutiwa na ile hali ya kuwa karibu sana na mauti. Watu sabini na nane walichunguzwa waliosonga karibu sana mno na kifo. Wataalamu wa udaktari walikuwapo wenyewe katika matukio asilimia themanini ama wakawasili pale mara baada ya majaribu hayo. Ni la kuvutia ya kwamba asilimia 41 katika hao walitoa taarifa ya kwamba walipokuwa karibu kufa walikuwa wamekwisha chukuliwa kuwa maiti [12]

Kama wataalamu wa matibabu walio na vyombo vyote vya kuchunguza wanaweza kumtangaza mtu aliye hai kwamba amekwisha kufa tayari, unawezaje kutegemea ushuhuda wa mtu aliyefadhaika ambaye akamwona Yesu akizirai na akamwamini kwamba amekufa? Isitoshe, alipomwona hai baadaye akafikiri kwamba amehuika katika wafu; hiyo kabisa haiwezi kukubaliwa, ni kinyume cha uadilifu moja kwa moja.

[12] The Phenomenology of Near-Death Experiences, by Bruce Greyson M. D na Ian Stevenson M.D., A.M. Psychiatry 137:10, Oktoba 1980

# 6 UTATU

Mpaka sasa tumechunguza mambo yaliyolazimisha kuzua imani isiyo ya kweli ya kumfanya Yesu kuwa mungu na kazi yake inavyosemekana katika Utatu akiwa Mwana wa Mungu. Lakini nafsi ya tatu katika itikadi ya Kikristo ya Utatu, yaani Roho Mtakatifu, ni vigumu kufahamika. Kwa nini 'Mbili katika Moja' isitoshe, na iko haja gani ya kuongeza nafsi hiyo ya tatu katika itikadi ya kimsingi? Kiakili nafsi ya tatu kupewa nafasi katika imani ya Kikristo ya kuwa mungu haiko sawa. Harnack, aliyefafanua suala hilo, anafikiri kwamba mwanzoni Ukristo ulifahamika kuwa Umoja wa nafsi mbili za Mungu na Yesu. Baadaye kanisa likaongezwa humo likiitwa 'Roho' ili kulitilia maana ya uungu ambao pasipo huo nyongeza hiyo ya tatu ingeonekana tupu isiyovutia. Hiyo pia ikatenda kazi ya zana dhidi ya dini ya kiyahudi.[1] Kuhusu habari hiyo, Rev K.E. Kirk anasema katika makala yake juu ya *The Evolution of the Doctrine of Trinity* kama ifuatavyo :

> Kwa kawaida twawageukia waandishi wa zama hizo ili kujua wanayo misingi ipi ya itikadi yao. Twashangaa ya kwamba tunalazimika kukiri kuwa hawana msingi wowote. Suala walilolikabili halikuwa ni *kwa nini* ziwepo nafsi tatu, bali lilikuwa *kwa nini zisiwepo?'*

Yeye anaendelea kuainisha theolojia ya Kikristo kushindwa kabisa kuleta hoja ya kiakili kuthibitisha itikadi ya Utatu, na kwamba utatu wa Kikristo unaweza kuelezwa kuwa hasa itikadi katika

---

[1] Harnack, 'Constitution and Law of the church', E.T.uk 264

uwili ambamo kiliongezwa kitu cha tatu kilicho tofauti kabisa ili kuchora picha kamilifu zaidi.[2]

Sisi tunaamini ya kwamba nafsi hiyo (Roho Mtakatifu) ilipata kukua hatua kwa hatua kwa kuathirika na falsafa na hadithi za kipagani zisizo na msingi ambazo zilijaa tele tele katika ufalme wa Kirumi. Kubadilishana mawazo na hao watu bila shaka kuliwahimiza kumwamulia Roho Mtakatifu kiwango chake. Kwa kuwa upo ushuhuda wa kutosha sana kwamba zipo imani na madhehebu zilizomfahamu Mungu kuwa ameungwa na dhati tatu, kwahiyo ni vugumu kutafuta chanzo hasa cha itikadi ya Kikristo katika Utatu. Kwani kama kwa vyovyote mbili zaweza kuwa moja, na moja kuwa mbili kwa nini tatu zisiweze kuwa moja pia? Ni juu ya wataalamu wa uchunguzi kugundua barabara kwamba lini na namna gani nafsi ya tatu ya mungu wa Kikristo ilipata kuimarika katika mitholojia ya Kikristo. Lakini habari hiyo hivi sasa haihusikani na mazungumzo yetu. Hapa twanuia kuchunguza upuuzi wa madai kama hayo ambayo yanakataliwa na fahamu ya binadamu moja kwa moja. Tabia ya asili ya mtu inakataa katakata fikara zinazojipinga na zenye hitilafu.

## UHUSIANO WA NAFSI TATU ZENYEWE KWA ZENYEYWE:

Mtu anapotaka kutambua namna zinavyohusiana nafsi hizo tatu zenyewe kwa zenyewe ndizo hizi zifuatazo:

a. Hizo ndizo jiha mbalimbali za dhati moja.
b. Hizo ni dhati tatu mbalimbali zinazoshirikiana kwa usawa daima milele.
c. Hizo ni dhati tatu ambazo kila moja katika hizo ina baadhi ya sifa za pekee ambamo nyingine hazishirikiani nazo kikamilifu.

---

2. 'Essays on the Trinity and the Incarnation', mkusanyaji A.E. J. Rawlinson, Longmans, London ( 1928 )

d. Hizo ni dhati tatu katika moja, na kila moja inazo sifa zilezile na nguvu zilezile, na zote hizo zimeunganika pamoja, na kazi zao pia ni zilezile pasipo tofauti yoyote ile iwayo.

**HALI AU JIHA MBALI MBALI ZA NAFSI MOJA:**

Kuhusu jambo la kwanza linalowezekana miongoni mwa hayo manne hapo juu hakuna haja ya kulijadili zaidi, kwani hamna siku hizi Mkristo yeyote ambaye angemwamini Yesu kuwa hali ama jiha moja ya Mungu kuliko kuwa nafsi moja maalum. Wanaouamini utatu wanasisitiza kuwepo kwa nafsi tatu tofauti zilizounganika na zikawa moja.

Pindi mtu anapokubali habari hiyo ya nafsi moja yenye hali mbali mbali zikidhihirika wakati mmoja, papo hapo itikadi ya Utatu, yaani miungu watatu katika mmoja, inatokomea, pasipo kubakia utatu wowote kabisa. Basi atakayebakia ni Mungu Baba ambaye kwa kuona huruma atakufa kwa ajili ya madhambi ya watu. Na hiyo itakuwa ni hali ya kupita ya nafsi hiyohiyo. Hali mbalimbali siyo nafsi, wala jiha mbalimbali hazimaanishi dhati tofauti. Mtu yeyote anaweza kupitia hali mbalimbali bila ya kugawanyika katika wawili, watatu ama watu wengi. Hivyo, kama Mungu akiamua kufa kwa ajili ya watu wenye dhambi, basi ni Mungu mwenyewe atakayekufa siyo hali zake fulani tu zitakazokufa.

Basi kuhusu habari tunayozungumzia, ile hali ya Mungu ambayo ilifanya kazi kubwa sana ya kutoa dhabihu yake kwa ajili ya watu wenye dhambi inaweza kufahamika kuwa kazi ya sifa moja tu yake. Hivyo, kama huruma ya Mungu peke yake ikihesabiwa kuwa 'nafsi' na nafsi hiyo ikapewa jina Yesu Kristo, hapo kile kilichokufa ni 'huruma' ya Mungu. Upingamizi mkubwa ulioje huu ya kwamba huruma ya Mungu ikiwahurumia watu wenye dhambi inajiiua. Hiyo inamaanisha ya kwamba Mungu hakubakiwa na huruma kwa siku tatu mchana na usiku.

Kumbukeni kwamba hapo Yesu hakuhesabiwa nafsi tofauti ya kujitegemea, bali ni sifa ama hali ya huruma ya Mungu ambayo huruma hiyo ikadhihirika kwa sura ya mtu. Na mtu huyo kwa vyovyote ndiye Mungu mmoja asiyeweza kugawanyika. Basi kama chochote kilikufa katika kisa hicho, hicho ni Mungu Mwenyewe ama ni sifa yake ya Huruma iliyofanya kazi kubwa sana katika tukio hilo. Basi hatuna hiari yoyote isipokuwa kuamini kwamba Huruma ya Mungu ilikufa ama Mungu Mwenye Huruma Mwenyewe Alikufa.

Matatizo mengi yatazuka kutokana na madai ya kwamba hali au sifa fulani inaweza kufutika kwa muda ama kwa kudumu. Habari hiyo inaweza kueleweka vizuri ikilinganishwa na majaribu ya binadamu. Mtu anaweza kupoteza nguvu yake ya kuona au kusikia kwa muda au daima, lakini mtu huyo bado atabaki kuwa yule yule mtu aliye hai. Kifo cha nguvu moja ya mtu kwa hakika ni nusu kifo cha mtu huyo. Hatimaye mwenye kupata hasara ama kusumbuka anakuwa mtu yuleyule.

## NAFSI MBALI MBALI ZIKISHIRIKIANA KATIKA UMILELE:

Kama sehemu za mungu wa Kikristo ni nafsi tatu mbalimbali zikishirikiana pamoja milele, hapo swali litazuka kuhusu uhusiano wa ndani wa nafsi hizo. Kama hizo ni tatu daima zikifanyiza mungu mmoja, haikosi kila moja katika hizo tatu itakuwa na fikra yake na upendo wake binafsi hata kwamba taabu ya mmoja, kama anaweza kutaabika, ni taabu yake tu. Nafsi nyingine mbili zinaweza kuihurumia tu bila ya kushirikiana katika shida yake. Naam, haiwezekani kuwaza namna Mungu anavyofikiri na kuamua, lakini madai haya ya kwamba yeye kwa hakika ni nafsi tatu zilizounganika pamoja kufanyiza Mungu mmoja yanatupatia haki ya kujaribu kutafuta uhusiano wa ndani baina ya mifumo mitatu ya kujitegemea ya kufikiria.

Mfano wa kwanza unaweza kuwa wa mtoto mmoja aliyezaliwa na vichwa vitatu. Hali hiyo mbaya kupita kiasi inamaanisha ya kwamba huyo ni mtu mmoja kwa sababu kuna kiwiliwili kimoja, mikono miwili na miguu miwili, lakini vichwa vitatu vinaleta matatizo yasiyoweza kuelezeka hakika hasa ya kila kichwa katika hivyo vitatu. Kama viumbe visivyo vya kawaida vikiishi muda wa kutosha mpaka viweze kusema na kujieleza, hapo tu ndipo twaweza kuwauliza yanayofanyika katika vichwa vyao vitatu mbali mbali. Bila ya kuwa na ujuzi huo haiwezekani kuamua huyo ndiye mtu mmoja ambaye anashirikiana katika mawazo matatu ama ni watu watatu wanaoshirikiana katika mwili mmoja. Ni la ajabu ya kwamba jiha hiyo ya muhimu sana ya itikadi ya Kikristo haikuelezwa kabisa katika maandiko. Naam, kuhusu Kristo na Roho Mtakatifu kuna ushuhuda mwingi wa kuhakikisha ya kuwa hao ni wawili mbalimbali wasioshirikiana katika fikara wala katika maono. La sivyo, itakuwa vigumu kufahamu madhihirisho ya Roho Mtakatifu tofauti kabisa na Kristo, hususan katika kipindi ambamo Kristo alikuwa amefungwa katika mwili wa mtu.

Maswali ambayo yangezuka kuhusu kilichotendeka kwa Kristo, katika muda wa kusumbuka kwake, kwa kulinganishwa na sehemu mbili nyingine za Mungu wa Kikristo, ni haya yafuatayo:

1. Je, nafsi nyingine mbili, Mungu Baba na Roho Mtakatifu, zilishirikiana kwa njia yoyote katika mwili wa Yesu Kristo au katika majaribu yake kwa kulingana na mwili huo?
2. Je, Yesu peke yake alikuwa ndani ya mwili huo, na kwa hiyo yeye hakushirikiana na nafsi nyingine mbili za Utatu katika majaribu yake kwa kulingana na mwili huo?

Matokeo ya hilo la kwanza yamekwisha zungumzwa tayari. Na kuhusu hilo la pili tatizo jingine tena linazuka kuhusu uhusiano

wa Yesu na nafsi nyingine mbili za utatu katika muda wa Yesu kuwa katika mwili wa mtu. Je, katika muda huo wote Yesu alitengwa kikamilifu na nafsi nyingine mbili na akajitegemea, ama bado alibaki kuwa sehemu isiyoweza kutengwa na nyingine mbili isipokuwa tu yeye akashika makao yake katika mwili wa mtu pasipo kushirikiana na wenzake wawili? Sasa tunalo swali jingine tena la kulijibu:

3. Je, uungu wake mzima-mzima ulikuwamo ndani ya mwili wake wa kibinadamu, ama huo ulijitokeza tu nje kutoka kwenye 'sura' ya Mungu Baba na Roho Mtakatifu ambayo alishirikiana nao katika hiyo, kama kajidole kadogo kale kanakojitokeza nje ya mwili wa vidudu vidogo vidogo mno visivyoonekana pasipo kutumia hadubini kali?

Jambo hilo litatufanya tuamini pia ya kwamba katika kipindi hicho Yesu alikuwa mkubwa kuliko wenzake wawili, kwani yeye alishirikiana kwa usawa pamoja na Mungu Baba na Roho Mtakatifu katika 'mwili' wa kiungu, lakini hao wawili hawakushirikiana naye katika 'kajidole' kale kalikojitokeza ka 'mwili' wa mtu.

Hivyo basi, ili kurahisisha kuelewa habari yenyewe twajaribu kufafanua hitilafu zilizomo humo na mambo yasiyoeleweka akilini kwa kueleza hali mbalimbali za kukisia ili kutafuta ukweli. Naam, mifano hii isichukuliwe na wasomaji kuwa hasa ndivyo ilivyotendeka.

Suala lililoko mbele yetu ni kwamba je, yupo mtu mmoja anayedhihirisha sifa tatu ama anapitia hali tatu tofauti. Hiyo itazusha swali la kufikiria shauri ya 'Watatu katika Mmoja' na 'Mmoja katika Watatu', hususan kwa jiha malimbali tofauti, na yule yule mmoja kudhihirisha mienendo na hali mbalimbali.

Hali hiyo imekwisha elezwa kirefu katika mlango uliopita. Hapa iko haja ya kusisitiza tena habari hii ya kwamba ikiwa mtu mmoja

ama dhati moja inadhihirisha hali mbalimbali, basi haiwezi kuzidhihirisha hali hizo tofauti wakati huohuo mmoja bila ya kujigawa katika sehemu mbalimbali.

Kwa mfano, chukua maji kiasi fulani maalum. Maji hayo yanaweza kugeuzwa yote kuwa mvuke ama barafu pasipo kubakiza sura ya maji. Kama kunahitajika kuyaona katika sura zote tatu, hamna budi kuyagawa hayo maji katika sehemu tatu ili theluthi moja igeuzwe kuwa barafu na theluthi nyingine kuwa mvuke na theluthi moja ibakie kuwa maji. Kila sura itakuwa tofauti na sura ya sehemu nyinginezo wala yoyote katika hizo haitashirikiana na nyingine mbili wakati uleule mmoja. Kiasi hicho cha maji chaweza kugawanywa katika hali tatu, lakini ukubwa wa kila sehemu utakuwa mdogo kuliko yale maji kwa jumla yaliyochukuliwa mwanzoni, wala hamna yeyote awaye awezaye kusema kwamba hayo ni 'moja katika tatu' na 'tatu katika moja'. Kadhalika, basi, kudhihirika Kristo kwa sura ya binadamu ya Yesu, ilhali aliendelea kuungika na Yesu-mtu na Mungu Baba, haiwezekani asilani kueleweka akilini.

Wanadamu wote wameumbwa kwa vitu vilevile vimoja, lakini kufanana kwao wao kwa wao hakuwafanyi kuwa mtu mmoja pekee. Sifa zao tofauti, dhati zao mbalimbali, na wote hao kuwepo mbalimbali vinawagawa na wakagawanyika kuishi kila mmoja peke yake, ijapokuwa wote hao wameumbwa kutokana na kitu kilekile kimoja. Huwezi kuwaita 'mmoja katika bilioni tano' na 'bilioni tano katika mmoja' juu ya wote hao kushirikiana katika uanadamu.

Hebu sasa na tuchunguze suala hilo kwa jiha nyingine. Kama kwa muda fulani maalum Yesu alikuwa ametengana na Mungu Baba upande mmoja na katengana na Roho Mtakatifu upande mwingine na akapambanuka mbali na hao wawili, basi ni sehemu zipi na maeneo yepi ambamo Yesu alikuwapo peke yake? Kumbukeni kwamba hapo Yesu anatakiwa kukaa peke yake pasipo kubaki kuunganika na Baba na Roho Mtakatifu, hata kwamba kujitolea kwake kwa nduguze wanadamu, ama tuseme

nusu-nduguze binadamu, kufikiriwe kuwa majaribu yake binafsi tofauti kabisa na yale ya Mungu Baba na Roho Mtakatifu. Matokeo yake ni sisi kufikiria ya kwamba Kristo peke yake alihamisha nia yake ama fikra yake kutilia mwili wa udongo wa Yesu-mtu. Pia itafahamika kwamba yeye Kristo alipitia majaribu pasipo kushirikiana na sehemu nyingine mbili za utatu wa Kikristo. Inakanganya, au sivyo ?

**NAFSI MBALI MBALI ZENYE SIFA TOFAUTI KABISA**

Kama Mungu Baba, Yesu na Roho Mtakatifu ni nafsi tatu zenye sifa mbali mbali kabisa ambazo katika hizo hazishirikiani zote tatu, hapo hizo tatu haziwezi kuhesabiwa kuwa 'Tatu katika moja' na 'Moja katika tatu'. Utatu unaweza kuunganika ukawa umoja hasa hapo tu ambapo nafsi zote tatu zinakuwa na mienendo ile ile na sifa zile zile na kazi zile zile na nguvu zile zile za aina moja wala hamna hata sifa moja maalum inayoitenga moja na nafsi nyingine mbili.

Hiyo inaweza kufananishwa kiasi fulani na watoto watatu waliozaliwa kutokana na mimba moja ambao wanafanana sana sana kabisa, hata fikra zao, maono yao na kazi za viungo vyao vinaafikiana mno hata kwamba majaribu ya kila mmoja wao ni majaribu ya wote hao kikamilifu bila tofauti yoyote. Kama ndivyo ilivyo, hapo Utatu wa Mungu, Mwana na Roho Mtakatifu utaweza kueleweka zaidi. Lakini bado tatizo litabaki kuhusu miili mitatu yenye nafsi hizo tatu zinazofanana kwa kila jiha kikamilifu. Lakini hiyo haiafikiani na wazo la Kikristo juu ya Utatu. Mtu akiangalia mara ya pili analazimika kuwaza picha ya mwili mmoja wenye nafsi tatu mle ndani. Lakini umoja huo wa watatu unaweza kuzingatiwa hapo tu ambapo mwili mmoja ukiweza kuwa na nafsi tatu ndani yake, jambo ambalo linazua matatizo mengi. Naam, kwa kuwa Mungu hana mwili, kwahiyo mithali ya mwili wa kibinadamu ilivyoshauriwa nyuma haifai. Twajua sana ya kwamba Mungu hana mwili, lakini bado tatizo litabakia kuhusu

dhati tatu za kiroho zilizo kama wale watatu waliozaliwa kutokana na mimba moja wanaofanana, wanaokuwepo mbalimbali lakini wanaungana katika mambo mengine yote.

Tatizo jingine litakalowakabili hao watatu wa kukisiwa ni namna wanavyohusiana wao kwa wao katika habari ya ibada. Je, nafsi zote tatu za 'Tatu katika Moja' zinaabudiana zenyewe kwa zenyewe? Je, zote hizo zinapokea ibada za viumbe vyao, lakini haziabudiani zenyewe kwa zenyewe?

Ingawaje Yesu Kristo anatajwa mara kwa mara katika Agano Jipya akimwabudu Mungu Baba na anawasihi wengine pia kumwabudu Yeye. Lakini haikuelezwa kuhusu Roho Mtakatifu akimwabudu Mungu Baba. Tena hamna kabisa habari ya Yesu kujaribu kuwaelekeza wengine kumwabudu yeye wala kumwabudu Roho Mtakatifu sawa na taarifa ya Agano Jipya. Mtu anakanganywa na kutokutajwa kuabudiwa kwa Yesu na Roho Mtakatifu katika Agano Jipya, lakini habari ya Mungu Baba kuabudiwa imetajwa mara kwa mara.

Ijapokuwa ni desturi ya kawaida ya Wakristo kumwabudu Yesu kuwa 'Mwana wa Mungu' pamoja na kumwabudu Mungu Baba, hata hivyo hamna taarifa yoyote iliyohifadhiwa katika maandiko ya kwamba mwanafunzi yeyote wa Yesu Kristo aliwahi kumwabudu yeye, ama Yesu akawaelekeza kufanya hivyo katika muda wote aliokaa ardhini. Hata kama yeye angelifanya hivyo, maswali mengi yasiyoweza kujibika yangezuka. Ndivyo ilivyo hali ya Roho Mtakatifu, yeye naye hakumtaka yeyote kumwabudu yeye. Kwa nini?

Ile hali imekwisha chunguzwa tayari kiasi fulani ambako hao walikuwa 'Tatu katika Moja' katika maana hii ya kwamba utambuzi wao wa kuwapo kwao ulikuwa mmoja juu ya kugawanyika katika hali ama jiha tatu. Dhati ya aina hiyo haiwezi kiakili kuhesabiwa kuwa 'watu watatu katika mmoja'. Aidha, hali ama jiha haziabudiwi, wala hazijiabudu. Kwa kuwatambua kuwa watu watatu tofauti, wanalazimika kujijua wanakuwapo kwa

kujitegemea. La sivyo, suala la kujitaja ama kuwataja wengine kwa kusema 'Mimi', 'Wewe' na 'Yeye' halizuki asilani.

Utatu ukitumika kwa dhati moja humaanisha sifa tu basi. Na sifa kwa kweli hazina kikomo, haziwezi kuwa tatu tu. Tujue tusijue, Mungu anazo sifa nyingi teletele.

Kwa kumalizia mazungumzo haya, twasisitiza mara nyingine ya kwamba suala la wao kuabudu wao kwa wao linaweza kuzuka hapo tu ambapo hao wangekuwa watu watatu wenye madaraka mbalimbali na sifa tofauti.

Katika shauri hiyo, mmoja tu ataabudiwa na wengine wawili wakiwa wenye daraja dogo watatazamiwa kumwabudu yeye. Hilo lakubaliwa, lakini ule 'Umoja katika utatu' utatoweka. Hamna njia yoyote ya kuwa na 'Tatu katika Moja' na 'Moja katika Tatu', zote mbili hizo, wakati huohuo mmoja.

Hiyo imenikumbusha kisa kimoja cha kuchekesha ambacho ningependa kuwaambieni. Imesimuliwa ya kwamba wakati Tamerlane alipovamia mji wa Baghdad alifurahiwa na Bwana Joha, mcheshi wa mahakama, mpaka akaamua kumchukua pamoja naye kama mateka na akampa kazi maalum ya kuwa mchekeshaji mkuu wa korti. Inasemekana safari moja Joha akajawa na shauku ya kula nyama akiwa peke yake bila kushirikiana na wengine. Akashikwa na kiherehere hicho sana hadi hakuweza kujizuia. Basi akanunua nyama kilo mbili nzuri kabisa kutoka kwa muuza nyama. Alipomkabidhi mkewe nyama hiyo akaagiza kuichoma vizuri sana, lakini akamuambia hakuna atakayeila isipokuwa yeye peke yake, yaani Joha, hata mkewe hawezi kuionja. Sasa kwa bahati mbaya, mkewe alipokwisha tu kuichoma vizuri sana nyama hiyo, ghafula wakaja nduguze kadha kumtembelea. Hiyo ilikuwa furaha aliyopata ghafula, lakini ikawa habari mbaya ya kwa Joha. Harufu nzuri ya kuvutia iliwashinda hao ndugu za mkewe, na matokeo ndiyo unaweza kukisia. Wakala na kumaliza mpaka kipande cha mwisho kisha wakamwaga dada yao ambaye sasa akaanza kuhangaika. Lakini akajituliza kabla hajawasili nyumbani Bwana Joha, maana

alishawaza hila ama udhuru fulani ili kujiokoa katika hali hiyo ngumu. Joha alipoingia na akasikia harufu nzuri ya kuvutia ya nyama iliyochomwa ambayo ilikwisha liwa tayari, akamwagiza mkewe kuleta haraka hiyo nyama. Hapo mkewe akiashiria kwenye paka wa Joha aliyekuwa amemfuga kwa shauku sana, akasema: Toa nyama yako kutoka katika paka huyu, ukiweza. Maana nilipokuwa nimeshughulika, huyu akaila yote. Hapo haraka sana Joha akamshika paka na kumpima katika mizani. Kumbe uzito wake ulikuwa kilo mbili barabara. Basi kamwelekea mkewe kwa upole na akamuuliza: Mke wangu mpenzi, hakika nimekubali ulivyosema, lakini kama hiyo ndiyo nyama yangu, basi yuko wapi paka wangu; na kama huyu ndiye paka wangu, basi nyama yangu iko wapi!

Achilia mbali vichekesho, nisingependa kujadili suala hilo juu ya msingi wa mafunzo halisi na ya kweli ya Yesu. Maandiko haya shabaha yake hasa ni kuchunguza itikadi za sasa hivi za Kikristo ambazo twaamini kwamba zimepotoka na kwenda mbali kabisa na mafunzo ya asili ya Yesu.

Tukiisha kanusha habari ya Yesu kuabudiwa ndani ya Biblia, inatulazimu kufafanua sehemu ya pekee ndani ya Biblia, yaani Luka 24:52 ambamo Yesu anaonekana aliabudiwa. Wengine wanasema ya kuwa mstari huo unatoa ushahidi ya kwamba Yesu aliwahimiza kumwabudu. Wataalamu wa Kikristo wa zama hizi wanaelewa sana ya kwamba mistari hiyo imekwisha hakikishwa kuwa ya uwongo iliyoongezwa baadaye wala hakuna haki ya kuihesabu mistari hiyo kuwa sehemu halisi ya Injili ya Mt. Luka. Hebu sasa tugeukie kwa suala la desturi ya kawaida kwamba je hiyo inathibitika kwa ushuhuda uliomo katika Injili ama hapana. Sawa na desturi ya kawaida, Yesu anaabudiwa akiwa 'Mwana wa Mungu' katika madhehebu mengi ya Kikristo. Hata hivyo wote hao wanakiri ya kwamba Yesu huyohuyo mwenyewe alikuwa anamwabudu Mungu Baba peke yake.

Bure kabisa nimewauliza mara nyingi wataalamu wa Kikristo wenye ujuzi mwingi ya kwamba kwa nini Yesu alimwabudu

Mungu Baba ikiwa yeye mwenyewe alikuwa sehemu ya Mungu isiyoweza kutenguka na alikuwa ameunganika naye kabisa kikamilifu kwa kuleta maana ya umoja japo nafsi tatu zilikuwepo? Je siku yoyote aliwahi kumwabudu Roho Mtakatifu pia aliye nafsi ya tatu katika Utatu? Je, alijiabudu wakati wowote? Je, Roho Mtakatifu alimwabudu Yesu siku yoyote? Na je, Baba aliwahi siku yoyote kumwabudu yeyote miongoni mwa wawili wengine wa Utatu? Kama hapana kwa nini? Pengine majibu ya suala hilo yatawalazimisha Wakristo kukiri ya kwamba Baba anacho cheo kikubwa zaidi kuliko nafsi mbili nyingine za Utatu. Inathibitika kutokana na hiyo ya kwamba sehemu tatu za Utatu haziko sawa katika daraja. Hivyo, hao ndio 'Watatu katika Watatu' kama kwa vyovyote wako watatu, lakini siyo kabisa 'Watatu katika Mmoja'.
Wakati mwingine wataalamu wa Kikristo wanapokabiliwa na swali la Yesu, wanayemwamini kuwa Mwana wa Mungu, kumwabudu Mungu Baba, husema Yesu-mtu ndiye aliyemwabudu Mungu Baba, siye Yesu Mwana aliyemwabudu Yeye. Hiyo inatupeleka nyuma tena kwenye mazungumzo tuliyokwisha fafanua tayari. Je, mwili huohuo mmoja wa Yesu ulikaliwa na nafsi mbili, moja yenye dhamira ya binadamu na nyingine ya Mwana wa Mungu?
Aidha, kwa nini mtu ndani ya Yesu aliepa na kumpuzilia mbali kabisa Mwana wa Mungu aliyekuwemo ndani yake asimwabudu Kristo hata mara moja? Huyo huyo Yesu-mtu alitakiwa kumwabudu Roho Mtakatifu pia aliye nafsi ya tatu katika Utatu, lakini mbona hakufanya hivyo katu!
Ibada ni tendo la moyo na roho ambalo pengine huoneshwa kwa alama za kimwili, lakini lina mizizi yake katika fahamu na maono ya dhamiri ya mtu. Hivyo inapaswa kungunduliwa nani aliabudu pindi Yesu Kristo alipomwabudu Mungu. Tumekwisha eleza jambo hilo hapo kabla pamoja na matatizo yake ya kwamba Kristo, Mwana wa Mungu, ndiye aliyemwabudu Mungu. Kinyume chake, kama alikuwa ni mtu aliyemwabudu Mungu Baba, na huyo mtu hakumwabudu Kristo, kwa nini basi Wakristo

wanaukaidi mfano huo bora wa Yesu mwenyewe? Kwa nini wanaanza kumwabudu Kristo pamoja na Mungu, ilhali Yesu-mtu hakumwabudu mwenzake Kristo japo alikaa karibu yake mno.

**NAFSI TOFAUTI ZENYE SIFA ZIFANANAZO ZILIZO SAWA:**

Hebu tuchunguze mara nyingine tena, lakini safari hii kwa jiha tofauti kabisa, kanuni ya 'Tatu katika Moja' ndani ya Utatu, tukizichukua kuwa dhati tatu tofauti lakini zenye sifa zilezile zifananazo kabisa kikamilifu. Hapa hatuzungumzii dhati moja yenye sifa mbalimbali zilizounganika pamoja, bali twazungumzia dhati tatu kama watoto watatu waliozaliwa katika mimba moja. Twazungumzia hao watatu ambao wanafanana wao kwa wao sana kabisa hata kwamba kufanana kwao hakuishii tu katika kufanana umbo na sura, bali hata fikara zao na maono yao pia ni ya aina moja. Wanashirikiana katika fikira zao, maono yao na majaribu yao kwa namna moja kabisa. Hapo mtu hana budi kukiri ya kwamba nafsi mbili katika utatu hazina kazi tena, ni bure kabisa. Kama hizo mbili zikiondolewa mbali, hazitaleta kasoro yoyote ile iwayo kwa nafsi iliyobaki ya Utatu ambayo nafsi hiyo itakuwa kamilifu peke yake.

Kurani Tukufu pia inauliza swali hilo inapodokeza ya kwamba kama Mungu akiamua kumuangamiza na kumfutilia mbali kabisa Yesu Kristo na Roho Mtakatifu, tofauti gani itatokea kwa utukufu wake, Umilele wake na Ukamilifu wake, na ni nani awezaye kumzuia Yeye asifanye hivyo (5:18). Hiyo inamaanisha ya kwamba sifa zote za Mungu zitaendelea kufanya kazi milele na kwa hivyo itikadi ya Utatu ilivyoelezwa hivi sasa haina maana wala haihitajiki.

Lakini kama ifikiriwe ya kwamba dhati tatu hizo za utatu zinafanya kazi mbalimbali, hapo bila shaka sehemu zote tatu za utatu zitahitajika ili kufanyiza Mungu. Hata hivyo hapo patakuwa na Miungu watatu tofauti wanaosaidiana wao kwa wao na kukaa pamoja kwa amani kamilifu na hapo wanaweza kuhesabiwa 'Miungu Watatu katika Watatu' wala hapana 'Miungu Watatu katika Mmoja'.

Na kama isemwe ya kuwa Utatu ndiyo kama mtu mmoja mwenye viungo mbalimbali vinavyofanya kazi tofauti vikiunganika ndani ya mtu mmoja, hapo bila shaka Umoja utakuwepo lakini Utatu utatoweka. Lakini tukumbuke ya kwamba hatuzungumzii hapa mtu mmoja mwenye viungo kadha vinavyofanya kazi, bali watu watatu wanaofanana kabisa kwa kila hali na kila jiha, na kila mmoja akifanya kazi hizohizo za aina moja na hata hivyo kila moja anabaki kuwa mtu binafsi peke yake. Iliyojadiliwa ni hali ya mtu mmoja mwenye viungo kadha. Mpaka hapo sawa, hamna kilicho kinyume cha akili. Lakini viungo vikihesabiwa kuwa watu na palepale watu hao wote wakiwa pamoja wanafanyiza mtu mmoja kwa jumla, hapo habari hiyo inakuwa kinyume cha akili wala haiwezi kukubalika. Ni sawa kuwa kila kiungo kina kuwapo kwake, lakini kuwapo huko ndiyo sehemu tu ya mtu ambaye si tu kwamba anacho kiungo hicho tu kimoja bali anavyo viungo vingine pia. Viungo hivyo vikiwa pamoja ndani ya mtu huitwa 'mtu' kwa jumla. Naam, baadhi ya viungo vinafanya kazi ya muhimu zaidi na vingine vina kazi si ya muhimu sana, na mtu anabaki kuwa mtu bila ya viungo hivyo vyenye kazi isiyo muhimu, lakini mtu huyo atakuwa si mkamilifu, bali atakuwa na kasoro fulani. Mtu mkamilifu hupaswa kuwa na viungo vyote vile anavyokuwa navyo mtu yeyote kikawaida, na jumla ya viungo hivyo hufanyiza mtu mkamilifu.

Tukichukua mfano wa mtu mmoja aitwaye Paulo, mtu hawezi kusema ya kwamba kwa kuwa ini, moyo, mapafu na mafigo ya Paulo ni vitu maalum mbalimbali ambavyo vina kazi mbalimbali,

basi kwa hiyo hivyo ni nafsi mbalimbali zilizokamilika ambazo kila nafsi katika hizo ni sawasawa na Paulo. Kila kiungo chaweza kuwa Paulo hapo tu ambapo kwa mfano mafigo peke yake yafanye kazi zote kwa jumla anazofanya Paulo, na kadhalika kila kiungo kiwe hivyo hivyo. Jambo hilo linamaanisha ya kwamba viungo hivyo vikikosekana, hakuna badiliko litakalotokea katika Paulo. Au tuseme kwamba Paulo bado atabaki kuwa Paulo kikamilifu kama viungo vyake yaani mapafu, moyo, mafigo na ubongo, kwa hakika viungo vyote vikiondolewa mbali. Hiyo ni kwa sababu katika ukaguzi wa mwisho viungo hivyo vyote vinafanana, na dhati ya Paulo inabakia tu pale pasipo kujali viungo hivyo vipo ama havipo.

Kama hiyo ndiyo picha ya 'Tatu katika Moja', basi si sawa kujaribu kuchambua itikadi za Kikristo kwa kutumia mantiki na akili. Hapo akili itakayotumika kuhusu itikadi ya Kikristo ya siku hizi ndiyo akili ya wanawake wachawi wa Macbeth wanaposema: 'Safi ndiyo chafu na chafu ndiyo safi'.

## 7 MAGEUZI YENYE KUENDELEA YA UKRISTO

Imani ya Utatu ambayo ndiyo sehemu ya muhimu kabisa ya Ukristo haikuwepo katika Ukristo katika zama za uhai wa Yesu Kristo. Sana sana unaweza kuruhusu kukubali ya kwamba imani hiyo ilianzia kuzuka baada ya tukio la Msalaba. Ilichukua karne nyingi kufikia sura ya mwisho waziwazi lakini isiyoweza kuelezeka. Hiyo ikapitia majadiliano machungu sana na ubishi mkubwa baina ya wataalamu wa Kikristo na wana falsafa wa dini mbalimbali, utamaduni tofauti na mafundisho yaliyotokea zamani.

Dini ya Kikristo iliathirika na visa vya kubuniwa na simulizi za nchi zilizoupokea Ukristo katika zama za mwanzoni. Shina hasa la Ukristo lililouhifadhi na kulea ukuaji wa itikadi za Kikristo na falsafa yake katika zama za kale lilikuwa ni shina la Kiyahudi. Athari ya Kiyahudi ilikuwa kubwa zaidi katika muda wote wa mwanzo wa historia ya Ukristo. Wanafunzi wa Yesu waliojifunza na kutambua Ukristo moja kwa moja kutoka kwa Yesu na wakaushuhudia katika sura ya maisha yake, walihusikana na asili hiyo ya Kiyahudi. Hao walikuwa wasimamizi wa kwanza wa Ukristo na waliimarika sana katika mwanga wa maagizo ya Yesu na namna alivyoishi. Ndio hao walioshuhudia tukio la msalaba na wakajionea Yesu akipona jaribio hilo la mauaji.

### WAFUASI WA KWANZA WA YESU:

Wakristo wa kale wanaonekana waligawanyika kimsingi kuhusu asili ya Yesu na kwamba wafungamane na sheria ya Musa ama hapana. Katika kipindi cha pili cha maendeleo ya Ukristo, Mt. Paulo akawa mtu muhimu kabisa kwa kuupatia Ukristo falsafa

na fikira mpya. Kulikuwa hitilafu za kimsingi baina ya Paulo na James Mnyofu. Wakati James aliposimamia Kanisa la Jerusalem, Paulo alikuwa anahubiri katika nchi za Magharibi hususan wale wasiokuwa Wayahudi. Kanisa la Magharibi likapata mageuzi na maendeleo kulingana na maoni ya Paulo kuhusu itikadi, lakini Kanisa katika Jerusalemu likasonga mbele kushikamana na mafundisho katika umoja wa Mungu.

Natija moja ya mahubiri ya James ndiyo Waebioni, dhehebu ambalo jina lake limechukuliwa kutoka kwa neno *Ebionim* la Kiebrania, maana yake 'wapole' au 'maskini'. Hao walikuwa Wakristo waliotokana na Wayahudi ambao kwa ajili yao Yesu akashika kazi ya kuwa Masihi wala siyo ile ya 'Mwana wa Mungu'. Hao jamaa walishikilia kwa jazba kubwa sheria ya Musa na walikuwa na Injili yao wenyewe iitwayo kwa jina 'Injili ya Waebrania', 'Injili ya Waebioni' au 'Injili ya Wanazareti'. Hapa chini twatoa picha ya Waebioni iliyochukuliwa kutoka katika vitabu mbali mbali.

Katika 'The History of the Church' kilichoandikwa katika karne ya 4 baada ya Yesu huko Ceasaraea, mwandishi Eusebius anawataja Waebioni katika kitabu cha 3, *Vespasian to Trajan.* Yeye anawadhihaki maoni yao akisema kwamba hata jina lao linatokana na rai yao duni na 'maskini' kuhusu Yesu. Waebioni walimwamini Yesu kuwa binadamu mfile na walimheshimu kuwa mwema kwa ajili ya mienendo yake myema. Wakiwa Wayahudi waliishika sabato na sheria kikamilifu, wala hawakukubali wazo la Paulo kupata wokovu wa kutegemea imani tupu. Yeye analitaja pia kundi jingine la Waebioni walioamini kuzaliwa Yesu bila baba, na Roho Mtakatifu vile vile, lakini wakakataa kukubali kwamba Yesu alikuwapo tangu na tangu akiwa 'Mungu - Neno na Hekima'. Waliifuata 'Injili ya Waebrania' ambayo pengine ndiyo Injili ya Mathayo. Hao waliishika Sabato na desturi ya Kiyahudi, lakini waliusherehekea ufufuo[1]

---

[1] 'Eusebius: 'The History of the Church', uk 90-91 (Penguin 1989)

R. Eisenman na M. Wise wakieleza habari za Waebioni katika kitabu chao *The Dead Sea Scrolls Uncovered* (1992) wanasema ya kwamba James (Zaddik au Zadok, maana yake mwema, mkweli) alikuwa kiongozi wa Kanisa la Jerusalemu katikati ya karne ya kwanza (40- 60 AD takriban). Tawi hilo kwa kuangalia mambo ya nyuma likaitwa Ukristo wa Kiyahudi katika Palestino. Waebioni wakazalika kutokana na tawi hilo.[2]

Jumuiya iliyomfuata James ilijulikana kwa jina 'Masikini' (Wagalatia 2:10, Waraka wa Yakobo 2:3-5), cheo cha heshima kilichoelezwa katika Hotuba ya Mlimani na katika Dead Sea Scrolls. Kwa jiha nyingi Eisenman anafikiri ya kwamba Waebioni walifanana na waandishi wa Dead Sea Scrolls. Hao walimuheshimu Yakobo Mwema na walimwamini Yesu kuwa Masiha wao mwenye kufa, ilhali Paulo akawa *Mkufuru kwa Sheria*. Waliishika sheria na Sabato kwa jazba kubwa. Walimheshimu sana sana Yakobo lakini walimhesabu Paulo kuwa 'Adui' (Mathayo 13:25-40)[3].

Sawa na maoni ya Baigent, Leigh na Lincoln katika 'The Messianic Legacy', chanzo cha mafundisho ya asili ya Waebioni, Wagnosi, Wamaniki, Wasabi, Wamandai, Wanestori na Waelkasi ndicho falsafa ya Kinazareti. Hao wanaieleza fikara ya Kinazareti kuwa:

'

> Kuelekea kwa Yesu na Mafundisho yake yaliyochukuliwa kutoka kwenye hali ya asili ya Nazareti yalivyoelezwa wazi wazi na Yesu mwenyewe, kisha yakaenezwa na Yakobo, Jude au Judas Thomas na wafuasi wao wa mwanzoni'. Itikadi zao zilikuwa hizi:
>
> 1. Kushikamana sana na sheria ya Musa.
> 2. Kumtambua Yesu kuwa Masihi.
> 3. Kuamini kuzaliwa kwa Yesu kwa njia ya kawaida ya kibinadamu.
> 4. Ukinzani kwa maoni ya Paulo.

---

[2] 'The Dead Scrolls Uncovered', R. Eisenman na M. Wise, uk 186 (Element Books, 1992)

[3] 'The dead sea Scrolls Uncoverd', kilichotajwa nyuma, uk 233 -34)

> Kuna miswada mingi ya Kiarabu iliyowekwa katika maktaba ya Istanbul ambayo ndani yake kuna maneno yaliyonakiliwa kutoka katika matini ya karne ya 5 au 6, yalionasibishwa kwa 'al-nasara'. Miswada hiyo imeandikwa katika lugha ya kishamu na ilipatikana katika nyumba ya Watawa huko Khuzistan katika kusini- magharibi ya Iran karibu na mpaka wa Iraq. Hiyo inaeleza jamii ya mapadre wa Nazareti kutorokea Jerusalem baada ya maangamio ya mwaka 66 AD. Hiyo miswada inamtaja Yesu kuwa binadamu na inakazania sheria ya Kiyahudi kufuatwa.
> Wafuasi wa Paulo waliachana na dini ya Kristo na wakaelekea kwenye itikadi za kidini za Warumi'.[4]

Miongoni mwa itikadi mbali mbali zilizojitokeza katika kipindi ambamo Ukristo ulikuwa unafanyika, itikadi za wale tu zinaweza kuthaminiwa walioamini falsafa ya Kinazareti. Wakristo hao wa kale walifundishwa Ukristo na Yesu mwenyewe.

## KAZI YA MT. PAULO:

Ni dhahiri ya kwamba Mt. Paulo na fikara zake hamna hapo. Kwa hakika kutokea zama za Paulo na kuendelea mbele, kwa kuwa Ukristo ulienea katika nchi ngeni na itikadi za kipagani zikiwa ndani ya Ufalme wa Kirumi, hivyo Ukristo ukaathirika kwa nguvu sana na kupindika kwa utamaduni na simulizi zilizopata kuenea katika nchi hizo na ukaenda mbali zaidi na uhalisi wake wa kale. Mt. Paulo kadiri alivyoweza akaathiri na kuiharibu fikira ya Kikristo kwa kuongeza humo mafundisho ya mafumbo ya aina yake. Yeye hakutokana na Wayahudi[5] wala hakuonana na Yesu isipokuwa katika ndoto alivyodai. Inaonekana yeye alikuwa mapema chini ya athari kubwa sana ya utamaduni wa kigeni.

---

[4] 'The Messianic Legacy', M. Baigent, R. Leigh, H. L:incoln, k 135 - 138 (Corgi Books)

[5] 'The Hiram Key'. Christopher Knight and Robert Lomas, p. 246 (Century 1996)

Kwa dhahiri Mt. Paulo alikuwa hana budi kuchagua njia mojawapo katika njia mbili. Ama angechagua kupigana vikali dhidi ya mawazo mabovu yasiyo ya msingi ya kiuchawi, vizimwi na simulizi zilizotapakaa katika nchi za Ufalme wa Kirumi tangu zama za kale, au angelegea na kuuacha Ukristo kubadilika ili kuzifaa tamaa na falsafa za kupendwa na watu wengi katika ulimwengu usiokuwa wa Kiyahudi.

Maarifa hayo yalifanya kazi vizuri katika maana hii ya kwamba yalinyakuwa idadi kubwa ya wale walioikubali imani mpya ambao wasingeweza kupatikana kwa urahisi. Lakini kwa hasara gani? Kwa bahati mbaya hayo yaliishia katika mashindano mabaya baina ya khulka bora za Kikristo na mawazo ya kipagani yasiyo na msingi. Aliyoyageuza Mt. Paulo yalikuwa ni majina tu ya miungu ya kipagani na badala yake akayaleta majina ya Yesu, Mungu Baba na Roho Mtakatifu. Kwa hakika si Paulo aliyezua wazo lisilo na msingi la Utatu na kuliingiza katika upagani kwa jina la Ukristo, bali kinyume chake yeye aliiga fikira mbovu ya Utatu kutoka kwa mitholojia ya kipagani na akaiingiza katika Ukristo. Kutokea hapo huo ulikuwa ni upagani uleule wa zamani lakini ukapewa majina mapya na sura mpya.

Kwahiyo, Ukristo wa Kipaulo haukufaulu kubadilisha itikadi, simulizi zisizo na msingi na mawazo mabovu yasiyo na hakika ya ulimwengu wa kipagani, bali akaishia kuugeuza Ukristo na kuusawazisha na upagani. Mlima usipomwendea alipouita, basi akaamua yeye auendee.

## UHAKIKA WA YESU

Naam, kila mmoja anayo haki ya kujichagulia Ukristo mmojawapo miongoni mwa Ukristo wa Kipaulo na Ukristo wa Yakobo Mwema na viongozi wengine wa kale wa Kikristo waliokuwa wanafunzi wa Yesu Kristo mwenyewe. Lakini twapenda kuhakikisha hapa habari hii ya kwamba Ukristo halisi

uliendelea kusonga mbele kushikamana na imani katika Umoja wa Mungu na ukajiweka kando kabisa na bidaa zilizozuka baadaye zilizozalisha upayukaji na matatizo ya itikadi ya Kikristo kama vile Yesu kuwa Mwana wa Mungu, Utatu, Dhambi ya Asili, Wokovu, kuhuika Yesu kimwili baada ya kufa na kadhalika. Fikara za viongozi wa zamani wa Kanisa, Yakobo Mwema akijulikana zaidi kati yao, zilikuwa nyofu na halisi zisizokuwa na upingamizi wa ndani wala hitilafu zilizofichikana nyuma ya wingu la moshi la siri. Mtaala wa historia ya Imani ya Umoja wa Mungu katika Ukristo unahakikisha pasipo shaka ya kwamba Umoja wa Mungu usiofanywa kuwa mgumu kueleweka na kelele za utatu, uliendelea kuwa imani safi na rasmi ya Kanisa halisi la Kristo.

Tafadhali kumbukeni ya kwamba kitabu hiki kidogo hakina lengo la kuwaingiza Wakristo katika imani yoyote nyingine isipokuwa tu kuwaongoza kwenye imani halisi ya Kristo mwenyewe. Hili ni jaribio halisi la kuwakaribisha Wakristo warudi nyuma na kuiamini imani na amali safi ya Yesu isiyochanganyikana na mambo mengine yasiyotakikana. Hili ni jaribio aminifu kwa kuondoa yaliyobuniwa na kuleta mahali pake mambo ya kweli ya Ukristo - mambo ya kweli ambayo kwa hakika ndiyo mazuri kama yalivyo ya hakika na yanatuliza akili na moyo.

Siyo hekaya za kubuniwa kumhusu Yesu Kristo zilizoubakiza Ukristo tangu miaka karibuni elfu mbili na kuusaidia kupona miito ya akili na busara inayodumu ya kuzidi kwa sababu ya maendeleo ya sayansi, wala haukubaki kwa sababu ya itikadi ya kubuniwa ya Utatu. Kilichobakiza ukweli na kiini cha Ukristo ndiyo dhati na mafunzo ya Yesu Kristo. Sio uungu wa Yesu bali ni matendo yake bora matakatifu yanayovutia ili mtu afungamane nao. Uti wa mgongo wa Ukristo hasa ulikuwa ni yale masumbufu na subira na uvumilivu kwa ajili ya shabaha njema na kukataa kwa uaminifu majaribio yote ya kikatili ya kumlazimisha yeye kugeuza kanuni zake. Bado ni mzuri na wakupendwa hata leo jinsi ulivyokuwa hapo kabla. Huo umeziathiri kwa nguvu sana fikira na nyoyo za

Wakristo hata kwamba wamebakia kufungamana na Yesu na wanaonelea kufumba macho yao wasiangalie hitilafu za kiakili katika Utatu na kadhalika ni afadhali kuliko kutengana na Yesu. Utukufu wake hasa umo katika hakika hii ya kwamba yeye akazishinda nguvu za giza zilizokula njama kumtiisha ijapokuwa yeye alikuwa mnyonge sana wala si zaidi ya kuwa binadamu. Ushindi wa Yesu ni kitu wanachopaswa watoto wa Adamu kushirikiana katika hicho kwa fahari. Sawa na nadharia ya Waislamu, yeye alikuwa miongoni mwa kizazi bora sana cha Adamu. Yeye aliwafunza wanadamu kwa mfano wake wa kuvumilia alipokabiliwa na usumbufu mkali na uchungu mwingi sana. Ushindi mkuu wa Yesu ulikuwa kutokujisalimisha na kukaa imara katika hali ngumu sana ya majaribio makali. Ni maisha yake ya uchungu na usumbufu yaliyookoa wanadamu na yalimfanya ayashinde mauti. Kama yeye angelichagua kufa kwa hiari, kitendo chake hicho kingelikuwa sawa na kujaribu kuyakimbia hayo mateso. Mtu anawezaje kulihesabu tendo hilo kuwa ushujaa? Hata wale wanaojiua kwa kulazimika, kitendo chao pia kinahesabika kuwa cha woga tu. Kushirikiana katika shida maishani ni afadhali kuliko kuzikimbia kwa njia ya kujiua. Hivyo wazo la dhabihu kuu ya Yesu kwa kukubali mauti kwa ajili ya binadamu ndiyo maono matupu yasiyo na kiini mle ndani. Ubora wa Yesu, twasisitiza tena, ulikuwamo katika kujitolea kwake sana katika maisha mazima. Katika maisha yake yote yeye alishindana na vishawishi bila kulegea na kuyabadilisha maisha ya uchungu kwa maisha ya raha. Kila siku aliyakabili mauti lakini akakataa kulegea na akaishi ili awapatie wenye dhambi uzima. Aliyashinda mauti si kwa kujisalimisha kwa mauti bali kwa kukataa kunyongea mbele yake. Aliyashinda waziwazi na akajitoa katika mamlaka yake ambapo mtu mdogo zaidi angeweza kuangamia. Basi akahakikisha ukweli wake na ukweli wa maneno yake pasipo shaka yoyote. Ndivyo hivyo tumwonavyo Yesu na ndiyo sababu twampenda sana. Sauti yake ilikuwa sauti ya Mungu wala siyo sauti ya matakwa yake na tamaa zake. Alisema

aliyoamrishwa kusema, si zaidi wala si kidogo kuliko aliyoambiwa na Mungu kusema. Yeye alimwabudu Mungu maisha yake mazima, naam, alimwabudu Yeye peke yake, na hakumtaka yeyote mwenye kufa kuinama mbele yake wala mbele ya mamake au mbele ya Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo hakika ya Yesu ambayo tunawakaribisha Wakristo wa madhehebu yote na imani zote kuirejea.

**KUENDELEA DINI:**

Sisi twaziamini dini kuendelea na kupatikana kwa watu wote katika ulimwengu mzima. Ndiyo maana Islam inasisitiza desturi ya Unabii ndiyo kawaida kwa ulimwengu mzima, na inamaanisha ya kwamba manabii wote kwa jumla wanapaswa kukubaliwa. Kumkataa mmojawapo ndiyo kuwakataa wote hao, kwani mtu kwa hakika anawaamini wote kwa sababu wote hao wametoka katika chanzo kilekile kimoja. Basi neno 'kuendelea' dini linamaanisha kufanana namna fulani na 'maendeleo' ya uhai lakini siyo kabisa kama hayo. Tunaamini ujumbe kuendelea kusonga mbele pamoja na binadamu kupata maendeleo katika maeneo mbalimbali. Inaonekana kwamba sura za mwanzoni za dini zilizofunuliwa na Mungu ijapokuwa zilikuwa na mafundisho yale yale ya asili lakini yalikuwa na maelezo mafupi zaidi. Yaani maamrisho na makatazo yalikuwa machache zaidi. Kisha hayo yakapanuka na kuzidi katika idadi ya maamrisho na makatazo yaliyoenea katika maeneo makubwa zaidi ya shughuli za binadamu. Pia inaonekana ya kwamba dini zilizohusikana na utamaduni wa kale zilikuwa kwa watu wachache zaidi wa makabila ama jamii au eneo fulani tu. Ujumbe wao ulilingana na mahitaji yao machache katika zama hizo. Hizo zaweza kuchukuliwa kuwa dini za kikabila, za kiukoo ama za kitaifa. Mfano mmoja ufaao wa jambo hilo ndiyo Wana wa Israeli na mafundisho ya Kiyahudi.

Maelekeo ya kihistoria kwa maendeleo yaweza kuelezwa kwa kifupi kwamba yalikuwa ya pande mbili:

1. Mafundisho yaliendelea kusonga mbele hatua kwa hatua kuelezwa zaidi na kukamilika zaidi na zaidi.
2. Maeneo ya dini yalizidi pole pole kupanuka.

Kuendelea dini siyo maana yake ya kwamba dini iliyofunuliwa kwa Adamu dini hiyohiyo iliendelea kuongoza watu na ikaendelea kubadilika ikiongeza mafundisho na eneo lake. Bali twamaanisha ya kwamba katika sehemu mbalimbali za dunia ambako utamaduni wa aina mbali mbali uliimarika na kustawi, funuo za Mungu zikazalisha dini tofauti kwa kulingana na maendeleo ya kijamii ya binadamu katika sehemu hizo za dunia. Lakini dini hizo zote zilikuwa zinasonga mbele katika njia hiyo kwa jumla.

**UPEO WA MWISHO WA MAENDELEO YA DINI:**

Miongoni mwa madhehebu hayo ya dini, twaamini ya kwamba mojawapo katika Mashariki ya Kati ilikuwa inalelewa ili kuzalisha dini kubwa ambazo zingesaidia kuleta maendeleo ya kidini katika dunia nzima hadi kukamilika dini. Hiyo ndiyo wazi kabisa kutokana na mtaala wa historia ya dini. Uyahudi kufuatwa na Ukristo kufuatwa na Islam kunadokeza bayana upande yasongao maendeleo ya mafundisho ya dini. Baina ya dini hizo, maendeleo ya mafundisho yanaweza kutafutwa nyuma na mbele kwa urahisi na itaonekana kwamba hayo yanalingana sana. Kwahiyo ni muhimu kabisa kufahamu mpango huo mkubwa ungesababisha, na ukasababisha, kutimiliza na kukamilisha mafundisho hayo kwa sura ya dini moja kwa ajili ya watu wote yaani dini ya Kiislamu. Katika hali kama hiyo inafaa Wayahudi wakazanie kutambua umuhimu wa Yesu bila chuki au upendeleo. Waliposhindwa kumtambua yeye, mfano wa Wayahudi ni kama mfano wa aina

nyingi za wanyama ambao wamekwisha fukiwa katika historia ya mageuzi *(evolusheni),* ambao hawana kazi yoyote muhimu ya kufanya katika uhai uliposogelea karibu na upeo wake. Hivyo hali ya Wayahudi ndiyo kama mabaki ya historia tu lakini bado wanaendelea kubaki katika eneo dogo la kuwepo.

Aidha hali ya Wakristo ni kama hali ya Wayahudi, isipokuwa wamesimama hatua moja mbele kuliko hao, karibu zaidi na Islam katika utaratibu wa kihistoria. Naam, ni muhimu kuzingatia ya kwamba walipoachana na njia ya Yesu na kuanza kuifuata njia mbovu waliyotayarishiwa mwanzoni na Mt. Paulo, basi hiyo njia mbovu iliwapeleka mbali zaidi na Islam kuliko Wayahudi. Maana Wayahudi baada ya zaidi ya miaka elfu nne tangu kuwapo kwao wamejifunza kwa uchache somo la Umoja wa Mungu ulio wa muhimu kabisa kwa ajili ya uhai wa dini yoyote. Lakini juu ya kuwa karibu zaidi ya Islam katika imani za msingi, zipo sababu nyingine zilizowafanya Wayahudi kuwa wagumu zaidi katika kukataa kukubali Islam kwa wingi.

Mtaala huo unanifanya niamini ya kwamba Wayahudi wataendelea kuwa mbali na Islam kuliko Wakristo juu ya imani zao kufanana na imani za Kiislam, isipokuwa tu wakikuza ile hali ya moyo iliyo muhimu sana kumtambua Kristo. Wamekosa kiungo cha muhimu sana yaani Yesu Kristo, kilicho baina yao na ujaji wa Mtume Muhammad s.a.w. Kukanusha ukweli kuliwafanya wagumu kiasi cha juu sana hata kwamba kitabia hawako tayari kupokea ujumbe wowote mpya. Wanadumu kumngojea Kristo, ilhali Kristo alikuja na kaondoka tayari. Wakiisha kosa kumtambua mara ya kwanza, haielekei wao kumtambua tena katika ujaji wake wa mara ya pili.Yaonekana imekadiriwa kwamba wataendelea kumngojea milele Kristo wa mawazo yao.

Ni Kristo aliyekuja kutengeneza njia ya kuongoza kwenye dini ya daraja la juu zaidi ambayo ndiyo Islam. Maneno hayo yasichukuliwe kwa ukali zaidi. Hatuna maana kwamba Wayahudi kwanza waukubali Ukristo ndipo wachukue hatua nyingine ya

kuingia katika Islam. Fikira hiyo ni kinyume kabisa na busara. Tunachojaribu kudokeza ni kwamba watu ambao wamemkataa nabii ama mjumbe fulani ambaye hakuwa nabii wa kawaida tu, bali alikuja kufanya kazi muhimu kabisa ya kuwapatia mazoezi ya kififikira na kiroho, wamekataa kwa sababu wanaugua kiroho na kitabia. Mpaka maradhi hayo yaponywe na tabia yao iliyopindamana isiyopokea ukweli irekebishwe, haielekei sana kwamba watamkubali nabii aliyewahi kuwapo baada ya kiungo kile walichokwisha kosa kukitambua.

Ama kuwahusu Wakristo ni hivi kwamba hao wanaweza kuongozwa kwenye ukweli wa Mtume Muhammad s.a.w. hapo tu ambapo wanarejea kwenye ukweli na uhakika wa Yesu Kristo. Yeye hakuwa njia ya kuongoza kwa Mungu tu, bali pia alikuwa, kama walivyokuwa manabii wengine vilevile, njia ya kuongoza kwenye Nabii yule aliyekadiriwa kuja nyuma yake.

Yesu alikuwa ni kiungo cha kati katika mfano wa shamba la mizabibu. Katika mfano huo, bado Bwana mwenyewe, yaani Mjumbe mkamilifu wa Mungu, alibaki kufika. Kwa hiyo, mpaka Wakristo waachane na fikara mbovu ya mawazo yao yasiyo na msingi kumhusu Yesu Kristo, na kukubali uhakika hasa mtukufu wa Bwana wao Mtakatifu, hawawezi kuongozwa kwenye njia inayomwunganisha yeye na Mtume Muhammad, amani na baraka za Mungu ziwe kwake.

Mtume Muhammad s.a.w. alikuwa hakika hasa wala siyo wa kubuni na kwa kweli hakika huongoza kwenye hakika nyinginezo. Hivyo basi, siyo fikra za kubuni juu ya Yesu, bali ni uhakika wake hasa utakaowabariki Wakristo kutambua ukweli wa Mtume Muhammad s.a.w.

# 8 UKRISTO KATIKA ZAMA HIZI

Tatizo kubwa zaidi linaloukabili ulimwengu wa Kikristo siku hizi siyo kukosekana ufahamu kama kukosekana hamu na upendo wa kupokea ukweli. Ukristo ukiwa wa kubuni ama wa uhakika umekuwa sehemu ya utamaduni wa Magharibi isiyoweza kutengwa, na umefanya kazi muhimu katika shabaha zao za kikoloni na kibepari. Huo unaitilia nguvu mifumo yao ya kisiasa na kiuchumi na unawapatia nguvu ya kuwaunganisha inayowaweka katika hali imara ya umoja. Umefanya kazi kubwa sana katika kufuma na kuimarisha mfumo mgumu wa kijamii ya kisiasa na kiuchumi wa Magharibi. Tunachoelewa kuhusu utamaduni wa Magharibi au ubepari wa Magharibi na utawala wake wa kiuchumi ni kwamba huo wote umekwisha ingiliwa na Ukristo. Katika hali ya hivi sasa Ukristo unaonekana unaelekea kutumikia miradi ya kiwiliwili ya Magharibi vizuri zaidi kuliko ile ya kiroho, ilhali katika zama zilizopita kazi ya Ukristo ilielekea zaidi kuimarisha imani za Kikristo na kustawisha khulka bora.
Kazi kubwa zaidi ya kihistoria iliyofanywa na Ukristo ndiyo kujenga na kukuza ubepari wa Magharibi. Mashariki ilitekwa kwa moyo wa bidii wa Kikristo, na hususan vita vilivyopiganwa na Ufalme wa Kiislam vilisababishwa hasa na chuki ya Wakristo dhidi ya Islam.

**UKRISTO NA UKOLONI:**

Utawala wa kikoloni ulipotiisha karibu bara zima la Afrika na kuwafunga Waafrika katika minyororo ya siasa, Waafrika hawakukawia sana mpaka wakatiwa katika mikono yao na miguu

yao minyororo ya utumwa wa kiuchumi pia. Kupata madaraka ya kutawala hakuna maana pasipo kuwatiisha watu kiuchumi. Baada ya mabwana wa siasa na uchumi, hawakukawia zaidi Mapadre wa Kikristo kuwasili nyuma yao haraka wakivaa majoho ya unyenyekevu na kujitolea. Shabaha yao ya kuwasili Afrika ilionekana kinyume kabisa na ujaji wa watangulizi wao wa kisiasa na uchumi. Walikuja, walivyodai, si kuwatia utumwani bali kuwatoa utumwani roho zao Waafrika. Inashangaza ya kwamba Waafrika hawakuonea mashaka nia hiyo njema ilivyodaiwa. Kwa nini hawakuwauliza kwa adabu viongozi hao wakarimu wa Kanisa: Mbona mwazihurumia roho zetu tu pekee? Hamwoni miili yetu imetiwa utumwani bila kuonewa huruma? Mbona tumenyang'anywa pasipo sababu uhuru wetu wa siasa, na kutiwa minyororo ya utumwa wa kiuchumi? Kwa nini hamkutuhurumia katika hali yetu ya utumwa wa kimwili na kwa nini mwapenda kuziachisha huru roho za watu waliotiwa utumwani?

Hitilafu iliyomo humo iko wazi, lakini ni masikitiko ya kwamba haikuwa wazi sana kwa wale waliotegwa na hila za Kikristo. Afrika ni nyofu haina hila, na haina hila hata leo jinsi isivyokuwa na hila miaka mia mbili kabla. Waafrika hata leo hawaoni kwamba wametiwa katika utumwa wa kisiasa na kiuchumi kwa njia ya mfumo usioonekana unaosimamiwa kutoka mbali na ukoloni mamboleo. Bado hawajafahamu kwamba Ukristo kwao ndiyo njia ya kuwatiisha. Huo ni kama dawa ya kutuliza iliyowatia usingizi wa usahaulifu. Hiyo inawapatia ufahamu usio sawa kwamba wako chini ya mabwana zao kwa uchache katika kushirikiana nao katika kitu fulani kwa usawa.

Ufahamu huo wa kuwa chini yao ndiyo uliowaongoza kuiga mtindo ghali sana wa maisha ya Magharibi. Miti inabaki kupandikizwa katika nchi za kigeni, lakini matunda yake husafirishwa na kupelekwa kwa watu walioshindwa na mazoea ya ladha yake. Huo ni mfano mdogo wa kuonesha namna Ukristo ulivyo kitu cha lazima kwa kuutawala kibepari na kiuchumi Ulimwengu wa Tatu.

Katika magharibi yenyewe mtu wa kawaida, bila kujali anafahamu matatizo ya itikadi ya Ukristo ama hapana, anauona Ukristo ndiyo sehemu isiyoweza kutengwa ya ustaarabu na utamaduni wake. Yafaa ikumbukwe ya kwamba nguvu hasa ya khulka za Kikristo popote zinapobakia haimo katika imani za simulizi za Ukristo. Bali imo katika mkazo ule unaotiliwa katika upole, huruma, huduma katika shida na taabu, khulka nyinginezo ambazo zimekuwa sawa na maana ya Ukristo. Ijapokuwa Khulka hizo zinafundishwa katika dini zote za ulimwengu na zinaonekana ni shabaha ambayo Mungu aliwawekea watu wote kuipata, hata hivyo propaganda yenye nguvu ya Kikristo inadumu kusisitiza mambo hayo kuyanasibisha kwa Ukristo tu pekee, na imefaulu kuwaaminisha watu habari hiyo mwishowe. Ujumbe wa huruma, upole, wema, na mwenendo mwanana unafanya kazi kama muziki mwororo wa kuvutia. Huo ndiyo ulimwengu wa hadithi za kubuni na kupigwa chuku ambao kwa kawaida unavutia watu kuipokea imani ya Kikristo. Hata hivyo, papo hapo kwa kutengana na habari hiyo, zipo hakika madhubuti za kisiasa na kiuchumi za maisha ya Magharibi na hayo kuutisha ulimwengu uliosalia.

Yaonekana hitilafu zilizomo katika imani wanazolazimika Wakristo kuwa nazo zimekwisha ingia kwa namna fulani katika mwenendo wao wa kidunia pia. Upole, huruma, uvumilivu, kujitoa na maneno mengine ya aina hiyo yanafuatana pamoja na ukatili, ukandamizaji, dhuluma na kuwatiisha watu wengi sana wasioweza kujitetea. Kanuni ya sheria, Uadilifu na kutokupendelea ni mambo yanayotumika humo ndani ya utamaduni wa Magharibi pekee. Lakini katika uwanja wa uhusiano wa mataifa, hayo yanahesabiwa istilahi za kipuuzi zisizofaa ambazo zinathaminiwa na wajinga tu.

Siasa, maarifa ya ujumbe na uhusiano wa kiuchumi baina ya mataifa havina uadilifu isipokuwa tu vikilinufaisha taifa. Khulka za Kikristo hata zikiwa nzuri namna gani haziruhusiwi kuingia katika uwanja wa siasa na uchumi wa Magharibi. Hiyo ndiyo hitilafu ya hatari mno ya nyakati mamboleo.

Linapokuja suala la kudhihirisha uzuri wa Ukristo, hapo Ukristo unaoneshwa katika sura ya kuvutia ya ustaarbu na utamaduni wa Magharibi, kwa kuziita nchi za mashariki kwenye maisha ya raha na uhuru yanayoruhusu kila ulipendalo dhidi ya kawaida ngumu za jamii zao chakavu za kidini. Ujumbe huo wa kupata uhuru ulikosa sana kueleweka hasa na watu wa kawaida walioelimika kidogo katika Dunia ya Tatu na wakauchukua kuwa wa kuvutia sana. Ongeza katika hiyo ziada ya manufaa ya ki-saikolojia ya upataji wa fikara kuhusiana na ulimwengu ulioendelea mbele kwa njia ya dini moja, na hapo ndipo mtu anaaza kutambua kazi halisi ya Ukristo ya kuwavutia idadi kubwa ya watu waliokuwa wamekandamizwa, na mara nyingi watu mafukara waliodhulumiwa ambao ni watu wa chini kabisa katika jamii zilizogawanywa watu katika madaraja mbalimbali. Kuifahamu imani ya Kikristo ni nje ya uwezo wa watu hao. Hiyo inanyanyua daraja lao la kibinadamu, lakini siyo kwa hakika hasa.
Ingebainika kabisa kutokana na hayo yaliyoelezwa juu ya kwamba Ukristo tunaozungumzia uko mbali sana na Ukristo wa Yesu Kristo. Kuutambua utamaduni wa Magharibi kuwa Ukristo ni kosa lililowazi sana. Kuunasibisha kwa Kristo Ukristo ulivyo sasa katika maeneo mbalimbali kwa hakika ni kumtukana Kristo. Lakini kuhusu kila kanuni kuna baadhi ya mambo yanayotengwa mbali. Hatuna kauli inayofaa moja kwa moja kundi lolote lenye idadi kubwa. Hakuna shaka ya kwamba yapo matumaini kidogo na uhai katika ulimwengu wa Kikristo ambako uaminifu wa Kikristo, upendo wa kujitoa vinashikwa kwa kitendo kwa nia halisi. Hivyo ni visiwa vya matumaini ambavyo pembezoni mwake mna bahari zilizochafuka za maovu ambazo zinamomonyoa sehemu za visiwa hivyo na kuziingiza katika bahari. Kama ulimwengu wa Kikristo usingelipambwa na mifano ing'aayo ya Ukristo unaofuatwa sawasawa na jazba ya Yesu Kristo, japo uko mbali sana na yeye, bila shaka giza totoro lingelienea katika Magharibi hadi upeo wa macho. Pasipo Ukristo hamna mwanga katika utamaduni wa Magharibi, lakini nasikitika

mwanga huo nao unaendelea haraka kufifia.
Yaulazimu Ulimwengu wa Kikristo kurudi kwenye hakika ya Kristo na kujitibu nafsi iliyogawanyika na unafiki uliofichikana. Kuendelea kuishi katika ulimwengu wa kubuni na simulizi zisizo na msingi kuna hatari ya kuangamia. Shabaha hasa ya majaribio haya ni kuuamsha ulimwengu wa Kikristo ili utambue hatari zisizoonekana kwa dhahiri lakini zipo tu kwa hitilafu ziendeleazo kuzidi zilizopo baina ya imani na matendo. Simulizi zisizo na msingi ni kitu kizuri maadamu zinasaidia shabaha ya kuwatiisha watu wenye hali ya chini sana katika jamii kwa Mapadre wanaohusikana na mfumo unaowatawala na kuwanyonya kwa sababu ya ujinga wao kwa kuwaweka katika hali ya kipumbavu. Lakini linapokuja swala la imani kufanya kazi ili kuwahuisha wafu wa roho na kurekebisha khulka zao zinazoendelea kuharibika haraka, hapo ndipo simulizi hizo hazifai kabisa. Hayo kwa hakika ni mawazo tu, na mawazo hayawezi kufanya kazi ya maana sana katika mambo yanayomuhusu binadamu.

**UJAJI WA YESU KRISTO MARA YA PILI:**

Tuliyonena hapo juu sasa yanaweza kuoneshwa kwa kitendo. Suala la muhimu la binadamu kuokoka leo linaitegemea picha halisi ya Yesu Kristo. Kwahiyo, ni jambo la muhimu kabisa kuutambua uhakika wake. Alikuwa nani hasa na akiwa Kristo alifanya kazi gani ya muhimu kwanza katika jamii iliyochakaa ya Wayahudi? Kiasi gani cha uzito twaweza kutia katika ahadi yake ya kuja mara ya pili katika zama za mwisho? Hayo ni maswali muhimu ambayo hakuna budi kuyazungumzia.
Kama fikira kuhusu Yesu siyo ya kweli bali ni matokeo ya mawazo tu ya kibinadamu, hapo bila shaka haiwezekani kutambua ufikaji wake mara ya pili. Lakini Yesu hakuwa matokeo ya mawazo. Yeye alikuwa mtu hasa na akiwa hivyo anaweza

kuzaliwa tena akiwa mtoto wa binadamu wala hawezi kuteremka kama mzuka akiwatembelea mara nyingine wenye kufa. Mawazo kama hayo hayahusikani na hakika za maisha ya binadamu. Aidha, watu wanaoishi wakitosheka na mawazo yao matupu na simulizi za kubuni wanadumu katika hali yao hiyo pasipo kupata nafasi ya kumtambua mwokozi wao wakati afikapo.

Kama Yesu alikuwa kweli Mwana wa Mungu, kama Wakristo wanavyotutaka tuamini, hapo bila shaka yeye atakuja mara ya pili katika utukufu akiweka mikono yake juu ya mabega ya malaika wa kweli. Lakini kama hayo ni mawazo ya kubuni yaliyopigwa chuku ya matumaini na matamanio ya Wakristo, hapo ujaji wake hautatokea katu. Abadan dunia haitalishuhudia tukio hili la kipuuzi la mungu fulani kuteremka kutoka mbinguni katika sura ya binadamu pamoja na jeshi la malaika kumbeba na kumwimbia nyimbo za dini.

Fikira yenyewe hiyo inakataliwa na akili ya mtu na dhamira ya binadamu. Hiyo ni hekaya ya kizimwi ya kipuuzi zaidi iliyozushwa kwa kutumbuiza akili za watu fulani. Kinyume chake, kama fikira ya Kiahmadiyya ikubaliwe kumhusu Yesu Kristo, hapo picha hiyo ya ajabu itabadilika kuwa picha nyingine ambayo siyo tu kwamba inakubaliwa na akili ya mtu, bali inaungwa mkono kwa nguvu na historia nzima ya kidini ya binadamu. Na hapo tutakuwa tunatizamia ujaji wa mwokozi asiye tofauti na Kristo katika ujaji wake wa mara ya kwanza. Tutakuwa twatazamia ujaji wa mtu mpole, mwenye kuzaliwa katika ukoo mpole kama Yesu Kristo alivyokuwa katika ujaji wake wa mara ya kwanza, atakayeanza kazi yake ya mahubiri kwa namna alivyofanya mara ya kwanza. Atatokana na watu wa dini wafananao na Wayahudi wa Judea katika tabia na hali. Na hao si tu kwamba watamkataa na kumtenga kwa sababu ya yeye kudai kuwa mwongozi aliyeahidiwa waliyemtazamia kufika akiwa mwokozi kutoka kwa Mungu, bali nao watafanya chini juu ili kumwangamiza. Ataishi alivyoishi Kristo kwa jumla na atafanyiwa dhihaka, chuki na ujeuri alivyofanyiwa Yesu. Atasumbuka mara nyingine, si kwa mikono

ya watu wake, bali kwa mikono ya maadui zake wafananao na wale waliomsumbua hapo kabla. Yeye atasumbuliwa vile vile na nguvu kubwa kabisa ya utawala wa kigeni ambao chini ya utawala huo atakuwa amezaliwa miongoni mwa watu waliofanywa kuwa watumwa.

P.D. Ouspensky, mwandishi habari maarufu aliye Mrusi wa mwanzo wa karne ya ishirini, akiandika juu ya kutokea kwa Yesu Kristo mara ya pili alishirikiana katika maoni ya aina hiyo Akaandika:

> Kwa vyovyote hii siyo fikira mpya ya kwamba Kristo akizaliwa ardhini baadaye siyo kwamba hatakuwa kiongozi wa Kanisa la Kikristo, bali pengine hatahusiana na hilo na katika zama nzuri sana za nguvu na uwezo wa Kanisa yeye kwa yakini atatangazwa kuwa mzushi na kuchomwa kufungiwa na mti. Hata katika zama zetu hizi za mwanga ambapo makanisa ya Kikristo japo hayajaachana na mambo yake yaliyo kinyume cha Ukristo lakini yameanza kuyaficha, Kristo ataweza kuishi pasipo kupata kudhulumiwa na 'Waandishi na Mafarisayo', labda huko katika nyumba ya watawa katika Urusi peke yake.[1]

Hiyo ndiyo njia ya pekee ya kuletwa manabii na waongozi wa dini. Nadharia yoyote nyingine ni tupu ya uwongo na isiyo na maana.

Siku zote inakuwa hivi ya kwamba wakati ambapo bishara za manabii kuhusu ujaji wa waongozi wa dini zinapokwisha timia, wale watu wanaoletewa mwongozi ili kuwaokoa wanashindwa kumtambua. Katika kipindi hicho cha historia wanakuwa wamekwisha geuza picha ya kweli ya mwongozi wao wa dini na kuchukua picha ya bandia ya mawazo yao yasiyo na msingi. Wanaanza kutazamia kutokea mawazo yao na kugeuka katika sura ya kiwiliwili, ilhali kinachotokea ni kufanyika mara nyingine

---

[1] P.D.Ouspensky, 'A New Model of the Universe', k. 149 -150, Kegan Paul , Trench, Truberner & Co.,Ltd 1938

sawa na historia ya dini jinsi ilivyotendeka tangu alipokuja Mwongozi wa kwanza wa dini. Waongozi wa dini siku zote huja wakiwa wanadamu wanyenyekevu waliozaliwa na mama wazazi wa kibinadamu na wanachukuliwa kuwa wanadamu siku zote katika maisha yao. Ni baada ya muda mrefu sana wakiisha kufa habari ya kuwafanya miungu inaanza. Ndiyo maana kuwapokea mara moja wanapotokea tena kunakuwa hakuwezekani.

Watu wa dini wa aina hiyo wanapozikabili hakika za Waongozi wa dini wanaoonekana watu wanyenyekevu, wanawakataa moja kwa moja. Mnapotazamia ujaji wa kizimwi ama kizuka, mwawezaje kukubali ujaji wa mtu wa kawaida badala yake? Ndiyo sababu dunia imeshindwa kumwona na kumtambua Yesu Kristo katika ujaji wake wa mara ya pili, ilhali amekwisha kuja tayari mara ya pili.

Hilo ni dai kubwa pengine ambalo yaelekea litakataliwa katakata na wasomaji. Yawezekanaje aje Yesu na aondoke pia pasipo dunia kuitambua habari hii? Anawezaje kuondoka bila ya ulimwengu mzima wa Ukrito na Islam kumjua? Nyakati mamboleo zimewaona wadai wengi wa aina hiyo ambao walishtusha pia kwa muda na kuleta msukosuko, Lakini hao wote wako wapi leo?

Hizi ni zama ambamo katika nchi nyingine madhehebu yanatokea ghafula kama uyoga na madai mabovu ya kurejea kwa Yesu ama Yesu kumtuma mtangulizi wake yanafanywa huko na huko. Dai hilo nililosema pengine ni mojawapo katika madai hayo. Kwa nini mtu mtulivu apoteze nafasi yake hata kuifikiria kwa makini habari hiyo? Shaka halisi zitazalika na mashaka makubwa yatakabiliwa. Tungemwomba msomaji kuzingatia hali ya ujaji hasa wa Yesu. Je, ujaji wake ndiyo wazo tu la uwongo ama yeye kweli anaweza kufika tena duniani yeye mwenyewe binafsi ama kwa njia ya ujaji wa mtu mwingine badala yake anayefanana naye? Hilo ndilo swali linalopaswa kujibiwa kwanza kabla hatujaweza kujaribu kutoa majibu kuhusu mashaka kadha yaliyodokezwa juu. Je, ulimwengu, ukiwa wa Kikristo au wa Kiislam, upo tayari kweli

kiroho kukubali ujaji wa mara ya pili wa Yesu? Kama ndiyo, katika sura gani na kwa njia ipi? Tukiangali sawa na nadharia ya Waislamu na pia Wakristo, Yesu kama akija atakuja na shani kubwa na ishara zilizo wazi akiteremka kutoka mbinguni saa za mchana na malaika wa kumbeba, hata kwamba haitawezekana kwa hata mwenye mashaka sana kukataa kumpokea.

Ni masikitiko ya kwamba zama za leo ziko tayari kumpokea Yesu wa mawazo tu matupu ambaye mfano wake haujatokea asilani hapo kabla katika historia ya binadamu. Kama historia ya dini izingatiwe kwa makini, mtu atakuta mifano mingi sana ya waanzilishi wa dini au watawa wengine waliosemekana walipaa mbinguni na miili yao. Madai hayo ni mengi sana na yametapakaa huko na huko hata kwamba inaonekana ni maelekeo ya mtu kubuni hadithi za aina hiyo kuwakuza viongozi wa dini yake na kuwafanya kuwa zaidi kuliko binadamu. Swali lipo hapa ya kwamba tunawezaje kukanusha taarifa hizo zote zinazokubaliwa na kuaminiwa na pengine mabilioni ya watu leo katika dunia hii? Wakristo na Waislam pekee wanaoiamini hiyo na matukio mengine ya kipuuzi wapo zaidi ya bilioni mbili. Kwahiyo msomaji anaweza kuuliza ya kuwa tuna haki gani au mtu yeyote duniani ana haki gani kukatalia mbali madai hayo yote kwa kusema kuwa hayo siyo ya kweli, ni mawazo tu ya watu. Tunakubali ya kuwa kuichunguza habari hiyo kwa jiha hiyo kutahitaji juhudi kubwa ili kukanusha madai hayo kwani hayasaidiwi na maandiko ya dini ambazo zinafanya madai hayo. Mtu akiisha ongozwa kuingia katika mzingile huu wa maelezo haya au yale yanayowezekana, habari hiyo itaishia katika swali la kupendelea na kujichagulia maelezo fulani. Hapo hiyo itakuwa ni mchezo wa mtu yeyote kutoa tafsiri ya maneno yalivyo katika maandiko au historia ya dini ilivyoripotiwa au kuyaeleza kwa kuyafikiria kuwa mafumbo au mithali. Kukanyaga katika bwawa la matope la maelezo yanayopinzana hakutasaidia kupata shabaha. Hata hivyo kuna njia moja ya kutokea jambo hilo zito tunayoweza kuwaonesha wasomaji na kuwakaribisha kuifuata ama kuikataa

jinsi wapendavyo.
Hebu tukubali, kwa shabaha ya kuhoji tu, madai yote hayo ya viongozi wa dini kupaa mbinguni na kuyahesabu jinsi yalivyo kidhahiri. Kama kupaa Yesu mbinguni jinsi kulivyoripotiwa kuchukuliwe katika maana ya dhahiri na ujaji wake wa mara ya pili halikadhalika uhesabiwe kuwa ujaji wake hasa, hapo hapatakuwa na sababu yoyote ya kukatalia madai ya aina hiyo ya wafuasi wa dini nyingine kuhusu kupaa kwa viongozi wao mbinguni na kuteremka tena na kiwiliwili chao ardhini. Kwa nini tuwatenge tena Eliya, Mfalme wa Salemu, Imamu wa Kumi na mbili wa Mashia Ithna Ashariyya - dhehebu moja la Waislam, kupaa kwa miungu ya Wahindu na watukufu wengine na wale wanaochukuliwa kuwa madhihirisho ya Mungu? Kwahiyo ni afadhali zaidi kujiepusha na kubishana na wenye kuamini hivyo kwani mabishano hayo hayataleta manufaa yoyote bali yatapotea bure kabisa. Mtu anaweza kuwauliza hao wenye kuamini haraka simulizi pasipo ushuhuda ya kuwa je wanaweza kutuonesha hata mmojawapo miongoni mwa wanaoaminiwa walipaa hadi sehemu za mwisho za huko mbinguni kwamba aliwahi kurejea duniani mara ya pili yeye mwenyewe binafsi. Je, historia yote ya binadamu yaweza kutoa hata mfano mmoja wa mtu kurudi duniani mara ya pili aliyeripotiwa kupaa mbinguni pamoja na mwili wake? Tuonesheni basi kama upo mfano hata mmoja.
Kwa kuangalia kwamba madai ya kurejea duniani mara ya pili hayakutimia abadan hata mara moja, mtu anabakiwa na kuchagua jambo mojawapo katika haya mawili: Ama kukataa katakata madai hayo yakiwa ya udanganyifu, au kuyakubali hayo madai yakiwa mafumbo ama mithali jinsi Yesu alivyofanya kuhusu ujaji wa Eliya mara ya pili. Hapo panabainika ya kwamba wale wanaomngojea Yesu ateremke mwenyewe binafsi kutoka mbinguni wanajiwekea kinga baina yao na uhakika halisi wa Yesu. Kama Yesu akija tena, lazima atakuja akiwa mtu jinsi walivyotazamiwa waongozi wote kabla yake. Ikiwa anadhihirika leo akiwa mtu mnyenyekevu wa kawaida aliyezaliwa katika nchi

ifananayo na Judea katika Palestino na akapewa kazi ya mahubiri alivyofanya katika ujaji wake wa kwanza, je, wenyeji wa nchi hiyo watamtendea tofauti na vile alivyotendewa hapo kabla?

**MASIHI ALIYEAHIDIWA**

Hivyo ndivyo ilivyo habari ya ujaji wa mara ya pili wa Masihi tunayemwamini. Ilikuwa karibu miaka mia moja na kitu hivi iliyopita ya kwamba mja mnyenyekevu wa Mwenyezi Mungu, jina lake Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, alipashwa habari na Mungu ya kuwa Yesu Mnazareti, Mwana wa Mariamu, ambaye ujaji wake wa pili unangojewa na Wakristo na Waislamu kwa usawa, alikuwa nabii maalum wa Mungu aliyekwisha kufa tayari walivyokufa manabii wengine wote wa Mungu. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alitangaza ya kuwa Yesu hayuko hai kimwili wala hakupaa mbinguni akisubiri huko kurejea tena kuitembelea ardhi. Alikwisha kufa kama manabii wengine wa Mungu wala hakuwa zaidi ya nabii. Ujaji wa pili wa Yesu Kristo unaoaminiwa na Wakristo na Waislamu kwa pamoja ulimaanisha kutokea kiroho siyo kimwili. Ndivyo alivyoambiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad na Mungu. Na akapashwa habari pia ya kwamba Mungu amemtuma yeye ili kutimiza bishara hiyo.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alitokana na ukoo mmoja wenye heshima wa Panjab. Shughuli kubwa zaidi za ukoo wake zilihusikana na kujijenga kiutajiri na heshima, lakini yeye alijitenga na shughuli za kidunia na akapitisha wakati wake mwingi katika ibada ya Mungu na kutaali vitabu vya dini. Alikuwa mtu asiyejulikana katika dunia, hata katika kijiji alimozaliwa hakujukana sana. Kisha akaanza kujitokeza katika ulimwengu wa kidini nchini India kama mtu thabiti mwaminifu na shujaa mwenye kupigania miradi ya Kiislam. Akawa mwenye kujulikana kuwa mtu Mtakatifu sana hata kwamba si tu ya kuwa Waislamu

pekee walimheshimu bali hata wafuasi wa dini nyingine nao wakampa heshima sana. Watu wakaanza kushuhudia ya kwamba yeye anaongea na Mungu ambaye maombi yake yanapokelewa na ambaye huruma yake kwa wanadamu na kusumbuka kwake kwa shida za watu ni jambo la hakika kabisa lisilo na shaka.
Katika zama hizo, Islam katika India kwa bahati mbaya ilikuwa na hali mbaya mno. Hiyo ililengwa na wamishionari wa Kikristo ambao sawa na mfumo wa himaya ya Uingereza wakaanzisha vikali shughuli za siyo kuyashambulia mafunzo ya Kiislamu tu bali na Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam pia. Isitoshe, katika dini ya Kihindu, iliyo dini kubwa katika India, miendeleo iliyonuia kutaka makuu ilianza kuzalika iliyokuwa na mpango wenye ncha mbili: Kuhuisha utamaduni wa desturi za kihindu, na kufutilia mbali Islam na Waislamu nchini India kwa kueneza ya kwamba hao sio wananchi halisi bali ni wageni ambao hawana haki ya kuimarika katika nchi hiyo. Miongoni mwa miendeleo hiyo, mkali zaidi ulikuwa ni Mwendeleo wa Arya Samaj ulioanzishwa na Pandit Swami Dyanand Sarsvasti (1824-1883) mnamo mwaka 1875. Huo pengine ulimhimiza zaidi Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. kuanza kuchunguza sana mambo ya dini mbalimbali kwa shabaha ya kuitetea Islam.
Mtaala wake huo wa dini mbalimbali ukaimarisha zaidi imani yake katika ubora wa mafunzo ya Kiislam. Aliathirika mno na Kur'ani Tukufu jinsi ilivyoshughulikia matatizo ya binadamu. Aligundua ya kwamba Kur'ani baada ya kufundisha khulka bora haikuishia tu hapo, bali iliendelea kuleta hoja madhubuti za kiakili zilizosaidiwa na ushuhuda ya kwamba mafundisho hayo ndiyo yanayofaa sana kufuatwa katika hali kadha wa kadha.

Mwishowe mtaala wake huo ukamwezesha kuishindisha Islam ambayo katika zama hizo haikuwa na uwezo wa kujitetea. Hivyo basi, yeye alifanya kazi ya muhimu sana iliyohitajika kwa kuitetea Islam katika India katika zama hizo. Alianza kujulikana baina ya watu alipoanza kufanya maongezi na mijadala na makundi ya

watu wachache kwanza lakini eneo lake likapanuka pole pole. Akaanza kujulikana kote kote kuwa msimamizi wa miradi ya Kiislam aliye mwenye akili nyingi na mwenye kuogofya sana.
Katika zama hizo yeye akaanza kutunga kitabu kikubwa sana kuhusu utaalamu wa kidini. Kitabu hicho, Barahine Ahmadiyya, alinuia kuandika majalada yake hamsini. Lakini alipokuwa amekwisha chapisha majalada manne tu akapatwa na mambo kadha ambapo ikawa haikuwezekana kwake kuendelea na kazi ya kitaalamu mpaka mwisho. Hata hivyo aliandika vitabu vingi kwa kulingana na haja za wakati huo. Vitabu vyake vilieleza yote yale aliyokuwa amenuia kuyaandika mwanzoni bali na zaidi pia. Kwa kweli akatimiza zaidi ya ahadi yake ingawaje siyo kwa jina hilo la Barahine Ahmadiyya. Inashangaza aliwezaje kuandika vitabu vingi hivyo peke yake bila kupata msaada sana wa kikarani. Vitabu, nyaraka na makala alivyowahi kuandika ni takriban mia moja na kumi hivi.
Siyo tu maandiko yake ya kitaalamu yaliyompa umashuhuri sana katika Bara Hindi zima, bali sifa zake za kiroho pia zilikuwa ni sababu kubwa ya yeye kujulikana sana na kuheshimika.
Katika hali hiyo ya yeye kuzidi kupata heshima Mungu akamtuma ili kubeba wajibu mzito wa kuwa Mwongozi mrekebishaji wa zama za mwisho aliyekuwa anatazamiwa na kungojewa na karibu dini zote za dunia. Kwa kulingana na nadharia ya Waislamu yeye alikuwa Al-Mahdi, msuluhishi aliyeongozwa na Mungu. Na kulingana na itikadi ya Kikristo na Waislamu yeye aliinuliwa kwa daraja la kuwa Masihi Aliyeahidiwa ili kutimiza bishara za ujaji wa mara ya pili wa Yesu Kristo. Lakini kutumwa huku kulisababisha yeye kupoteza umashuhuri wake na kupendwa kwake na watu, hali aliyokuwa nayo hapo kabla. Papo hapo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alitengwa na kukataliwa si tu na wafuasi wa dini nyingine bali vikali zaidi na Waislamu wenyewe wa India ambao yeye alikuwa anaitetea dini yao kwa bidii kubwa mno.

Tuseme yeye alizaliwa upya kiroho. Jinsi alivyokuja duniani akiwa peke yake, ndivyo alivyoanzia uhai mpya akiwa peke yake katika ulimwengu wa kidini, akiisha achwa kwa kitendo na watu wote waliokuwa pembeni mwake. Lakini Mungu hakumwacha. Akahakikisha mara kwa mara kupatiwa msaada wa Mungu kwa njia ya Wahyi aliofunuliwa katika muda alipofanyiwa uadui mkali sana. Wakati mwingine alifunuliwa yafuatayo:

> Mwonyaji mmoja alikuja duniani, lakini dunia haikumpokea; lakini Mungu atampokea na atadhihirisha ukweli wake kwa mashambulio makali.
>
> Mimi nitafikisha ujumbe wako hadi pembe za dunia.

Hizo ni baadhi ya funuo zake zilizomsaidia na kumpa nguvu katika hali alipokuwa peke yake na ambapo alikataliwa na wapinzani wake. Sasa miaka zaidi ya mia moja imepita, na mambo yaliyodhihirika polepole na kwa mfululizo yanahakikisha ukweli wa madai yake na bishara zake na ukweli wa funuo zake.

Mtu huyo aliyekuwa mmoja tu pekee sasa wafuasi wake walio zaidi ya milioni kumi wanapatikana katika nchi mia moja na thelathini na nne wakitawanyika katika mabara matano. Ujumbe wake umekwisha fika hadi pembe za dunia, kutoka Magharibi ya mbali hadi Mashariki ya mbali. Anakubaliwa kuwa Kiongozi Mwongofu na Masihi Aliyekuwa Ameahidiwa kuja mara ya pili, katika Marekani, katika Yuropa, katika Afrika, katika Asia, hata katika visiwa vilivyo mbali sana vya bahari ya Pasifiki ya kusini-mashariki, kama vile Fiji, Tuvalu, visiwa vya Soloman na kadhalika. Hata hivyo wafuasi wake wanaweza kufananishwa na kidimbwi kidogo kulingana na bahari kubwa ya ulimwengu wa Kikristo.

Ufaulu wa Jumuiya ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s unahitaji maelezo marefu lakini nafasi tuliyo nayo ni ndogo. Hata hivyo ni jambo la kuzingatia ya kwamba hakuna mwendeleo wowote wa kidini katika zama hizi ulio imara, uliosonga mbele

na kuenea haraka kwa hatua hii. Hiyo siyo dhehebu wala kitu kinachotamaniwa sana lakini kwa muda. Huo ndiyo ujumbe wa maana sana - kazi ngumu inayohitaji bidii kubwa na maadili kwa wale wanaothubutu kuufuata. Wanaoufuata, kwa hakika, wanafanya hivyo kwa kukubali wajibu mzito wanaotakiwa kutimiza maisha yao mazima. Huo ni mgumu kama ilivyokuwa jamii ya kale ya Waesseni. Kuupokea siyo kusuhubiana katika hali ya raha, bali ahadi ya kutimiza maisha mazima. Wanaoingia katika Jumuiya hii wanalazimika kutengana na furaha zisizofaa katika maisha, siyo kama ulivyo mtindo wa wale wanaojinyima hata furaha za halali au wale wanaoitwa Watawa wanaokaa katika upweke pasipo kuoa na kadhalika, bali kwa imani thabiti, kujitolea sana na utulivu wa moyo unawawezesha kutoa dhabihu na kuvumilia shida kwa wema wa hali ya juu sana katika njia hii. Yeye aliunda Jumuiya inayopatikana duniani kote ambayo haina kifani chake katika kutoa sadaka ya mali sana. Wanajumuiya wote wenye mapato wanajilazimisha kutoa kwa uchache sehemu ya kumi na sita ya mapato yao katika njia hii njema. Roho ya kujitolea mhanga na kiasi cha bidii inayofanywa duniani kote inashangaza mno. Hata hivyo hayo yote yanatendwa pasipo kushurutishwa hata kidogo. Wale wanaoweza kutoa sehemu ya bidii yao na sadaka ya mali yao hujihesabu kuwa ni wenye bahati njema sana. Hiyo ni Jumuiya inayojitegemea kabisa katika mambo ya fedha. Mpango huo wa kuchanga mchango kwa hiari unaendelea kufanya kazi duniani kote tangu miaka mia moja iliyopita kwa uaminifu wa hali ya juu sana na wema mwingi kabisa. Humo ndimo imo siri ya ufaulu wake katika kujitegemea pasipo kuathirika na sababu za nje kwa zaidi ya karne moja. Lakini hiyo ndiyo jiha moja tu ya kuiangalia Jumuiya hii. Kuangalia sifa za Wanajumuiya wake kwa jiha nyingine kunaleta picha ya kuvutia mno. Hii ndiyo Jumuiya inayojulikana kwa khulka zake njema, kukaa kwa amani, kupendana na kuheshimu sana khulka za kibinadamu. Hii ndiyo Jumuiya ya dini inayosifiwa sana duniani kote kwa sababu inaiheshimu sheria ya nchi na kuthamini

kuhusiana na watu bila kujali dini, rangi na imani.
Msomaji anaweza kufikiria pengine ya kwamba tumetoka nje na kuingia katika habari isiyohusikana na madhumuni yenyewe tuliyokuwa twazungumzia. Hebu tumdokezee msomaji huyo kwa heshima ya kwamba yeye amekosa shabaha. Habari hiyo itaonekana inalingana na madhumuni tuliyokuwa twazungumzia kama tukizingatia kauli hii ya Yesu Kristo ya kwamba mti hujulikana kwa matunda yake.[2]

Kama kuna mtu leo anayependa kweli kuhakikisha ukweli wa madai ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. hicho ni kipimo kinachoweza kutegemewa kabisa. Sawa na kipimo hicho inawezekana kuamua ya kwamba yeye alikuwa kweli Masihi Aliyeahidiwa ambaye ujaji wake ulitabiriwa si tu na Yesu Kristo bali na Mwanzilishi Mtukufu wa Islam pia. Kugundua kwamba yeye alizalisha wafuasi wa aina gani na karne moja iliyopita iliwatendeaje itakuwa ni kazi ya kufaa sana. Swali litazuka pia ya kwamba je, wanatendewa na zama jinsi walivyotendewa wafuasi wa Yesu Kristo katika karne ya kwanza ya Kikristo? Tena hakuna budi swali lizuke ya kwamba na Mungu Alimtendeaje Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wakati alipojaribiwa kuangamizwa na kufutiliwa mbali yeye na Jumuiya yake? Je, Mungu aliitendea kwa upendo Jumuiya hiyo iliyokuwa inasakwa ama akaitendea kinyume chake? Je, kama Wakristo wa kale, wafuasi wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. pia walipata kusaidiwa na Mungu katika shida? Ikiwa kila mara walipoteswa na kusagwa kwa dhuluma badala ya kusagika tikitiki wakajitokeza wakiwa wengi zaidi na wenye nguvu maradufu na heshima nyingi kuliko

---

[2] Ufanyeni mti kuwa mzuri na matunda yake kuwa mazuri; au ufanyeni mti kuwa mbaya na matunda yake mabaya, kwa maana kwa matunda yake mti hutambulikana. (Mathayo 12:33).

zamani, hapo bila shaka madai ya mdai kama huyo hayawezi kupuuziliwa mbali kama jambo lisilo na maana. Hayo siyo madai makubwa ya mwendawazimu, au mawazo ya kupendeza ya mtu azoeaye kuwaza mambo yasiyo ya kweli. Uahmadiyya umeisha kuwa hakika inayotakiwa kutiwa maanani sana zaidi kuliko Ukiristo ulivyoonekana mwishoni mwa karne yake ya kwanza.

Hapa pana habari ya Masihi aliyekuwa kweli ya historia wala hakuwa mazao ya ngano, na hapa tena pana habari ya Masihi ambaye ujaji wake mara nyingine ulikuwa hakika halisi jinsi ulivyokuwa ujaji wake wa mara ya kwanza akiwa ametumwa kuwa mwongozi wa dini. Sasa ni juu ya watu wa zama hizi kujichagulia kuendelea kuishi katika ulimwengu wa simulizi na mawazo yasiyo na msingi na kudumu kuwangojea viongozi walioahidiwa na dini na imani zao au kuzikubali hakika halisi za maisha haya. Jambo moja lazima tulikubali ya kwamba viongozi wengi wa dini wamekwisha pandishwa kutoka cheo cha kawaida cha binadamu hadi cheo cha kuwa miungu. Mara nyingi viongozi wa dini walifikiriwa kupaa mbinguni kusubiri huko katika kona za mbali sana angani ili kuja tena kuitembelea sayari ya Ardhi. Hakuna sababu kwamba mtu alikubali dai moja la aina hiyo na kuyakatalia mengine ya aina hiyohiyo, kwani ni madai matupu pasipo uthibitisho halisi wowote wa kisayansi kuhakikisha ukweli wake. Basi hakuna hiari yoyote isipokwa tu kuyakubali yote hayo ama kuyakataa yote kwa jumla. Hiyo itakuwa njia ya kutenda uaminifu na uadilifu. Naam, lipo jambo moja la hakika sana ya kwamba walipokwisha ondoka dunia hii, bila kujali waliaga kwa njia ipi sawa na imani ya wafuasi wao, kamwe hawakurejea duniani humu hata mmoja wao katika historia nzima ya binadamu. Aidha, ni jambo la hakika kabisa pia ya kwamba watawa na viongozi wote wa dini walionyanyuliwa kwenye cheo cha kuwa miungu au washiriki wa Mungu walianzia maisha yao kama watu wa kawaida hadi walipokufa. Ni wafuasi wao tu waliowafanya kuwa miungu. Lakini kumbukeni hata mmoja kati yao hakuonesha

kuwa anashughulikia kazi ya kuendesha kanuni za asili za ulimwengu. Daima Yupo Mmoja tu anayeonekana anaendesha na kutawala kanuni za ulimwengu. Kioo cha mbingu na kanuni za asili za ulimwengu vinaonesha uso wa Mungu Mmoja tu pekee. Kurani Tukufu inasema:

> Nao husema: Rahmani Amejipangia mwana. Bila shaka mmeleta jambo lichukizalo. Karibu mbingu zitatuke kwalo na ardhi ipasuke na milima ianguke vipande-vipande, kwa sababu wamemdaia Rahmani kuwa na mwana. Wala haimpasi Rahmani kupanga mwana. (19:89-93)

**MWISHO:**

Ama kuhusu swali hilo, twaona tumekwisha lieleza vya kutosha. Lakini kabla hatujamalizia habari hiyo, twapenda kuwasihi Wakristo kwa jazba kubwa waachane na mawazo yao ya kujifurahisha yasiyo na msingi na kukubali hakika ngumu za maisha.

Yesu Kristo alikuwa mtu mkamilifu kulingana na zama zake, lakini hakuwa zaidi ya binadamu. Alifikia ule upeo aliokuwa amekadiriwa kuufikia akiwa nabii maalum wa Mungu aitwaye Masihi. Jambo hilo likamfanya kuwa wa pekee kati ya manabii waliokuja baada ya Musa hadi alipokuja yeye.

Kwa hakika kila nabii alikabidhiwa kazi ngumu kuitekeleza.

Wanalazimika kuwarekebisha watu ambao wanageuka kuwa wabaya moja kwa moja. Kwa Yesu, kazi yake hiyo ilikwa ngumu zaidi kwani si tu kwamba yeye alitakiwa kupigana na maovu ya kawaida ya jamii, bali pia alipaswa kuleta mabadiliko ya kimapinduzi katika mwendo wa Wayahudi.

Kama inavyofanyika kwa wafuasi wa kila dini ya kwamba wanaanza kupotoka njia polepole wakiachana na ukweli na kuhangaika katika nyika za dhambi, ndivyo ilivyotendeka kwa Wayahudi pia. Wakati alipodhihirika Yesu, hao walikuwa kwa dhahiri wamekwisha kufa kiroho. Maji ya uhai wa dini yalikuwa yamekupwa, kwa kuacha nyuma nyoyo ngumu kama mawe zilizokwisha kufa. Kazi aliyokuwa amepewa Yesu ilikuwa kuzigeuza hizo kuwa nyoyo za binadamu zinazodunda na kububujisha kutoka humo chemchem za huruma ya kibinadamu. Huo ulikuwa mwujiza alioutenda Yesu na humo mnapatikana ukuu wake.

Sasa Waislamu na Wakristo wakiwa pamoja wanapomngojea Yesu Kristo aje mara ya pili duniani, wanapaswa wasisahau ya kwamba Yesu aliyekusudiwa kuja analazimika kuwa Yesu yule kisifa na kikazi ya dini. Walakini sawa na bishara za Mwanzilishi wa dini ya Kiislamu, Mtume Muhammad s.a.w., Yesu huyu alitakiwa kuja mara ya pili si katika ulimwengu wa Kikristo bali katika ulimwengu wa Kiislamu. Na safari hii ni nyoyo za Waislamu wa zama za mwisho atakazopewa kuzigeuza na kuzirekebisha. Muradi huo wa ujaji wake wa mara ya pili unaungwa mkono na baadhi ya bishara nyingine za Mtume s.a.w. Yeye alitabiri ya kwamba hali za Waislamu katika zama za mwisho zitafanana kabisa na hali za Wayahudi walipokuwa wamekwisha haribika, jinsi kiatu kimoja kinavyofanana sana na kiatu cha pili cha jozi hiyo moja.

Hivyo kama maradhi ni yale yale, basi na tiba pia ni ile ile. Masihi hana budi kurejea duniani akiwa mtu mnyenyekevu, siyo mtu yuleyule binafsi bali kiroho na kisifa, na ndivyo hivyo ilivyofanyika kwa kitendo. Watu wa dini kama hao wanaokuja kuleta mapinduzi ya kiroho daima huzaliwa katika hali ya kutokujulikana na huwa watu wapole wanyenyekevu na wanaishi maisha kwa unyenyekevu. Hao wanarejea katika dunia kuitembelea kabisa kwa njia hiyo na wanatendewa pia kikatili na kwa chuki na uadui mkali sana. Hawatambuliwi kwa urahisi kuwa

ni wajumbe wa wale walioahidi kurejea tena.

Alivyotendewa Kristo mara ya kwanza na Wayahudi, ndivyo hivyo alivyolazimika kutendewa mara ya pili lakini safari hii kwa mikono ya Waislamu na Wakristo waliokuwa wakingojea kurejea kwake. Matumaini yaleyale yaliyopindama yasiyo ya kweli, shabaha zilezile za kuwaza zisizo za hakika alizotazamiwa kuzifuata, nadharia zilezile zisizokuwa sawa za kazi zake na ufaulu wake hapa ardhini, vyote hivyo jinsi vilivyodhihirishwa na Wayahudi wa zama za Yesu Kristo, ndivyo vilivyotakiwa kurudiwa na Waislamu katika zama za ujaji wake wa mara ya pili. Na kwa njia hiyo historia ilitakiwa kujirudia mara nyingine.

Kwa kuangalia nyuma, mtu anaweza kutambua vizuri zaidi sababu za Wayahudi kushindwa kumtambua Masihi wao. Twaweza kuzingatia kwa urahisi shida yao na kujifunza kutokana na msiba wao. Kuchukua maana ya dhahiri ya maandiko yao kuliwapoteza. Hayo yote yamekwisha zungumzwa tayari, lakini ili kusisitiza habari hiyo twaikumbusha tena. Siku zote inafanyika hivi katika historia ya viongozi wa dini wanaotazamiwa kuja ya kwamba watu wao wanaowangojea zaidi, mara nyingi wanashindwa kuwatambua, kwani alama za utambuzi wao zinasomwa vibaya na zinatambuliwa vibaya. Mambo ya hakika yanageuzwa kuwa ya kubuni, na mafumbo na mithali huchukuliwa katika maana ya dhahiri.

Yote hayo takriban yamerudiwa wakati wa ujaji wa mara ya pili wa Masihi, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wa Qadian. Jinsi alivyotazamiwa Eliya kuteremka kutoka mbinguni na Wayahudi wa zama za Yesu Kristo, ndivyo mtu fulani alivyokuwa anatazamiwa kushuka kutoka mbinguni mara nyingine tena, naye alikuwa Masihi Mwenyewe safari hii.

Wayahudi walikuwa wanamtazamia Masihi kufika katika utukufu na kuwaongoza kwenye zama mpya za kupata utawala na kuwashinda mabwana zao wa Kirumi. Matumaini hayo yote yalivunjika tikitiki alipofika Yesu wa Nazareti. Maana, kwa vyo vyote alipofika, alionekana mbali sana na ile picha waliyokuwa

wamechora katika mawazo yao tangu karne nyingi kuhusu ujaji wa Masihi.
Ni jambo la kushtusha ya kwamba matukio kama hayo yametukia sasa ambapo amekuja Kristo kwa sura ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian. Waliyotenda wapinzani wake ndiyo yale yale isipokuwa majina ndiyo tofauti. Waislamu kwa jumla na Wakristo kwa pamoja wameshikilia kazi ya Wayahudi wa zama za Yesu. Upinzani ni uleule. Hoja za kumkataa ndizo zilezile. Hata hivyo alimtendea mja wake huyu mnyenyekevu kwa kumpatia ishara kubwa zaidi za kumsaidia kuliko Yesu wa zamani na kumsaidia yeye kueneza ujumbe wake haraka zaidi katika nchi nyingi zaidi na katika mabara yote ya ardhi. Hayo ndiyo mambo ya kweli yaliyo dhahiri shahiri, lakini kwa wale wenye masikio ya kusikia. Hayo ndiyo mambo ya kweli ambayo yanaendelea kudhihirika waziwazi pamoja na kupita wakati, lakini kwa wale tu wanaojali kuangalia.
Isitoshe, kiini cha ujumbe wa Masihi kulingana na hali za sasa za Waislamu na Wakristo siyo tofauti. Lakini wataufahamu wale ambao hawatafumba macho yao.

Hebu mwishowe niwakumbushe Wakristo na Waislamu wanaongojea ujaji wa mara ya pili wa Kristo tangu karne nyingi zilizopita, maneno aliyonena Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, aliyefanywa na Mungu kuwa Masihi wa zama za mwisho, ambayo ndiyo yafuatayo:

> Kumbukeni ya kwamba hakuna atakayeshuka kutoka mbinguni. Wapinzani wetu wote walio hai wakati huu watakufa wote wala hamna kati yao yeyote atakayemwona Yesu mwana wa Mariamu akishuka kutoka mbinguni. Kisha wazao wao watakaobaki nyuma yao nao watakufa, wala hamna kati yao vilevile yeyote atakayemwona Yesu mwana wa Mariamu akiteremka kutoka mbinguni. Kisha wazao wa wazao wao pia watakufa wala hawatamwona Yesu mwana wa Mariamu akishuka kutoka mbinguni. Ndipo Mungu atawatilia nyoyoni mwao fadhaa ya kwamba zama za utawala wa msalaba pia zimekwisha pita, na hali ya dunia imebadilika tayari, lakini mwana wa Mariamu

> hajateremka kutoka mbinguni. Ndipo wenye busara watachoka mara moja na imani hiyo: Na haitapita karne ya tatu tangu leo hii hata kwamba wamngojeao Yesu, wakiwa Waislamu na Wakristo, kwa kukata tamaa na kudhania vibaya wataachana na imani hiyo mbovu.[3]

Basi mwaweza kusubiri hadi kizazi kipya kizaliwe. Hao nao watangojea mpaka mwisho na kizazi kingine kipya kitashika mahali pao. Hali hiyo ya kungojea yaweza kuendelea hadi siku ya mwisho, lakini hakuna Yesu atakayeteremka kimwili kutoka mbinguni. Fikara zao kuhusu ujaji wake binafsi kimwili hazitasadikika kamwe, hata wakitamani sana namna gani kurejea kwake. Wanaweza kujijengea ukuta wa vilio jinsi walivyofanya Wayahudi miaka elfu tatu iliyopita. Na wanaweza kugonga vichwa vyao kwenye ukuta huo. Lakini jinsi ilivyotendeka kwa Wayahudi, ndivyo itakavyotendeka tena. Hawatamwona Masihi yeyote kushuka juu ya maombolezo yao kizazi hata kizazi hata kizazi. Matumaini yao ya ujaji wa Kristo katika siku zijazo hayatazalisha chochote ila patupu. Hayo ni matazamio matupu kabisa.

Ama kwa Wakristo wale wanaomchukua Kristo kuwa mwana wa Mungu katika maana ya dhahiri, twamaliza maelezo haya kwa kutoa maonyo ya Kurani Tukufu ambayo ni kitabu cha Mungu kilichofunuliwa kwa Mtume Mtukufu wa Islam. Hicho kinaeleza shabaha ya ujaji wake kikisema:

> Yeye (Mtume Mtukufu wa Allah) awaonye wale wanaosema: Mungu Amepanga Mwana. Wao hawana elimu ya jambo hili, wala baba zao. Ni neno kubwa litokalo katika vinywa vyao; hawasemi ila uwongo tu. (18: 5-6)

---

[3] Ruhani Khazain, J 20: Tadhkiratush Shahadatain uk 67

## NYONGEZA I

Orodha ya baadhi ya vitabu vinavyotaja habari za Marhamu ya Yesu pamoja na kueleza ya kuwa marhamu hiyo ilitengenezwa kwa ajili ya Yesu, yaani kwa kumtibu majeraha yake. Tafadhali kumbukeni ya kuwa kwa jumla vitabu vinavyoeleza hayo ni zaidi ya elfu moja. Hapa chini twataja baadhi yake:

*Qanun*, na Shaikh-ul-Rais Bu Ali Sina, J 3, Uk 133.
*Sharha Qanun*, na Allama Qutb-ud-Din Shirazi, J 3.
*Kamil-us-Sunnat,* na Ali Bin Al-abbas Al-Majusi, J 3. Uk 602.
*Kitab Majmua-e-Baqai,* Muhammad Ismail Mukhatif az Khaqan, na Khitab pidar Muhammad Baqa Khan, J 2, uk 497.
*Tadhkirai Ulul-Albab,* na Sheikh Dawud-ul-zarir-ul-Antaki, uk 303.
*Qarabadin-i-Rumi,* kilichokusanywa katika zama zilizo karibu na Yesu na kilifasiriwa katika enzi ya mamun al - Rashid katika Kiarabu, angalia habari ya marahamu hiyo chini ya Skin Diseases.
*Umdatul - Muhtaj,* na Ahmad bin Hasan Al-Rashidi al-Hakim. Katika kitabu hiki *Marhamu* ya Yesu na dawa nyingine zimetajwa kutoka katika vitabu mia bali zaidi ya mia. Vitabu hivyo vyote viko kwa kifaransa.
*Shifaul-Asqam,* J 2, uk 230.
*Mir'atush-Shifa,* na Hakim Natho Shah - (Muswada) Skin Diseases.
*Zakhira-i-Khawarazm Shahi,* Skin Diseases.
*Sharha Qanun Gilani,* J 3.
*Sharha Qanun Qarshi,* J 3.
*Qarabadin, na Ulwi Khan,* Skin Diseases.
*Ilajul Amradh,* na Hakim Muhammad Sharif Khan Sahib, uk 893.
*Qarabadin Unani,* Skin Diseases.
*Tuhfatul - Muminin,* kwenye hashiya ya Makhzanul - Adwiya, uk 713.
*Muhfit fi Tibb,* uk 367.
*Aksir-i-A'dham,* J 4, na Hakim Muhammad Adham Khan Sahib, Al-Mukhtabba ba Nadhim-i-Jahan, uk 331.
*Qarabadin*, na Masumi-ul-Masum bin Karamu-Din Al-Shustri Shiraz.
*Ijala-i-Nafiah*, na Muhammad Sharif Dehlavi, uk 410.
*Tibbi-Shibri,* yajulikana pia kwa jina Lawami Shibriyya, na Seyid Hussain Shibr Kazimi, uk 471.
*Makhzan-i-Sulaimani*, tafsiri ya Iksir Arabi, uk 599, na Muhammad Shams-ud-Din wa Bahawalpur.

*Shifa-ul-Amradh,* tafsiri ya Maulana Al-Hakim Muhammad Nur Karim, uk 282.
*Kitab Al-Tibb dara Shakohi,* na Nur-ud-din Muhammad Abul Hakim, Ain-ul-Mulk Al Shiraz, uk 360.
*Minhaju-ud-Dukhan ba Dastur-ul-A'yan fi Amal wa Takrib al - Nafiah lil-Abdan*, na Aflatun-i-Zamana wa Rais-i-Awana Abdul Mina Ibn nasrul-Ataa Al-Israili Al-Haruni (yaani Myahudi) uk 86.
*Zubdatul-Tibb,* na Seyid Al-Imam Abu Ibrahim Ismail bin Hasan-ul-Husaini Al-Jurjani, uk 182.
*Tibb-i-Akbar,* na Muhammad Akbar Arzani. uk 242.
*Mizan-ul-Tibb,* na Muhammad Akbar Arzani, uk 152.
*Sadidi,* na Rais-ul-Mutakallimin Imamul Muhaqqiqin Al-Sadid-ul-Kaz-runi, J 2, uk 283.
*Hadi Kabir,* na Ibn Zakariyya, Skin Diseases.
*Qarabadin,* na Ibn Tilmidh, Skin Diseases.

Orodha hiyo hapo juu imenakiliwa kutoka kwenye ‘Jesus in India’ kilichoandikwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, Masihi Aliyeahidiwa, uk 56-57.

## NYONGEZA II

**Parthenogenesis:** Kuzaa bila ya kuingiliana, yaani 'yai' la kike kukua na kufanyika kiumbe pasipo kushika mimba kwa kuchanganyika na mbegu za kiume.

Parthenogenisis ni jambo la kawaida katika ulimwengu wa vijidudu na pia katika samaki, na ni desturi katika vijidudu vile kama nzi wa kijani kibichi (greenfly) wanaoharibu mimea. Miongoni mwa wanyama watambaazi, jambo hili linaweza kufanyika kati ya mijusi katika mahali penye kunyesha kidogo sana mvua pasipo kutabiriwa.[1]

Katika Lancet mnamo 1955 iliripotiwa ya kwamba mama mmoja alizaa binti ambako parthenogenesis haikuweza kukanushwa. Jambo hili limefanyizwa kimajaribio katika wanyama wanaonyonyesha watoto wao. Lakini hatuna taarifa ya uzazi katika wanyama wanyonyeshao kwa njia ya parthenogenesis. Kwa wingi, ufaulu umepatikana kiasi hiki ya kwamba panya na sungura walishika mimba kwa njia hii na mimba ikapata kukua mpaka nusu yake lakini kisha mimba ikaharibika.

Kati ya wanadamu hivi majuzi uchunguzi ulifanywa juu ya 'Parthnogenesis kufanyika na kuchunguzwa kimpango na ukuaji wa 'yai' la kibinadamu mapema.'[2] Katika uchunguzi huo, 'mayai' ya mwanamke yalichukuliwa, lile liliokuwa limefanyika tu na lile lililogusana na mbegu za kuime lakini halikushika mimba na yote mawili yalibenuliwa kwa *ionophore* ya dawa ya *alcohol* au *calcium* na yakachunguzwa kushuhudia yaliofanyika. Matokeo ya uchunguzi huu yalikuwa ya kwamba upo uwezekano wa 'yai' la mwanamke kushika mimba kwa njia ya parthenogenesis kwa kutumia *ionophore* ya *calcium,* lakini kidogo zaidi kuliko inavyoshuhudiwa katika panya. Parthenote za mwanamke zaweza kukamilisha mgawanyiko hadi hatua ya seli 8. Hayo yanaleta uwezekano ya kwamba mimba iliyoharibika mapema inaharibika kwa sababu ya 'mayai' yaliyoshika mimba ghafula kwa njia ya parthenogenesis.

Tukio moja la parthenogenesis nusu nusu liliripotiwa katika gazeti la *New Scientist* la tarehe 7 Oktoba 1995 chini ya kichwa cha maneno, *'The boy whose blood has no father'*[3] (Yaani mtoto ambaye damu yake haina baba mzazi). Katika wanaume seli zote zinatakiwa kuwa na Y Kromosom moja,

---

[1] Genetics : 1991 September : 129 ( 1 ): 211-9

[2] Fertility - Sterility - 1991 Novemba; 56 (5) : 904-12.

lakini seli nyeupe za damu ya mvulana huyo zilingunduliwa kuwa na XX Kromosom pekee. Mwenye kutoa ripoti anaeleza pia ya kwamba mara moja moja kike cha kromosom kinakuwa na X kromosom moja iliyomo humo pia kijine (gene) cha kiume, na wachunguzi kwanza walidhani ya kwamba mfano huu wa mvulana ndiyo mfano wa alama zinazoashiria kwenye hali hiyo isiyo ya kawaida. Lakini walipotumia ufundi mwepesi sana wa DNA hawakuweza kugundua hata Y kromosom moja katika seli nyeupe za damu ya mvulana huyo. Hata hivyo ngozi ya mvulana iligunduliwa kuwa tofauti isiyolingana na damu yake, maana ilikuwa na kromosom X na Y pia.

Uchunguzi zaidi wa X kromosom katika noizi na damu ya mvulana ulitoboa ya kwamba X kromosom zake zote zilikuwa zinafanana kabisa na zilitokana na mamake peke yake. Kadhalika sehemu zote mbili za jozi nyingine 22 za kromosom pia zilikuwa zinafanana moja kwa moja, na zote zilitokana na mamake. Maelezo yaliyotolewa na wachunguzi ni kwamba 'yai' lisiloshika mimba likaanza kujigawa katika seli zifananazo; kisha seli mojawapo ikapatwa na mbegu ya baba mzazi, basi mchanganyiko wa seli hizo ukaanza kukua kama mimba ya kawaida. Jambo hili linahakikisha ya kwamba seli zinafanyizwa kwa njia ya parthenogenesis katika wanyama wanyonyeshao siyo kila mara zinalemaa. Katika mfano wa mvulana huyo hizo ziliweza kufanyiza utaratibu wa kawaida wa damu.

HERMAPHRODITISM:

Mtu kinyume cha kawaida anakuwa na sehemu zote mbili za uzazi, ya kiume na ya kike pamoja. Sehemu zake za nje zina dalili za yeye kuwa wa kike na wa kiume, na kromosom zake zinaonyesha mchanganyiko wa kiume na kike (XX/XY).

Katika uchunguzi mmoja huko Netherlands mnamo mwaka 1990 ulioitwa 'Combined Hermaphroditism and Auto-fertilization in Domestic Rabbit', sungura mmoja aliyekuwa Hermaphrodite (huntha) kweli aliwapanda sungura wengi majike. Matokeo yake ni kwamba hao majike wakazaa watoto 250 ambao kati yao walikuwapo majike na madume pia. Katika majira mengine ya kuzaa, huyo sungura huntha ambaye alikuwa amewekwa upweke pasipoweza kugusana na sungura wengine, akatunga mimba na hatimaye

[3] Ripoti hii inahusiana na uchunguzi wa David Bonthron na wengineo na unarejeza kwa toleo la Octoba 1995 la *Nature Genetics* ambamo ripoti hii inapatikana.

akazaa sungura majike na madume saba kwa jumla. Mchanganyiko wa kromosom ulionyesha idadi kubwa ya *Autosomes* na kromosom mbili zisizobainika vizuri kuwa ni za kuime ama za kike.
Uchunguzi ulifanywa juu ya mtu-huntha katika idara ya Obstetrics and Gynaecology, Chicago, Lying-in Hospital, Illinois.[4] Shabaha ya uchunguzi huo ilikuwa kuhakikisha matukio yanayosababisha huntha wa kweli mwenye 46xx, 46xy kupatikana na kuripoti mimba ya kwanza katika huntha halisi mwenye 46xx, 46xy aliye na sehemu za kike na kiume za uzazi.
Mpango wa uchunguzi huu ulioshughulikia kuchunguza Kromosom uliofanywa juu ya *Iymphocytes* za mgonjwa, na antigenes za seli nyekundu, *Ieucocytes antigene* za binadamu na kuwepo kwa *y-kromosom deoxyribonucleic acid* zilichanganuliwa. Matokeo yake yalilinganishwa na vifungu vya damu ya baba mzazi na ndugu na dada zake.
Natija ya uchunguzi huo ilihakikisha ya kwamba mgojwa wetu ni kitu chenye uhai ambamo mna aina mbili kwa uchache za matengenezo ya seli yanayohitilafiana katika umbo la kiuzazi, na kwahiyo mgonjwa wetu huyo anatenda kazi mbili za baba na mama pamoja. Isitoshe, juu ya kuwa na sehemu mbili, uke na uume, yeye alishika mimba na akazaa mtoto.

---

[4] Journal of Fertility and sterility - JC : evf 57(2) : 346 - 9 1992 Februari.

*Siyo kazi ya mwandishi au mhubiri wa Kikristo kufifisha Ukristo ili uwafae watu wote walioelimika. Itikadi ya Mungu kuzaliwa kwa sura ya mtu - Yesu ilikuwa kikwazo kwa Wayahudi na upumbavu kwa Wagiriki na ndivyo itakavyokuwa siku zote, kwani itikadi hiyo si tu kwamba inaruka mipaka ya akili, hiyo ni fumbo la hali ya juu sana na inaweza kuyakinishwa kwa imani tu kwa harara ya ndani na moyo wa kupenda. Kutia akili mahali pa imani kunamaanisha kifo cha Ukristo.*

Keirkegaard